# Nipashe

Ijumaa Januari 10, 2020 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0580124

www.ippmedia.com

The Guardian digital | nipasheTZ | nipasheTZ | nipasheTZ | 0745 700710




## DC asimulia askari alivyojitoa muhanga kuzima valvu ya mafuta

UKURASA 4




UKURASA 13

**MATOKEO KIDATO CHA 4:**

# KILIO, KICHEKO

**WASICHANA** wawagalagaza tena wavulana, mikoa iliyofanya vizuri, vibaya yaanikwa, aliyeongoza kitaifa afunguka... *Endelea ukurasa wa 2 & 3*



Joan Titte

### Shule 10 bora kitaifa

- Kemebos
- St Fransis Girls
- Feza Boys
- Canossa
- Anwarite Girls
- Precious Blood
- Marian Boys
- St. Augustine Ragaste
- Maua Seminari
- Musabe Boys



Katibu Mtendaji wa Necta, **Dk. Charles Msonde**

### Wanafunzi 10 bora kitaifa

- Joan Titte (St. Francis Girls)
- Denis Kinyange (Nyegezi Seminari)
- Erick Mutasingwa (Sengerema Seminari)
- Rosalia Mwidege (St. Fransis Girls)
- Domina Wamara (St. Francis Girls)
- Mvano Cabangoh (Feza Boys Girls)
- Agatha Mlelwa (St. Fransis Girls)
- Sarah Kaduma (St. Fransis Girls
- Shammah Kiunsi (St. Fransis Girls
- Lucy Magashi ( Huruma Girls)

### Shule 10 zilizoshuka ufahulu

- Mbwego
- Mbezi Beach
- Maahad Istiqama
- Mwaniko
- Nyamtelela
- Gombe High School
- Alliance Rock Arm
- Ndomba
- Glorius Academy
- Kirinjiko Islamik Seminari

## UTATA MTUPU SAKATA LA MEYA JIJI DAR

UKURASA 4

## BoT sasa yawafunga 'pingu' wakopeshaji binafsi, Vicoba

UKURASA 4


Scan Hapa



Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu

Google Play | App Store



**MICHEZO** SIMBA, AZAM NGOMA NZITO UK. 32

MAONI, KATUNI UK.6

## HABARI KITAIFA

# Wasichana waongoza matokeo ya kidato IV

Na Mwandishi Wetu

BARAZA la Mitihani (Necta) limetangaza matokeo ya mtihani wa kidato cha nne mwaka jana, yakionyesha wasichana kufanya vizuri zaidi katika nafasi za ubora kitaifa.

Katika matokeo hayo yaliyotangazwa na Katibu Mtendaji wa baraza hilo, Dk. Charles Msonde, kati ya watahiniwa 10 bora kitaifa, nane ni wasichana na saba wanatoka Shule ya Sekondari St. Francis Girls ya Mbeya.

Msichana Joan Ritte kutoka Shule ya Sekondari St. Francis Girls ameibuka mtahiniwa bora kitaifa kwa mwaka 2019.

Dk. Msonde aliwataja watahiniwa wengine walioingia 10 bora kitaifa ni nyuma ya Joan kuwa ni Denis Kinyange wa Shule ya Sekondari Nyegezi Seminary jijini Mwanza, Erick Mutasingwa (Sengerema Seminary, Mwanza), Rosalia Mwidege na Domina Wamara (wote kutoka St. Francis Girls, Mbeya).

Wengine ni Mvano Cabangoh (Feza Boys, Dar es Salaam), Agatha Mlelwa, Sarah Kaduma, Shammah Kiunsi (wote kutoka St. Francis Girls, Mbeya) na Lucy Magashi (Huruma Girls, Dodoma).

Dk. Msonde alisema katika mtihani huo, watahiniwa wa shule 340,914 (asilimia 80.65) kati ya watahiniwa 422,722 kwenye matokeo hayo, wamefaulu.

"Wasichana waliofaulu ni 175,296 (asilimia 79.46) na wavulana ni 165,618 (asilimia 81.94)," alisema.

Alikumbusha kuwa mwaka 2018 watahiniwa walikuwa ni 284,126 (asilimia 79.27) ya watahiniwa wa shule waliofaulu mtihani huo, hivyo ufaulu umeongezeka kwa asilimia 1.38 ikilinganishwa na mwaka juzi.

Aliwataja wasichana 10 waliofanya vizuri zaidi katika mtihani huo kuwa ni Joan, Rosalia Mwidege, Domina Wamara, Agatha Mlelwa, Sarah Kaduma, Shammah Kiunsi (wote St. Francis Girls), Lucy Magashi (Huruma Girls, Dodoma), Imani Sanga, Joyce Magwaza na Marther Ngowi (wote St. Francis Girls).

Dk. Msonde aliwataka wavulana waliofanya vizuri zaidi kitaifa katika mtihani huo kuwa ni Denis Kinyange (Nyegezi Seminary), Erick Mutasingwa (Sengerema Seminary), Mvano Cabangoh (Feza Boys), Yohana Mwashambwa (Malangali, Iringa), Bruno Bassilley (Don Bosco Seminary, Iringa), Nelson Mbigili (St. Dominic Savio, Iringa), Ebenezer Mujungu (Faraja Seminary,

INAENDELEA UK. 8

# Wavulana vinara kidato cha pili

Na Mwandishi Wetu

KATIKA matokeo ya kidato cha pili yaliyotangazwa na Baraza la Mitihani Tanzania (Necta) wavulana wameongoza nafasi ya kwanza hadi ya tano kitaifa, huku mwanafunzi bora kitaifa katika matokeo ya upimaji huo akiwa ni Stephen Mwanzalima kutoka Shule ya Sekondari ya Wavulana ya Marian ya mkoani Pwani.

Katibu Mtendaji wa Necta, Dk. Charles Msonde, aliitangaza matokeo hayo jana jijini Dar es Salaam sambamba na ya upimaji wa darasa la nne na mtihni wa kidato cha nne.

Akitangaza matokeo ya kidato cha pili, alisema ya wanafunzi 514,251 sawa na asilimia 90.04 kati ya 571,137 wenye matokeo ya upimaji wamepata ujuzi na maarifa ya kuwawezesha kuendelea na kidato cha tatu.

Kwa mujibu wa Dk. Msonde, kati yao wasichana ni 270,750 sawa na asilimia 89.30 na wavulana ni 243,501 sawa na asilimia 90.88.

Dk. Msonde aliwataja wanafunzi wengine walioingia 10 bora kitaifa na shule na mikoa yao kwenye mabano ni Raimond Tewele (Marian Boysa, Pwani), Jovin Magulu (Marian Boys, Pwani), Julius Mwaka (Marian Boys, Pwani), Luis Osena (Marian Boys, Pwani), Violeth Emmanuel (Precious Blood, Arusha), Raymond Miho (Marian Boys, Pwani), Anna Kajiba (Canossa, Dar es Salaam) na Ibrahim Mawala (Marian Boys, Pwani).

**WASICHANA 10 BORA KITAIFA**

Violeth Emmanuel (Precious Blood, Arusha), Anna Kajiba (Canossa, Dar es Salaam), Leila Nakapi (St. Monica Moshono Girls, Arusha), Doreen Pallangyo (Marian Girls, Pwani), Marystella Lyimo (Precious Blood, Arusha), Cecilia Dickson (Canossa, Dar es Salaam), Esther Lugola (Canossa, Dar es Salaam), Irene Mbai (Precious Blood, Arusha), Daima Salum (Marian Girls, Pwani) na Hope Kitaluka (St. Joseph Millenium, Dar es Salaam).

**WAVULANA 10 BORA KITAIFA**

Stephen Mwanzalima (Marian Boys, Pwani), Raymond Tewele Marian Boys, Pwani), Jovin Magulu (Marian Boys, Pwani), Julius Mwaka (Marian Boys, Pwani), Luis Osena (Marian Boys, Pwani), Raymond Miho (Marian Boys, Pwani), Emmanuel Mtyama (Marian Boys, Pwani), Ibrahim Mawala (Marian Boys, Pwani), Norshad Kipenzi (Tengeru Boys, Arusha) na Gabriel Temba (Libermann Boys (Dar es Salaam).

Dk. Msonde alitaja shule 10 bora kitaifa na idadi ya wanafunzi wake kwenye mabano ni St. Francis, Mbeya (92), Kemebos Kagera (68), Centennial Christian Seminary, Pwani (152), Thomas More Machrina, Dar es Salaam (49) na Bethel Sabs Girls, Iringa (83).

Zingine ni St. Augustine-Tagaste, Dar es Salaam (163), Bright Future Girls, Dar es Salaam (119), Anwarite Girls, Kilimanjaro (82), Feza Girls, Dar es Salaam (64) na Canossa, Dar es Salaam (89).

Dk. Msonde alitaja shule 10 zilizoongoza ufaulu kwa miaka mitatu mfululizo ni Sogesca (Simiyu), Nyangao (Lindi), Jamhuri (Dar es Salaam), Dr. Asha Rose Migiro (Kilimanjaro), Consolata (Iringa), Kilwa Islamic (Lindi), Tabora Girls (Tabora), Arusha Day (Arusha), Magazini (Ruvuma) na Ahmes (Pwani).

Kwa upande wa shule 10 zilizoshuka ufaulu kwa miaka mitatu mfululizo ni Mbwego (Tanga), Kibirashi (Tanga), Feo Girls (Ruvuma), Nkama (Tanga), Mrike (Kilimanjaro), Kilindi (Tanga), Kasela (Tabora), Katoke-Lweru (Kagera), Jaila (Tanga) na Mama Maria Nyerere (Mara).

Dk. Msonde alitaja mikoa mitatu iliyofanya vizuri zaidi ni Arusha, Iringa na Kilimanjaro na mkoa wa Lindi ulioongoza ufaulu kwa kipindi hicho huku mikoa miwili ambayo ni Tabora na Mara iliyoshuka ufaulu.

Alisema halmashauri 10 zilizofanya vizuri zaidi na idadi ya shule zake kwenye mabano ni Bagamoyo (21), Bukoba (30), Meru (60), Njombe (26), Morogoro 59 na Monduli (20).

Nyingine ni Kibaha (38), Moshi Mjini (23), Moshi Vijijini (94) na Arusha (51).

"Halmashauri 10 zilizoongeza ufaulu kwa miaka mitatu ni Meatu, Madaba, Newala, Arusha, Lindi, Siha, Ukerewe, Kibaha, Kiteto na Liwale," alisema.

Pia halmashauri 10 zilizoshuka ufaulu kwa miaka mitatu mfululizo ni Kilindi, Mkuranga, Nzega, Kasulu, Buhigwe, Bukombe, Kigoma, Ulanga, Musoma na Serengeti.

Dk. Msonde alisema takwimu za matokeo zinaonyesha kuwa wanafunzi wamefanya vizuri zaidi katika masomo mengi ya msingi ambapo ufaulu wa masomo hayo uko juu ya wastani kati ya asilimia 50.28 na 92.19.

Aidha, alisema takwimu za matokeo zinaonyesha kuwa wanafunzi hawakufanya vizuri katika masomo matatu ambayo ni Hesabu, Kemia na Historia.


LAND O'LAKES VENTURE37 — AgResults INNOVATION IN RESEARCH AND DELIVERY

**Wito wa maombi ya kushiriki katika shindano la mradi wa AgResults (AgResults Tanzania Dairy Productivity Challenge Project)**

Kwa niaba ya **Mradi wa AgResults , Land O' Lakes Venture37** inapenda kukaribisha mashirika na taasisi zinazojihusisha na uuzaji na usambazaji wa pembejeo kwa wafugaji wa ng'ombe wa maziwa, kushiriki katika shindano la tuzo ambapo mradi umedhamiria kutumia mfumo wa kutoa motisha kutokana na kuuza pembejeo na kutoa huduma za ugani ili kuongeza wigo wa kutumia teknolojia bunifu, vifaa na mitizamo kwa ajilli ya kuongeza uzalishaji wa maziwa kwa kutumia pembejeo zilizo bora. Shindano hili litafanyika katika eneo la **Pwani ya Tanzania**, hasa Mikoa ya **Dar Es Salaam, Pwani, Tanga na Morogoro** (bila kushirikisha Wilaya za **Kilombero na Ulanga**)

**Land O' Lakes Venture37** inatoa wito kwa wote wanaotamani kushiriki kutoka kwenye sekta binafsi, taasisi au mashirika ya umma, na taasisi zisizo za kiserikali kushiriki katika mradi.

Wito wa Maombi ya Ushiriki (Request for Proposal – RFA) unaeleza historia, malengo, sheria ya kushiriki shindano hili ikijumuisha fomu ya maombi na taratibu za namna kuomba na mawasilisho. Katika kuwasilisha maombi, kampuni / shirika / Taasisi itakubaliana na masharti ya wito wa maombi ya ushiriki, ikiwa ni pamoja na taratibu za maombi na maelekezo yaliyowekwa.

Tafadhali kumbuka muda uliopangwa kwa ajili ya kupokea/kuwasilisha maombi ni **saa 11:00 Jioni ya Tarehe 28 Februari 2020.** Nyaraka za maombi lazima ziwasilishwe au zitumwe kwa anwani maalumu ya barua pepe ambayo ni **AgResultsTanzania@gmail.com**, kwa kuwasilisha Ofisi za AgResults zilizopo Veterinary Complex;131 Nelson Mandela Road, Dar es Salaam. Tafadhali andika "**Competitor RFA-AgResults Tanzania Dairy Productivity Project**" katika mstari wa somo la barua pepe au kwenye bahasha itakayobeba maombi hayo.

Mradi utapitia maombi yote na kutathimini kulingana na vigezo vilivyowekwa. Wale wote watakaofanikiwa kuchaguliwa watajulishwa na kuelezwa namna ya ushiriki.

**Ndugu mdau,** unahimizwa kuwasilisha maombi kwa wakati ili ujipatie tuzo/motisha na kuchangia maendeleo katika sekta ya maziwa Tanzania. Kama una maswali au maoni tafadhali tuma kwenye barua pepe ifuatayo; NMrema@landolakes.org.Tunatanguliza shukrani zetu kwa kwa kutuma maombi ya wito huu kwa wakati na pia tunategemea ushiriki wako katika mradi huu muhimu.

**Pata nakala ya wito wa maombi kupitia:**

https://agresults.org/news-and-blog/10-blog/152-rfa-tanzania-dairy-competitors

215578602

# Utata mtupu sakata Meya

**Na Waandishi Wetu**

VURUGU ziliibuka katika kikao cha Baraza la Madiwani wa Jiji la Dar es Salaam baada ya mmoja wa madiwani kudai kutiwa saini ya jina la mjumbe ambaye hakuwapo ndani ya chumba cha kikao jijini jana.

Kutokana na mvutano wa wajumbe, askari polisi walilazimika kuingia ndani ya ukumbi ili kutuliza vurugu kati ya wajumbe wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) na Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema).

Kikao hicho kilikuwa mahsusi kwa ajili ya kupokea taarifa ya uchunguzi dhidi ya tuhuma zinazomkabili Meya wa Jiji hilo, Isaya Mwita, baada ya tume iliyoundwa na Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Paul Makonda, kukamilisha uchunguzi wake. Akizungumza na Nipashe, Meya wa Ubungo (Chadema), Boniface Jacob, alidai vurugu zilianza baada ya madiwani wa CCM kuongeza jina la mjumbe ambaye hakuwapo kwenye kikao hicho.

Jacob alisema idadi ya madiwani wa CCM ndani ya kikao hicho ilikuwa 16, hivyo akidi ilikuwa haijatimia theluthi mbili ya idadi ya madiwani 26 ili kupiga kura ya kumwondoa meya madarakani.

"Idadi yao walikuwa 16 walikuwa, hawajatimia, hivyo waliongeza jina la mtu mmoja kwenye orodha ili wafike 17, waliongeza jina la mtu wa CUF, anaitwa Kasim Mshamu, ambaye ni Diwani wa Minazi Mirefu, hakuwapo kwenye kikao, lakini amesaini, hapo ndipo vurugu zilipoanzia," alidai.

Wakati vurugu hizo zinaanza, Jacob alisikika akisema: "Naomba kutoa taarifa katika hili daftari kuna mjumbe hayupo anaitwa Mshamu ameisaniwa namba 18, lakini mbona hayupo? Mkurugenzi na wewe unasimamia sheria, lakini hii siyo sawa mmeghushi. Dunia nzima leo inaona mlichokifanya, hatuwezi kukubali uhuni mlioufanya."

Vurugu hizo zilizidhibitiwa na askari polisi waliingia ndani ya ukumbi na kuwatoa Meya Jacob, Diwani wa Tabata (Chadema), Patrick Asanga, kwa sababu hawakutia saini daftari la mahudhurio ikiwa ni amri iliyolewa na Mkurugenzi wa Jiji, Sipora Liana, baada ya kuibuka mvutano wa kutokutia saini kwenye daftari hilo.

Miongoni mwa tuhuma anazokabiliana nazo Mwita ni kutotumia Sh. bilioni 5.8 za Shirika la Usafiri Dar es Salaam (Uda).

Fedha hizo ni asilimia 51 ya hisa zilizotolewa na Kampuni ya Simon Group kama sehemu ya ununuzi wa asilimia 51 ya hisa za Uda.

Tuhuma nyingine ni kutumia vibaya gari ya ofisi ambalo alipata nalo ajali, kushindwa kuongoza kikao cha baraza la madiwani na kusababisha Meya wa Ubungo, Jacob kugombana na Meya wa Temeke, Abdallah Chaurembo, na kudaiwa kuwapendelea baadhi ya mameya kuingia kwenye kamati ya fedha.

**KORTINI**

Viunga vya Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu jana saa nane mchana vilikuwa vinaonekana kuwa na askari kanzu na wenye sare za Jeshi la Polisi wenye silaha kabla ya kuahirishwa kutoa uamuzi mdogo wa kisitisha mchakato wa kumvua umeya, Meya wa Jiji la Dar es Salaam, Isaya Mwita. Mwita aliwasilisha kiapo chini ya hati ya dharura kuwazuia mlalamikaji wa kwanza, Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam na wa pili, Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Paul Makonda, kuendelea na mchakato wa kumwondoa kwenye kiti cha umeya mpaka kesi ya msingi itakaposikilizwa.

Hakimu Mkazi Mwandamizi, Janeth Mtega, aliyesikiliza maombi madogo ya mlalamikaji, alisema jana kuwa: "Uamuzi bado sijamaliza kuandika, mpaka kesho (leo) saa tano asubuhi, kesi hii naipanga Januari 10, 2020."

**Imeandikwa na Gwamaka Alipipi na Hellen Mwango**



Mwanafunzi wa Shule ya Feza, aliyeshika nafasi ya sita kitaifa, Mvano Cabangoh, akiwa amebebwa na wanafunzi wenzake, baada ya kutangazwa matokeo ya kidato cha nne, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# BoT yawabana wakopeshaji binafsi, Vicoba

**Na Salome Kitomari**

BENKI Kuu ya Tanzania (BoT), imevitaka vikundi, kampuni au mtu binafsi wanaopokea amana au kutoa mikopo, kujisajili kabla ya Oktoba 31, mwaka huu.

Aidha, imesema mtu yeyote atakayekutwa anatoa huduma hizo bila leseni atachukuliwa hatua za kisheria, huku ikibainisha kuwa usajili ulianza Novemba Mosi, mwaka jana.

"BoT inatoa onyo kwa mtu, kikundi au taasisi yoyote inayojihusisha na biashara ya upokeaji amana /au utoaji wa mikopo bila kuwa na leseni kucha mara moja," ilisema taarifa hiyo jana.

Aidha, taarifa hiyo ilieleza kuwa kifungu cha 6 (1) cha Sheria ya Benki na Taasisi za Fedha ya Mwaka 2006, kinakataza mtu yeyote kufanya biashara ya kibenki au kupokea amana kutoka kwa umma bila kuwa na leseni kutoka BoT.

Ilifafanua kuwa kifungu cha 16 (1) cha Sheria ya Huduma Ndogo za Fedha ya 2018, kinakataza mtu binafsi, kampuni au kikundi kilichoanza biashara kuanzia Novemba Mosi, mwaka jana kujihusisha na biashara ya kutoa mikopo bila kuwa na leseni halali inayotolewa na benki hiyo.

"Wananchi wanaombwa kutoa taarifa BoT, Jeshi la Polisi na vyombo vingine vya ulinzi na usalama pale wanapopata taarifa za uwepo wa watu binafsi, kampuni au vikundi vinavyotoa huduma za fedha bila kuwa na leseni," ilisisitiza.

**MMILIKI VICOBA MBARONI**

Katika hatua nyingine, BoT imebainisha uwapo wa kampuni za kitapeli zinazodai kutoa mikopo kwa wananchi ndani ya muda mfupi baada ya kujiunga kwa kuweka amana kwa njia ya mtandao. Tarifa hiyo ilibainisha kuwa kampuni mojawapo ni Vicoba Foundation ambayo inajinasibu kwa kutoa mikopo ya kuanzia Sh. milioni mbili hadi 10 baada ya mteja kulipia ada ya kujiunga ya kati ya Sh. 200,000 hadi 500,000.

"Ili kuvutia wananchi kampuni hii imekuwa ikiudanganya umma kwamba ni taasisi ya serikali, jambo ambalo halina ukweli wowote. Uchunguzi wa awali unaonyesha kwamba kampuni hii haina ofisi ya kudumu," ilibainisha na kuongeza:

"Kampuni hiyo inadaiwa kutumia majina ya viongozi wakuu wa nchi na watu mashuhuri katika kufanikisha utapeli wao."

Majina waliyodaiwa kuyatumia ni Rais John Magufuli, Makamu wa Rais, Samia Suluhu Hasan na Waziri Mkuu Kassim Majaliwa.

"BOT inapenda kuufahamisha umma kwamba mmiliki wa Vicoba Foundation kwa sasa anashikiliwa na vyombo vya dola ambavyo vinaendelea na uchunguzi ili kuchukua hatua stahiki," ilifafanua.

# DC asimulia askari alivyojitoa muhanga kufunga valvu mafuta

**Na Elizabeth Zaya**

MKUU wa Wilaya ya Kigamboni, Sarah Msafiri, amesimulia askari wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji alivyojitosa katikati ya moto kwenye matangi ya kuhifadhia mafuta ya kampuni ya Lake Oil na kufanikiwa kufunga valvu iliyokuwa inavuja mafuta na kuudhibiti.

Akizungumza jana katika eneo la tukio, Kigamboni, jijini Dar es Salaam, Msafiri alisema baada ya kufika eneo hilo na kushuhudia moto ukiwa unasambaa kwa kasi, askari huyo aliamua kuingia katikati ya moto na kwenda kufunga valvu katika moja ya matangi hayo baada ya kuona inatoa mafuta. "Askari wetu alishuka chini kwa kujitolea huku kukiwa na moshi mwingi na moto, akajitosa kuingia katikati ya moto ili kuokoa maisha ya maelfu ya wakazi wa Kigamboni. Kwa hiyo hali imetulia kwa sababu ya askari huyu mzalendo," alisema Msafiri.

"Lakini si kuokoa wananchi wa Kigamboni na Watanzania tu, bali hata kuokoa uchumi wa nchi zaidi ya sita ambazo zinapata mafuta kupitia Tanzania. "Mafuta, gesi, 'depot' yao kubwa ni hapa Kigamboni Vijibweni. Tuna 'supply' (sambaza) mafuta ndani ya nchi na zingine sita zinazotuzunguka. Kwa hiyo unaweza kuona uzalendo ambao askari wetu anao."

"Ameonyesha kwamba pale inapotokea janga ipo haja ya kuokoa taifa, inabidi ujitoe muhanga. Tumefanikiwa kudhibiti moto, askari wetu 'amefaint' lakini anaendelea vizuri. Nimshukuru Kamanda wa Zimamoto na Uokoaji wamejipanga vizuri na kuna timu imebaki kwa ajili ya kusoma mazingira," alisema Msafiri.

Alisema walibaini kwamba moja ya valvu ilikuwa inavuja katika matangi hayo ya mafuta na kwamba bado wanafanya uchunguzi zaidi wa tukio hilo.

"Kilichokuwa kinachochea moto kukua ilikuwa valvu kuvuja, lakini chanzo chenyewe cha moto kutokea bado hakijafahamika. Bado uchunguzi unaendelea na utakapokamilika tutafahamishana kitaalamu," alisema.

Kamanda wa Zimamoto Mkoa wa Temeke, Elia Kakwembe, alisema licha ya kuzima moto huo, bado timu maalum iliachwa jana katika eneo hilo kwa ajili ya kufanya uchunguzi ili kufahamu chanzo cha moto huo.

"Tunaendelea kufanya uchunguzi na tutafanya wa kina kubaini nini chanzo cha moto. Hiyo itatusaidia kupunguza majanga mengine ya namna hii, tunachoshukuru hakuna majeraha makubwa," alisema Kakwembe.

# Waziri aishukia halmashauri kupima viwanja 105 miaka 40

**Na Munir Shemweta,** LINDI

NAIBU Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Angeline Mabula, ameishukia Idara ya Ardhi katika Halmashauri ya Wilaya ya Mtama mkoani Lindi, kwa kuwa na viwanja 105 ndani ya miaka 40.

Dk. Mabula alikutana na kadhia hiyo juzi akiwa katika ziara yake ya kuhamasisha ukusanyaji maduhuli ya serikali kupitia kodi ya ardhi pamoja na kuangalia utendaji kazi wa sekta ya ardhi katika Halmashauri za Mkoa wa Lindi.

Alisema pamoja na halmashauri hiyo kuwa ya siku nyingi, imeshindwa kupima maeneo na kuwamilikisha wananchi jambo lililosababisha hadi leo kuwa na hati 105 pekee.

Licha ya hatua hiyo kuikosesha serikali mapato yatokanayo na kodi ya pango la ardhi, Dk. Mabula alisema hatua hiyo pia inasababisha wananchi kutokuwa na miliki za viwanja, hivyo kuwakosesha fursa ya kujiendeleza kiuchumi kupitia hati za ardhi ambazo zingetumika kuchukulia mikopo benki.

"Halmashauri ina viwanja 105 wakati ni ya siku nyingi. Hii inaonyesha watumishi wa sekta ya ardhi hawafanyi kazi yao ipasavyo. Hapa kuna uzembe, Mkurugenzi fuatilia suala hili kwani vifaa vya upimaji vipo katika kanda, tatizo ni nini?" Alihoji.

Aidha, Naibu Waziri alishangazwa na Halmashauri ya Mtama ambayo katika kipindi cha mwaka mmoja imeandaa hati mbili tu za ardhi jambo alilolieleza kuwa linampa shaka na utendaji wa watumishi wa sekta hiyo katika halmashauri hiyo.

Kutokana na hali hiyo, ameiagiza Ofisi ya Ardhi Kanda ya Kusini kuiangalia halmashauri hiyo na kuisaidia katika masuala ya ardhi ikiwamo kupima maeneo ili kuwa na idadi kubwa ya viwanja vilivyopimwa.

INAENDELEA UK. 8



Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Ali Mohamed Shein, akipata maelezo kutoka kwa msimamizi wa mradi wa ujenzi wa daraja la Kibondemzungu, Mhandisi Cosmas Masolwa, kuhusu ujenzi wa daraja hilo, baada ya kulifungua katika Barabara ya Fuoni mjini Zanzibar jana, kama sehemu ya shamrashamra za Miaka 56 ya Mapinduzi ya Zanzibar. **PICHA: IKULU ZANZIBAR**

# Mbaroni akidaiwa daktari feki

**Na Futuna Seleman,** RUFIJI

MKAZI wa Panyakoo mkoani Mara, Ismail Onyango (42), anashikiliwa na Jeshi la Polisi Mkoa wa Kipolisi Rufiji kwa tuhuma za kujifanya daktari na kutoa tiba kwa wananchi bila kuwa na taaluma hiyo.

Onyango anadaiwa kuelekeza tiba zake wanawake ambao aliokuwa akiwatoa mimba nyumbani kwa mtu katika Kata ya Ngarambe, Rufiji mkoani Pwani.

Mwenyekiti wa Kamati ya Ulinzi na Usalama Wilaya ya Rufiji, Juma Njwayo, akizungumzia tukio hilo, alisema jana kuwa alipewa taarifa na raia wema juu ya kuwapo kwa daktari feki.

"Tulipata taarifa kutoka kwa raia wema, yupo mtu anadai ni daktari, amefikia Kijiji cha Ngarambe, Kata ya Ngarambe na kutoa huduma za tiba, lakini cha kushangaza zaidi anatibu wanawake tu. Baada ya taarifa hizo, tuliagiza ofisi ya Kata Ngarambe ifuatilie na kutoa taarifa," alidai.

Mkuu huyo wa Wilaya ya Rufiji alidai walibaini uwapo wa jambo hilo na kupiga simu kwa Mganga Mkuu wa Wilaya ambaye alitoa wataalamu wake, wakiwamo wa maabara, Hamis Bungala na Said Muba na Ofisa Afya wa Wilaya, Ali Rashid, ambao walishirikiana na Mganga wa Zahanati ya Kijiji cha Ngarambe kufuatilia na kufanikiwa kumpata akiwa nyumba ya mtu ambaye bado anatafutwa.

Alidai kuwa Onyango alikutwa na vifaa mbalimbali vya hospitali, ikiwamo mikasi, mabomba ya sindano, kipimo cha ugonjwa wa kisukari, hadubini na pamba na kwamba alipohojiwa, hakuwa na cheti chochote cha taaluma ya daktari, uuguzi wala utabibu.

"Alihojiwa aonyeshe vyeti vyake vya taaluma hakuwa navyo na uchunguzi umebaini alikuwa akitoa pia huduma za utoaji mimba na wateja wake wengi aliwalenga wanawake," alidai.

Njwayo alidai Jeshi la Polisi linaendelea kuchunguza watu aliokuwa akishirikiana nao kufanya biashara hiyo baada ya kubaini kuna watu nyuma yake.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Rufiji, Onesmo Lyanga, akizungumza na Nipashe, alithibitisha kukamatwa kwa mtu huyo, ingawa alidai suala hilo bado halijamfikia ofisini.

"Nipo nje ya ofisi, pengine linazunguka zunguka, likinifikia, nitalizungumzia. Kwa sasa sijalipata," alidai.

# JPM kuanza ziara Zanzibar leo

**Na Mwandishi Maalum**

RAIS John Magufuli jana aliwasili jijini Dar es Salaam akitokea nyumbani kwake Chato mkoani Geita na leo anatarajiwa kuanza ziara ya kikazi visiwani Zanzibar.

Taarifa iliyotolewa jana kwa vyombo vya habari na Kurugenzi ya Mawasiliano ya Rais Ikulu, ilieleza kuwa Rais Magufuli leo ataanza ziara ya kikazi visiwani huko, akitarajiwa kuweka jiwe la msingi la jengo la Idara ya Usalama wa Taifa Zanzibar.

Ilielezwa katika taarifa hiyo ya Ikulu kuwa, kesho Rais Magufuli ataweka jiwe la msingi la Shule ya Sekondari ya Mwanakwerekwe iliyoko Mjini Magharibi na atafungua hoteli yenye hadhi ya nyota tano iitwayo Hotel Verde Azam Luxury Resort and Spa iliyoko Mtoni.

"Mheshimiwa Rais Magufuli atashiriki sherehe za maadhimisho ya Miaka 56 ya Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar zitakazofanyika Jumapili Januari 12 mwaka huu katika Uwanja wa Amaan, Mjini Magharibi," ilielezwa katika taarifa hiyo ya Ikulu.


DRC DANISH REFUGEE COUNCIL

TANGAZO LA ZABUNI

SHIRIKA LA KUHUDUMIA WAKIMBIZI LA DANISHI LINATARAJIA KUINGIA KWENYE MKATABA KWA MUDA WA MWAKA MMOJA NA MTOA HUDUMA YA KISHERIA.

NYARAKA ZA KUJAZIA MAPENDEKEZO YA BEI ZINAPATIKANA KATIKA OFISI ZA DANISHI KIBONDO KUANZIA TAREHE 09.01.2020 HADI TAREHE 22.01.2020 SIKU ZA KAZI SAA 2:00 ASUBUHI MPAKA SAA 10:30 JIONI. TUNAPATIKANA BARABARA YA IRC KIBONDO. KWA MAWASILIANO ZAIDI PIGA 0627423991 au barua pepe jean.kabore@drc.ngo

MWISHO WA KURUDISHA ZABUNI NI TAREHE 22.01.2020, 10:30 JIONI.

ZABUNI ZITAFUNGULIWA HADHARANI TAREHE 24.01.2020 SAA 4:00 ASUBUHI OFISI ZA DANISHI KIBONDO NA KAMATI YA KUFUNGUA ZABUNI LA DANISHI.

UNAWEZA KURUDISHA ZABUNI KUPITIA rfq.tza@drc.ngo AU KULETA MOJAKWA MOJA OFISINI VINGINEVYO NI BATILI.



TAARIFA KWA UMMA.



JOSEPHAT M. MWANIWALAZYA.

MTAJWA HAPO JUU SIO MFANYAKAZI WA TUNAKOPESHA LIMITED TANGU 03.06.2017 NA HAUSIKI NA SHUGHULI ZOZOTE ZINAZOHUSU TUNAKOPESHA LIMITED HIVYO BASI, TUNAKOPESHA LIMITED HAITAHUSIKA NA MIAMALA AU SHUGHULI ZOZOTE ZITAZOFANYWA NA MTAJWA HAPO JUU.

IMETOLEWA NA UONGOZI WA TUNAKOPESHA LIMITED

11578402

# MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

## Utoaji vyeti vya kuzaliwa kwa watoto uchangamkiwe

**WAZIRI** wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Selemani Jafo, ameingilia kati sakata la wazazi na walezi wanaoandikisha watoto kwa ajili ya kuanza darasa la kwanza, kwa kulazimishwa kuwa na vyeti vya kuzaliwa.

Wakuu wa shule katika maeneo yote nchini tangu Jumatatu shule zilipofunguliwa, wamekuwa wakiwataka wazazi na walezi wanaokwenda kuandikisha watoto wa darasa la kwanza kutimiza takwa la kisheria la kuwa na vyeti hivyo, ambavyo hutolewa na Wakala wa Usajili, Ufilisi na Udhamini (Rita).

Hata hivyo, wazazi wengi na walezi hususan maeneo ya vijijini wameshindwa kutimiza sharti hilo, kutokana na kutokuwa na vyeti hivyo, na kulalamika baada ya kukataliwa kuwaandikisha watoto.

Kutokana na hali hiyo, Waziri Jafo juzi aliingilia kati kwa kutangaza kuwa ni marufuku mwanafunzi kuzuiliwa kuandikishwa darasa la kwanza, kwa sababu ya kukosa cheti cha kuzaliwa.

Jafo alitangaza mafuruku hiyo wakati wa ziara yake wilayani Bahi Mkoa wa Dodoma kukagua uandikishaji wa wanafunzi wa darasa la kwanza kwa shule za msingi pamoja na mapokezi ya wanafunzi wa kidato cha kwanza katika shule za sekondari.

Alieleza kuwa amepokea malalamiko kutoka baadhi ya maeneo nchini kwamba wanafunzi wa darasa la kwanza hawaandikishi kama hawana vyeti vya kuzaliwa.

Waziri huyo alifafanua kuwa cheti cha kuzaliwa ni haki ya kila mtoto, lakini isimzuie mtoto huyo kuanza shule eti kwa sababu tu hajapata cheti hicho, na kuagiza kuwa watoto wote wapokelewe, waandikishwe na waanze masomo wakati wazazi wao wakiendelea na mchakato wa kuwatafutia vyeti hivyo.

Alisema hataki kusikia eneo lolote mtoto ameachwa kupokelewa na kuanza shule kwa sababu ya kukosa cheti cha kuzaliwa, hivyo mzazi ahakikishe ndani ya miezi minne amepata cheti hicho, lakini mtoto huyo aanze masomo wakati masuala ya cheti yanaendea kushughulikiwa kwenye mamlaka husika.

Uamuzi wa Jafo ni wa kupongeza, kutokana na hataruki iliyoibuka katika maeneo mengi nchini kutokana na vyeti vya kuzaliwa kukwaza mchakato wa kuwaandikisha wanafunzi wa darasa la kwanza.

Huo ndio uwajibikaji kwa viongozi wa umma; kwamba pale linapotokea tatizo kubwa la msingi kama hilo linaloathiri wananchi, anachukua hatua haraka za kulitatua.

Ni ukweli kuwa vyeti vya kuzaliwa kwa wananchi kadhaa hususan wa vijijini bado ni changamoto, hivyo ipo haja kwa mamlaka husika hususan Rita kuangalia utaratibu mzuri zaidi wa kuvitoa hususan katika maeneo ya vijijini, ambako kinamama wanajifungulia majumbani.


Katika mazingira kama haya, inakuwa vigumu watoto kuwa na vyeti vya kuzaliwa, hivyo tunaishauri jamii kujenga utamaduni wa kufuatilia vyeti vya kuzaliwa kwa watoto baada ya kuzaliwa kwa kuwa kwa sasa ni nyaraka muhimu.

Ikumbukwe kuwa cheti cha kuzaliwa ni miongoni mwa nyaraka zinazotakiwa wakati wa kuanza elimu ya msingi, sekondari, kujiunga na vyuo, kupata pasi za kusafiria na huduma nyinginezo.

Kwa siku za karibuni, Rita imekuwa na utaratibu mzuri na endelevu wa kutoa vyeti vya kuzaliwa katika maeneo mbalimbali kama maonyesho ya Sabasaba, Nanenane na shughuli nyingine, hivyo wananchi tuichangamkie ili kila mmoja awe na cheti cha kuzaliwa hususan watoto.

Kwa kufanya hivi, changamoto zinazojitokeza kila mara ikiwamo ya uandikishaji wanafunzi zitakuwa historia.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Meneja Matangazo:** Kauthar D'souza, 0767 223311
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge

# Kutambua wadudu sugu kwa dawa ni elimu tosha



Na Sabato Kasika

**MAANA** ya usugu kwa antibaiotiki inaelezwa na wataalamu wa afya, ni hali ya vimelea vya magonjwa kutokufa kwa dawa iliyothibitika na inayotumika kuua vimelea hivyo.

Dawa za antibaiotiki zinatajwa kuwa katika kundi la dawa linalojulikana kitaalamu 'antimicrobials' ambazo hutumika kuua au kuzuia ukuaji vimelea vinavyosababisha magonjwa ya kuambukiza binadamu na wanyama.

Aidha, inakadiriwa watu 700,000 hufariki duniani kila mwaka, kutokana na usugu wa wadudu na kwamba asilimia 89 ya vifo vyote hutokea barani Afrika na Asia.

Hiyo ni kwa mujibu wa ofisa kutoka Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi) Dk. Boniface Marwa, alipofungua mafunzo ya namna ya kujikinga dhidi ya maambukizi kwa kufuata miongozo wakati wa kumuhudumia mgonjwa mkoani Kigoma.

Ni mwezi Oktoba mwaka jana, alikaririwa na vyombo vya habari, akisisitiza kuwa jitihada za makusudi ni lazima zichukuliwe kila mtaalamu katika sekta ya afya, apambane na tatizo hilo.

Dk. Marwa anasema, tatizo hilo linazidi kuwa tishio duniani na haja ya kufanyika utafiti kupata dawa mpya zitakazoweza kupambana na wadudu sugu.

Wakati serikali ikielekeza hayo, ipo haja kwa jamii nayo kuchukua hatua, ikiwamo kuzingatia elimu, ambayo imekuwa ikitolea kila mara kuhusu madhara ya usugu wa wadudu dhidi ya dawa.

Ikumbukwe, usugu wa dawa umekuwa moja ya tishio kubwa kwa afya ya wananchi katika jamii, hivyo ni muhimu kuzingatia maelekezo au elimu kwa ajili ya kukabiliana na tatizo hilo.

Wadudu sugu dhidi ya dawa ni tatizo linaloendelea kusumbua jamii, hivyo jamii izingatie elimu inayotolewa kuhusu madhara yanayoweza kutokea na pia watumishi wa sekta ya afya, wafuate miongozo na taratibu za utoaji huduma za afya wakati wa kutoa huduma kwa mgonjwa.

Kwa kuzingatia hilo, Watanzania wenye mtindo wa kutumia dawa zisizo na ulazima yanaweza kupungua kama siyo kumalizika kabisa ili yasiendelee kusababisha tatizo la usugu wa wadudu dhidi ya dawa.

Hivyo, elimu kwa umma ni muhimu izingatiwe na kutambua usugu wa dawa ni hali, ambayo dawa husika inashindwa kuua wadudu mbalimbali kama bakteria.

Shirika la Afya Duniani (WHO), linaweka wazi kwamba usugu wa dawa ni janga la kidunia kwa vile karibia kila nchi imeripoti kushindwa kwa baadhi ya dawa kufanya kazi.

Linafafanua kuwa kushindwa kutibu magonjwa mbalimbali ya kuambukiza mwisho wa siku kupelekea ugonjwa kukaa muda mrefu, mgonjwa kushindwa kufanya shughuli mbalimbali na hatimaye kusababisha kifo.

Umma unatakiwa kupata elimu ya kutosha ya kujua visababishi vya usugu wa dawa ambavyo vimekuwa vikitajwa na wataalamu wa afya na kuvizingatia, kwani hiyo ni njia mojawapo kuwa salama.

Kiuhalisia dawa inapotumika muda mrefu, vijidudu huishia kuwa sugu kwa dawa hiyo, ingawa kuna baadhi ya tabia za kibinadamu, ambazo huchangia kwa uharaka zaidi kwa usugu huo kutokea.

Kupitia elimu tena ya kutosha, jamii itajua kuwa kuishi katika mazingira yasiyo masafi kama vile kunywa maji yasiyochemshwa, kula vyakula visivyoandaliwa katika mazingira yanayotakiwa huchangia kusambaza vijidudu sugu kutoka kwa mtu mmoja kwenda kwa mtu mwingine.

Mbali na hilo, jamii pia itajua kwamba kutokumaliza dozi ya dawa za kuua vijidudu, na kuishia njiani pale mtu anapoona amepata nafuu, husababisha kuzalishwa kwa vijidudu sugu.

Suala la kufuata maelekezo ya wataalamu wa dawa (wafamasi), katika matumizi ya dawa ikiwamo kuhakikisha mgonjwa anamaliza dozi na kutokusahau kunywa dawa kwa muda elekezi ni jambo la msingi.

Kwa kuzingatia elimu, kutamfanya mtu aepuke kwenda katika duka la dawa na kununua dawa bila kupata ushauri wa daktari au kufanyiwa uchuguzi ili kufahamu ni mdudu yupi aliyesababisha ugonjwa husika.

## HABARI KITAIFA

# Korti yasikiliza kesi ya uchochezi kwa video

**Na Hellen Mwango**

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Kisutu, jijini Dar es Salaam jana, ilisikiliza kesi ya uchochezi wa ugaidi wa njia ya mtandao wa Facebook inayomkabili Jackson Mkuki kupitia 'video conference' wakati mshtakiwa akiwa Gereza la Keko.

Shughuli za Mahakama hiyo ziliendelea kwa mujibu wa taratibu za kawaida tofauti, ambapo mshtakiwa alimsikiliza Hakimu Agustina Mmbando akiwa mahabusu katika gereza hilo kwa njia ya video.

Mshtakiwa alimweleza hakimu kwamba kesi yake ina miaka mitano, lakini upande wa Jamhuri bado unasuasua kukamilisha upelelezi.

Awali, Wakili wa Serikali, Ester Martin, alidai upelelezi umekamilika, lakini wanasubiri wapelelezi wakamilishe maelezo ya Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP).

"Mheshimiwa DPP, ameandika barua kwa wapelelezi kutoa maelekezo ya upelelezi wa kesi hiyo, tunaomba tarehe nyingine ya kutajwa tutakayokuja na majibu kamili kuhusu kesi hii," alidai Martin.

Hata hivyo, mshtakiwa aliomba nafasi ya kuiomba mahakama, na ilipomruhusu alidai Desemba 19, 2019 DPP alipowatembelea alimlalamikia kuhusu jalada lake kuchelewa kufanyiwa kazi na ofisi yake.

"Nilimlalamikia DPP kuhusu jalada la kesi yangu kukaa kwake tangu Agosti, 2019 bila kulifanyia kazi, alishangaa kwamba hajaliona... naomba mheshimiwa upande wa Jamhuri wanitendee haki niko mahabusu miaka mitano sasa," alidai Mkuki.

Akijibu malalamiko ya mshtakiwa kwa njia ya video, Martin alidai kuwa awape muda upande wa Jamhuri utafuatilia, na kwamba tarehe ijayo watakuwa na majibu kuhusu malalamiko yake.

Hakimu Mmbando aliuagiza upande wa Jamhuri kufuatilia jalada la kesi hiyo tarehe ijayo mahakama ijue wamefikia wapi.

Alisema kesi hiyo itatajwa Januari 23, mwaka huu na mshtakiwa aendelee kukaa mahabusu.

Wakati huohuo, mahakama hiyo imepiga kalenda kesi ya uhujumu uchumi ikiwamo kulisababishia Shirika la Umeme Tanzania (Tanesco) hasara ya Sh. 930,433,396.50.

Kesi hiyo inawakabili walinzi wawili wa Security Guard, Rafael Kisaucha na Athuman Shekiufya ilitajwa jana mbele ya Hakimu Mmbando wakati washtakiwa wakiwa mahabusu ya Keko kwa njia ya video.

Hakimu alisema kesi hiyo itatajwa Januari 23, mwaka huu.

## Watumbuliwa kubambikia wateja bili za maji

**Na Innocent Ng'oko,** MBEYA

MAMLAKA ya Majisafi na Usafi wa Mazingira jijini Mbeya (Mbeya UWSSA), imewafukuza kazi watumishi watatu kutokana na kubainika kujihusisha na vitendo vya kuwabambikizia bili za maji wananchi.

Mkurugenzi Mtendaji wa Mbeya UWSSA, Mhandisi Ndele Mengo, alibainisha hayo jana wakati akizungumza na Nipashe, na kusema kuwa ofisi yake inaendelea na msako wa kimya wa wafanyakazi wanaoshindwa kutekeleza wajibu wao.

Alisema watumishi hao watatu walifukuzwa kazi mwishoni mwa Desemba mwaka jana kutokana na kubainika kuwabambikizia bili za maji wateja kwa kuandaa taarifa za kupika tofauti na taarifa zinazoandaliwa na mmalaka hiyo kulingana na matumizi ya maji waliyotumia wateja.

Alisema mamlaka hiyo haitakuwa tayari kuona wateja wao wananyanyasika kwa kubambikiziwa bili zao za maji kutoka kwa baadhi ya watumishi wasiowaaminifu ndani ya mamlaka hiyo.

"Ninarudia kutoa onyo kwa watumishi wa mamlaka kuwa yeyote atakayebainika kujihusisha na vitendo vya kuihujumu mamlaka itawachukuliwa hatua za kinidhamu ikiwamo kufukuzwa kazi mara moja kwa kuwa hatuko tayari kuona wananchi wanapata tabu," alisema Mhandisi Mengo.

Alisema mefika wakati wananchi lazima watoe ushirikiano kwa uongozi wa mamlaka kutokana na changamoto za huduma wanazokumbana nazo ikiwamo kubambikiziwa bili za maji au baadhi ya watumishi au 'vishoka' wanaohihusisha na kuhujumu miundombinu ya mamlaka kwa makusudi.

Mhandisi Mengo alisema mpaka sasa mamlaka hiyo imejipanga kuhakikisha inatoa huduma bora kwa wananchi hususani wateja wa maji katika maeneo mbalimbali ya Jiji la Mbeya na kuwa ambao hawajaunganishiwa maji wawasilishe maombi ya kupata huduma ya maji.


Tuna Habari njema

Barclays Bank Tanzania Limited itabadilisha jina lake rasmi na kuitwa Absa Bank Tanzania Limited tarehe 10 Februari 2020. Tumekuwa tukikuhudumia kwa miaka 19 na tunatazamia kukuhudumia zaidi kwa miaka inayokuja.Tusherehekee nyakati zijazo pamoja.

#journeytoAbsa

Kujua zaidi, tembelea barclays.co.tz/journeytoabsa

BARCLAYS

absa Part of the Absa family

Barclays is changing to Absa.
Even though things may look different, your banking details won't change and we'll never ask you for these details.

Barclays Bank Tanzania yenye usajili namba 38557 inaendeshwa na kanuni za Benki Kuu ya Tanzania. Barclays Bank Tanzania Limited inatumia chapa ya Barclays chini ya leseni ya Barclays Bank Plc.

# Majaliwa afuta mnada wa TRA wa Januari 7



Na Mwandishi Wetu

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, (pichani) amefuta mnada wa nafaka ulioendeshwa na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) Januari 7, 2020 na kuagiza uongozi wa mamlaka hiyo kutangaza upya zabuni baada ya kutoridhishwa na taratibu zilizofanyika awali.

Mnada huo ambao unahusisha mahindi tani 5,000 na ngano tani 460.12 unafanyika baada ya wahusika kushindwa kutimiza masharti ya kiforodha, hivyo serikali imeamua kuuza ili kufidia gharama zake. Nafaka hizo ziliingia nchini Machi 2017. Waziri Mkuu alisitisha mnada huo jana wakati akizungumza na Kamishna wa Forodha na Ushuru wa Bidhaa wa TRA, Ben Asubisye, ofisi ndogo ya Waziri Mkuu jijini Dar es Salaam.

Waziri Mkuu aliagiza kutangazwa upya kwa mnada mwingine wa kuuza mahindi hayo sambamba na ngano to wahakikishe masuala yote kuhusu mnada huo yanakamilika ndani ya siku tatu kuanzia jana.

"Mahindi yameuzwa kwa bei ya Sh. 340 kwa kilo moja ambayo ni chini na bei ya soko kwa sababu bei ya mahindi sokoni kwa sasa ni Sh. 800. Zabuni imetangazwa kwa muda mfupi watu wameshindwa kushiriki. Ilifunguliwa saa 8 mchana na imefungwa saa 5 usiku."

Kadhalika, Waziri Mkuu aliutaka uongozi wa TRA uhakikishe mnada unaofuata unakuwa wa wazi, huru pamoja na kutoa muda wa kutosha kwa wananchi wote kushiriki ili kuondoa malalamiko.

"Kwa kuwa mnada unafanyika kwa njia ya mtandao, hakikisheni matumizi ya mtandao yanakuwa rafiki kwa wananchi wote watakaovutiwa kuwasilisha zabuni zao."

Hata hivyo, Majaliwa alisisitiza kuwa TRA ishirikiane na mamlaka nyingine za serikali kuhakikisha wanunuzi wa nafaka hizo hawaziingizi sokoni kwa ajili ya matumizi ya binadamu. Nafaka hizo zimepimwa na kuthibitika kuwa zinafaa kwa matumizi ya wanyama.

# Mwanafunzi aliyeongoza afunguka mazito

INATOKA UK. 2

maisha ya kawaida.

"Baba yangu ni mhasibu katika Halmashauri ya Wilaya ya Arusha na mama ni mwalimu katika Shule ya Sekondari ya Ufundi Moshi."

**MWALIMU ATOA NENO**

Mwalimu wa shule hiyo, Leonard Peter, alisema siri kubwa iliyochangia wanafunzi wa shule hiyo kufanya vizuri ni mazingira mazuri ya kazi waliyojengewa wafanyakazi wake.

Nyingine ni kazi kubwa inayofanywa na walimu katika shule hiyo katika kuwafundisha wanafunzi kwa bidii, kuwajengea misingi mizuri ya hofu ya Mungu na nidhamu.

**MAMA MZAZI ANENA**

Kwa upande wake mama mzazi wa Joan, Marina Mkonyi alisema matokeo ya mtoto wao yamewapa faraja kubwa.

"Si kwamba hatukutegemea kwamba angefaulu, tulijua atafaulu vizuri kwa sababu ripoti zake zote za shuleni hakuna alipowahi kufeli, isipokuwa hatukujua kwamba angeongoza kabisa," alisema mama mzazi wa mwanafunzi huyo.

Alisema kama wazazi siku zote walikuwa wanahakikisha anakuwa na nidhamu katika kila kitu awapo shuleni.

"Mimi ni mwalimu, kwa hiyo siku zote nilikuwa namsihi kwamba zote ni mbwembwe tu, lakini vitu muhimu vinavyosaidia mwanamke aheshimike ni kuwa na elimu nzuri, kwa hiyo alikuwa analijua hilo na alikuwa anakazana kweli," alisema.

"Mwanangu huwa anashukuru sana anapopatiwa zawadi hata kama ni ndogo, kwa hiyo nilikuwa nachochea na vitu vya namna hiyo, kipindi cha mitihani yake nilikuwa nampa ahadi ya zawadi mara moja moja, kwa hiyo ilikuwa lazima nitimize kwa sababu alikuwa anafaulu," aliongeza.

Mkonyi alisema mbali na kwamba kulikuwa na umuhimu wa kuzingatia masomo, lakini alihakikisha anamfundisha kufanya shughuli zote za nyumbani anapokuwa likizo.

"Unajua na malezi pia kwa watoto wetu huwa yanasaidia. tusipende kuwasikiliza kila kitu wanachotuambia au wanachotaka, tunawaharibu. Mimi mwanangu sikumlea kama mayai, shughuli zote za nyumbani anafanya na haya matokeo tumeyapata nikiwa nimempa kazi ngumu za kufanya hapa nyumbani.

# Waziri aishukia halmashauri kupima viwanja 105 miaka 40

INATOKA UK. 5

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Mtama, Methew Makwinya na Mbunge wa Mchinga, Hamidu Bobali, walimweleza Naibu Waziri Mabula kuwa eneo kubwa katika halmashauri hiyo halijapimwa na kubainisha kuwa njia pekee ya kuwasaidia wananchi wa Mtama ni kuwapatia timu ya wataalamu watakaosaidia kupanga, kupima na kumilikisha maeneo na hatimaye kutoa hati zikiwamo za kimila.

Walimwomba Naibu Waziri kuangalia namna fukwe zilizomo kwenye halmashauri hiyo zitakavyowanufaisha wamiliki wake kwa kuwapatia hati zitakazowasaidia kiuchumi.

Akiwa mkoani Lindi, Dk. Mabula aitembelea pia Halmashauri ya Wilaya ya Ruangwa na Manispaa ya Lindi. Katika Halmashauri ya Ruangwa, alikagua masijala ya ardhi na kubaini majalada ya hati takriban 300 yakiwa hajakamilishwa kwa ajili ya kutoa hati kwa wamiliki wake kwa muda mrefu.

Kutokana na hali hiyo, aliipa miezi mitatu Idara ya Ardhi katika Halmashauri ya Ruangwa kuhakikisha inawatafuta na kuwamilikishi waombaji wote na kupatiwa taarifa kuhusiana na suala hilo.

Kwa upande wa Manispaa ya Lindi, alisikitishwa na halmashauri hiyo kushindwa kuwafuatilia wadaiwa sugu wa kodi ya pango la ardhi na wadaiwa hao kupelekewa ilani za madai.

Kwa mujibu wa Ofisa Ardhi wa Manispaa ya Lindi, Andrew Munisi, ofisi yake ilipeleka hati za madai 245 zenye thamani ya Sh. bilioni tatu na baadhi ya wadaiwa wamelipa zaidi ya Sh. bilioni mbili, huku Sh. bilioni moja zikiwa bado hazijalipwa.


**bgtl BEST GROUP (T) LIMITED**

Debts collectors, Auctioneer, Commission Agent & Legal Consultant

**TANGAZO LA MNADA WA HADHARA**

Kwa idhini tuliyopewa na **AKIBA COMMERCIAL BANK PLC** tutauza kwa **MNADA WA HADHARA,** dhamana za wadaiwa. Mnada utafanyika kuanzia saa **4:00 asubuhi** na kuendelea mahali dhamana zilipo kama inavyoonyesha hapo chini.

| No | JINA LA MDAIWA | DHAMANA | TAREHE YA MNADA | BRANCH |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Freeman Njou Kimaro | Mabanda ya kufugia kuku yaliyopo kwenye kiwanja chenye hati ya umiliki namba135784, kiwanja namba2 kitalu" G" Chenye jina la Freeman Njou kimaro.Maeneo ya Kongowe mkoa wa Pwani. | 25/01/2020 | MWANZA |
| 2 | Awadhi Omary Nasoro | Nyumba ya makazi ambayo haijakamilika iliyopo kwenye kiwanja chenye hati ya mauziano. Maeneo ya Pugu mnadani. | 24/01/2020 | UKONGA |
| 3 | Abdulrahman Rajab Mahaba | Nyumba ya makazi iliyopo kwenye kiwanja chenye hati yamauziano maeneo ya Zingiziwa-Ngobeti | 29/01/2020 | UKONGA |
| 4 | Leornard Bakuza Kabilo | Nyumba ya makazi iliyopo kwenye kiwanja chenye hati ya mauziano,maeneo ya Viwege. | 24/01/2020 | UKONGA |
| 5 | Abdallah Rashid Mbegu/A.J HARDWARE LIMITED | Nyumba ya makazi iliyopo kwenye kiwanja chenye hati ya mauziano maeneo ya kinyerezi yenye jina la Abdallah Rashid Mbegu | 29/01/2020 | UKONGA |

**MASHARTI YA MNADA**

1. Dhamana itauzwa kama ilivyo.
2. Mnunuzi atatakiwa kulipa siku ya mnada asilimia 25% ya bei iliyofikiwa.
3. Malipo ya asilimia 75% yalipwe ndani ya siku kumi na nne (14). Kukamilisha malipo yote. Kushindwa kufanya hiyo mnunuzi atakuwa amepoteza malipo yote ya awali ya asilimia 25%, na mnada kurudiwa.
4. Gharama za kuona, kukagua, kuhamisha umiliki, kumtoa mdaiwa/mpangaji na zingine zinazoambatana na hilo ni jukumu la mnunuzi.

**Kwa Taarifa zaidi wasiliana na: AU**

**Mkurugezi Mtendaji**
**Best Group (T) LTD**
**Alli Hassan Mwinyi Road.**
**Green Acres Buliding, 2nd Floor.**
**P.O. BOX 1088**
**DAR ES SALAAM**
**MOBILE + 255 715-363537/ +255 765-363537**

**Mkurugezi Mtendaji**
**Akiba Commercial Bank PLC,**
**P.O. BOX 699,**
**DAR ES SALAAM.**
**Tel: +255 022 211 8340-3**

215580702


# Wasichana waongoza matokeo ya kidato IV

INATOKA UK. 3

Kilimanjaro), Timothy Mjuni (Centennial Christian Seminary, Pwani), Richardson Kwareh (Centennial Christian Seminary, Pwani) na Henry Kimbori (Centennial Christian Seminary, Pwani).

Dk. Msonde alizitaja shule 10 bora kitaifa na idadi ya watahiniwa kwenye mabado kuwa ni Kemebos (70) Kagera, St. Francis Girls (91) Mbeya, Feza Boys (74) Dar es Salaam, Canossa (103) Dar es Salaam, Anwarite Girls (54) Kilimanjaro, Precious Blood (91) Arusha, Marian Boys (108) Pwani, St. Augustine Tagaste (110) Dar es Salaam, Maua Seminary (52) Kilimanjaro na Musage Boys (118) Mwanza.

Shule 10 zilizoongoza ufaulu kwa miaka mitatu mfululizo ni Ibun Jazar Islamic (Pwani), St. Achilleus Kiwanuka Kijwire (Kagera), Mlalo (Tanga), Paramiho Girls (Ruvuma), Huruma Girls (Dodoma), St. Augustine Tagaste (Dar es Salaam), Nyaishozi ( Kagera), Waja Boys (Geita), Boniconsili Mabamba Girls (Kigoma) na St. Getrude Mlandizi Girls ( Pwani). Dk. Msonde alitaja shule 10 zilizoshuka ufaulu kwa miaka mitatu mfululizo ni Mbwego (Tanga), Mbezi Beach (Dar es Salaam), Maahad Istiqama (Kusini Unguja), Mwaniko (Mwanza), Nyamtelela (Mwanza), Gombe High School (Kigoma), Alliance Rock Army (Mwanza), Ndomba (Kagera), Glorious Academy (Mjini Magharibi) na Kirinjiko Islamic Seminary (Kilimanjaro).

Katika matokeo hayo, baraza hilo limetaja mikoa mitatu iliyofanya vizuri zaidi kuwa ni Kilimanjaro, Arusha na Iringa na iliyoongeza ufaulu kwa kipindi hicho ni Iringa, Njombe na Ruvuma huku kukiwa hakuna iliyoshusha ufaulu mfululizo.

Dk. Msonde alizitaja halmashauri 10 zilizofanya vizuri zaidi na idadi ya shule kwenye mabano ni Bagamoyo (19), Bukoba (30), Meru (56), Mafinga (16), Kibaha (36), Njombe (26), Kibondo (23), Kahama (29), Moshi (93) na Bariadi (16).

Halmashauri 10 zilizoongoza ufaulu kwa miaka mitatu ni Madaba (Ruvuma), Mbinga (Ruvuma), Mafinga (Iringa), Bukoba (Kagera), Mpimbwe (Katavi), Pangani (Tanga), Kasulu (Kigoma), Iringa (Iringa), Njombe (Njombe) na Kilolo (Iringa).

Dk. Msonde alitaja halmashauri 10 zilizoshuka ufaulu kwa miaka mitatu mfululizo ni Mafia (Pwani), Kibiti (Pwani), Geita (Geita), Kakonko (Kigoma), Kondoa (Dodoma), Mpanda (Katavi), Kishapu (Shinyanga), Kiteto (Manyara), Bumbuli (Tanga) na Malinyi (Morogoro).

HABARI KITAIFA

# Uzalishaji mdogo samaki maji asili bado changamoto

**Na Idda Mushi,** MOROGORO

KATIBU Mkuu Wizara ya Mifugo na Uvuvi anayeshughulikia uvuvi, Dk. Rashid Tamatama, amesema licha ya mafanikio katika sekta ya uvuvi bado kuna changamoto ya uzalishaji mdogo wa samaki kutoka kwenye maji ya asili ikilinganishwa na kiasi cha maliasili ya maji yaliyopo nchini.

Dk. Tamatama alisema hayo mjini Morogoro wakati akizungumza na wadau waliokuwa wakiupitia mpango wa biashara wa Shirika la Uvuvi Tanzania, TAFICO, ambapo alibainisha zaidi ya wananchi milioni 4.5 wameendelea kutegemea shughuli za uvuvi kuendesha maisha yao.

Alisema licha ya Tanzania kuwa na rasilimali nyingi za maji na sekta ya uvuvi kutoa mchango mkubwa katika usalama wa chakula na lishe hususan kwa jamii zinazoishi maendeleo ya vijijini kwa kuchangia takribani asilimia 30 ya protini itokanayo na wanyama, bado kuna uzalishaji mdogo wa samaki kutoka kwenye maji ya asili.

"Hata hivyo uzalishaji wa samaki umeendelea kuongezeka ambapo umefikia tani 448,469 katika mwaka wa fedha wa 2018/2019 zenye thamani ya Sh. trilioni 2.11, na kati yake, jumla ya tani 51,718.3 ya samaki, na samaki wa mapambo 81,373, wote wakiwa na thamani ya Sh. bilioni 691.88 waliuzwa nje ya nchi katika kipindi husika," alisema Dk. Tamatama.

Akaongeza kuwa nguvu ya uvuvi imekuwa ikiongezeka kwa kasi kubwa hali inayoweza kutishia uendelevu wa rasilimali hizo na mchango wake kwa taifa.

Hata hivyo alisema lengo la serikali ni kuifufua Tafico ili kukidhi mahitaji ya nchi ya sasa ya kufikia uchumi wa kati wa viwanda na utekelezaji wa sera ya uvuvi ya mwaka 2015 pamoja na mpango wa taifa wa miaka mitano 2016/17 hadi 20/21. Alibainisha kuwa kwa sasa sekta ya uvuvi imekuwa ikitoa ajira ya moja kwa moja kwa takribani wavuvi 202,053 na zaidi ya wananchi milioni 4.5 wanategemea sekta hiyo kuendesha maisha yao.

Mkurugenzi wa Uvuvi wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Emanuel Bulayi, alibainisha serikali imejipanga kulifufua upya Tafico lililoanzishwa tangu mwaka 1974 likilenga kuendeleza sekta ya uvuvi, ingawa baadaye mwaka 96 liliwekwa kwenye orodha ya mashirika ya umma yaliyotakiwa kubinafsishwa, hivyo kusitisha shughuli zake, ingawa baada ya kukosa mwekezaji anayeweza kuliendeleza lilirudishwa upya serikalini.

Kaimu Meneja Mkuu wa TAFICO, Easter Mulyila, alisema wizara hiyo imekusudia kununua meli kubwa tano za uvuvi kwa awamu ya kwanza kwa kuanza ndani ya mbili ili kuvua kwenye ukanda wa uchumi wa bahari kuu, ikiwa ni sehemu ya mikakati yake kuhakikisha inaendesha sekta ya uvuvi kibiashara.




Wakazi wa eneo la Sinza kwa Remmy, jijini Dar es Salaam, wakichangamkia madafu, baada ya katapila linalochonga barabara ya Shekilango, kuangusha mti wa mnazi, jana. **PICHA: SABATO KASIKA**

## Bil. 27/- kuboresha uwanja wa ndege

**Na Tiganya Vincent,** TABORA

JUMLA ya Sh. bilioni 27 zinatarajiwa kutumika katika uboreshaji wa Uwanja wa Ndege wa Tabora.

Kauli hiyo imetolewa jana na Meneja wa Wakala wa Barabara nchini (Tanroads) Mkoa wa Tabora, Damian Ndabalinze, wakati wa kikao cha Bodi ya Barabara Mkoa wa Tabora.

Alisema kuwa fedha hizo zitatumika katika ujenzi wa jengo la abiria, uzio na maegesho katika Uwanja wa Ndege wa Tabora ambao unataka kuanza ndani ya mwaka huu wa fedha baada ya fedha hizo kutolewa.

Ndabalinze alisema kukamilika kwa ujenzi huo kutaliwezesha kuwa na jengo la abiria katika uwanja huo ambalo litakuwa na uwezo wa kuchukua 500,000 kwa mwaka.

Alisema ujenzi huo unatarajiwa kufanywa na mkandarasi Beijing Construction. & Engineering Group, Consultant; Khatib and Alami wa Lebanon.

Katika hatua nyingine, Meneja huyo wa Tanroads Mkoa wa Tabora alisema kuwa jumla ya magari 41,735 yalipimwa kwa mwaka jana.

Alisema katika zoezi hilo magari yaliyozidisha uzito yalikuwa ni 753 ambapo yalilipa faini ya Sh. milioni 73.7.

Aidha, alisema Tanroads imetenga mzani wa kudumu katika eneo la Ilolanguru kwa gharama ya Sh. milioni 125.

# Sangoma wanaoogesha watoto dawa za mapenzi kikaangoni

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

WAGANGA wa kienyeji mkoani Shinyanga ambao wamekuwa wakiwaogesha watoto wa kike dawa za kimapenzi ili wapendwe na wanaume maarufu kwa jina la 'Samba', wataanza kusakwa ili kupewa maagizo mazito ya serikali.

Serikali imewaonya waganga hao kuwa watakaokaidi watachukuliwa hatua kali.

Hayo yalibainishwa juzi na Katibu wa Mpango mkakati wa kitaifa wa serikali wa kupunguza ukatili dhidi ya wanawake na watoto mkoani Shinyanga (Mtakuwwa), Tedson Ngwale, wakati akizungumza na Nipashe juu ya mkakati uliopo wa serikali kupunguza tatizo la mimba na ndoa za utotoni mkoani humo.

Alisema moja ya tatizo ambalo limekuwa likisababisha mimba na ndoa za utotoni kuendelea mkoani Shinyanga, ni waganga wa kienyeji kuwaogesha dawa za kimapenzi watoto wa kike ili wapendwe na wanaume, na hatimaye kuolewa ndoa za utotoni ili wazazi wao wapate mahari ya mifugo.

"Mkakati ambao ni miongoni mwa mipango yetu ya kupunguza tatizo la mimba na ndoa za utotoni mkoani Shinyanga, ni kuwasaka waganga wote wa kienyeji, ambao wamekuwa wakiwaogesha watoto wa kike dawa za kimapenzi," alisema.

Aliwaonya waganga watakaoendelea kuogesha watoto wa kike dawa hizo, na kwamba watakaoendelea watachukuliwa hatua kali.

"Mkoa umeshaagiza wakuu wa wilaya wote pamoja na wakurugenzi, kufanya msako wa waganga wa kienyeji, ambao wanaogesha dawa za mapenzi watoto wa kike pamoja na kuileta orodha yao yote hapa mkoani ili wapate kutambulika. Mkuu wa mkoa atafanya mazungumzo nao na kuwapatia maagizo mazito," alisema.

Aidha, mkakati mwingine ambao mkoa umepanga ni kuendelea kutoa elimu ya afya ya uzazi na madhara ya kuozesha watoto wadogo, kwa kushirikiana na mashirika mbalimbali ambayo yanatekeleza miradi ya ulinzi wa mtoto. Pia kujenga nyumba salama ya kuhifadhi waathirika wa mimba ili kutoharibu kesi mahakamani.

Alisema pia wanafanya mawasiliano na kumpuni za simu za mkononi, ili kuwa zinatumwa jumbe fupi kwa wakazi wa mkoa wa Shinyanga zinazopinga matukio ya ukatili dhidi ya wanawake na watoto, ambapo ujumbe hizo moja ya kampuni ya simu zimeshaanza kutumwa.

Mmoja wa waathirika wa ndoa za utotoni (jina limehifadhiwa) mwenye umri wa miaka 14 mkazi wa Kata ya Lubaga wilayani Kishapu mkoani Shinyanga, ambaye aliozeshwa kwa mzee mwenye umri wa miaka 70 kwa ng'ombe sita, amelaani kitendo cha kuogesha dawa ambacho kimezima ndoto zake ambapo alitaka kuja kuwa muuguzi.

Takwimu za kitaifa za mwaka 2012, Mkoa wa Shinyanga unaongoza kwa tatizo la mimba na ndoa za utotoni kwa asilimia 59, ukifuatiwa na Tabora 58, na wa tatu ni Mara 55, ambapo watoto wamekuwa wakiolewa chini ya umri wa miaka 18.

# Kesi ya mtuhumiwa 'Tereza' yapigwa kalenda

**Na Joctan Ngelly,** KIGOMA

MAHAKAMA ya Wilaya ya Kigoma Mkoa wa Kigoma, imeahirisha kesi inayomkabili mkazi wa Gungu Manispaa ya Kigoma/Ujiji, Joseph Richard (25) ambaye ni mtuhumiwa wa kundi la uhalifu la 'Tereza', baada ya upande wa mashtaka kudai kuwa haujaanda maelezo ya awali dhidi ya mashtakiwa.

Mshtakiwa huyo alifikishwa mahakamani jana majira ya saa 3 asubuhi akitokea mahabusu katika Gereza la Bangwe na kupandishwa kizimbani mbele ya Hakimu Mkazi wa Mahakama hiyo, Eva Mushi.

Mshtakiwa huyo anakabiliwa na shtaka moja la kumshambulia Mwamini Hussein kwa kumkata na panga sehemu ya kichwani na kwenye mguu, na kumsababishia majeraha.

Upande wa mashtaka ukiongozwa na Wakili wa Serikali, Clement Masua, alidai kuwa hawajaandaa maelezo ya awali dhidi ya mshtakiwa huyo, na kuomba mahakama ipange tarehe nyingine ili aweze kumsomea mshtakiwa maelezo ya awali.

Hakimu Mushi alikubaliana na ombi hilo na kuahirisha kesi hiyo hadi Januari 23, mwaka huu kwa ajili ya kumsomea mshtakiwa huyo maelezo ya awali.

Aidha, Hakimu Mushi alisema mshtakiwa ataendelea kukaa mahabusu hadi hapo atakapopata mdhamini. Hakimu Mushi alimsisitiza Wakili wa Serikali kuharakisha maelezo ya awali dhidi ya mshtakiwa.

Awali, Hakimu Mushi aliyataja masharti ya dhamana kwa mshtakiwa huyo kuwa anatakiwa kuwa na mdhamini mmoja mwenye barua ya utambulisho kutoka kwa ofisa mtendaji wa kata na mali isiyohamishika yenye thamani ya Sh. milioni 2.

Awali upande wa mashtaka ukiongozwa na Wakili wa Serikali Raymond Kimbe, ulidai kuwa upelelezi wa kesi hiyo umekamilika, na kuomba tarehe nyingine ya kutajwa kwa ajili ya kumsomea mshtakiwa huyo maelezo ya awali.

Akisoma hati ya mashtaka, Kimbe alidai kuwa Agosti 8, mwaka 2019 majira ya usiku eneo la muongwe Mkoa wa Kigoma, mshtakiwa alimshambulia Mwamini Hussein kwa kumkata na panga sehemu za kichwani na kwenye mguu wa kushoto.




Meneja wa Kampeni ya Ibuka Kidedea na NBC Malengo, Mtenya Cheya ( kushoto), akizungumza na mmoja ya washindi aliyeshinda zawadi ya bodaboda katika droo ya tatu ya kampeni hiyo iliyofanyika jijini Dar es Salaam jana. Kushoto kwake ni Meneja wa Bidhaa za Kuwekeza wa NBC, Dorothea Mabonye, Meneja Chapa na Mawasiliano wa benki hiyo, David Raymond na Wakaguzi kutoka Bodi ya Michezo ya Kubahatisha, Elibariki Sengasenga na Abdallah Hemedi. **MPIGAPICHA WETU**

## Matumizi malengo akaunti yahimizwa

**Na Mwandishi Wetu**

BENKI ya Taifa ya Biashara (NBC) imewahamasisha Watanzania kutumia akaunti ya malengo ya benki hiyo kama suluhisho ya changamoto mbalimbali za kifedha hivyo kuwawezesha kutimiza ndoto zao.

Akizungumza jijini Dar es Salaam jana kwenye droo ya tatu ya kampeni ya Ibuka Kidedea na NBC Malengo, Meneja Chapa na Mawasiliano wa benki hiyo, David Raymond, alisema wateja wa benki hiyo waendelee kutumia benki hiyo ili kutatua changamoto zao za kila siku.

"Huu ni mwanzo wa mwaka na Watanzania wengi wanakabiliwa na majukumu kadhaa kama vile ada za shule, kodi za nyumba na bima za gari na nyumba, ni muhimu kwao kuendelea kuwa karibu na benki hii na kwa wale ambao bado hawajafungua akaunti ya malengo ni vyema wakufungua ili waweze kunufaika na zawadi," alisema Raymond.

Alisema droo hiyo ni ya tatu ambayo ilianza mwezi wa Oktoba mwaka jana na washindi kadhaa wa bodaboda na safari za kutalii mbuga za wanyama Serengeti na visiwani Shelisheli walikwenda na kurudi salama kwa usimamizi na ufadhili wa benki hiyo kupitia kampeni ya malengo akaunti.

Kwenye droo hiyo ya jana, washindi watano waliibuka kidedea kwa kujishindia pikipiki aina ya Yamaha, washindi hao ni; Luka Haule Baraka wa Dodoma, Juma Halfani kutoka Songea, Rebeka Ndosh anayeishi Mwanza, Rosemary Kibodya wa Dar es Salaam na Restituta Mbuya wa Morogoro.

Kampeni ya Ibuka Kidedea na NBC Malengo itashuhudia washindi watatu wakiibuka kidedea na kujishindia zawadi ya pikipiki ya miguu mitatu aina ya Toyo katika droo kubwa inayotarajiwa kufanyika mwezi Machi mwaka huu.

# Ujenzi jengo la NEC wamridhisha waziri

**Na Elizabeth Zaya**

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Uratibu, Bunge, Kazi, Ajira, Vijana na Watu wenye Ulemavu), Jenista Mhagama, ametembelea na kukagua hatua ya ujenzi wa jengo la Ofisi za Tume ya Taifa ya Uchaguzi zilizopo eneo la Njedenwa jijini Dodoma kuridhishwa na hatua iliyofikiwa.

Mhagama alitembelea na kukagua mradi huo ukiwa ni utekelezaji wa maagizo ya Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, aliyoyatoa Novemba 18, 2019, alipotembelea na kukagua mradi huo na kuonekana kutoridhishwa na kasi ya ujenzi wake.

"Kwa kipindi chote ambacho SUMA JKT imeendeela na kazi ya ujenzi wa jengo hili hali inaridhisha, na ni vyema kuhakikisha mnaendana na kasi inayotakiwa kwa kuzingatia gharama zilizokubalika za Sh. bilioni 16," alisema Mhagama. Alieleza kuwa ujenzi wa majengo ya serikali ni moja ya hatua za kuhakikisha kazi ya kuhamisha watumishi Dodoma linafanikiwa kwa kuendelea kuweka miundombinu rafiki ya ofisi zao.

"Mpaka sasa watumishi wapatao 14,868 wameshahamia hapa Dodoma, hivyo tutaendelea kuandaa mazingira ikiwamo ujenzi wa ofisi hizo kwa kuzingatia kazi ya uratibu huo ipo chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu," alisema Mhagama.

Alisema kukamilika kwa jengo hilo kutasaidia kuhakikisha watumishi wa ofisi hiyo wanatoa huduma vizuri kwa kuzingatia mwaka 2020 ni mwaka wa uchaguzi mkuu. Mhagama alisema kuwa miongoni mwa majukumu ya ofisi yake ni kuhakikisha inaratibu shughuli zote za kuhamisha watumishi wa serikali na kuweka mazingira mazuri ya ofisi zao ili kuendelea kuitumikia nchi kwa weledi na kujiletea maendeleo yao kwa kutoa huduma bora zinazostahili.

Kwa upande wake, mmoja wa wasimamizi wa ujenzi wa majengo hayo, Michael Mussa, alieleza kuwa wataendelea kufanya kazi kwa viwango vinavyotakiwa ili kuwa na majengo yenye ubora kwa kuzingatia gharama zilizofikiwa kwenye mkataba wa ujenzi huo.

"Tumefarijika kwa ujio wako waziri na tunaahidi tutajenga kwa kipindi kilichopangwa kwa kuzingatia gharama zilizopo kwenye mkataba wa ujenzi huu," alieleza Michael.




Msaidizi wa Katibu Mkuu wa Umoja wa Mashirika ya Posta Afrika, Kalawole Aduloju, akifafanua jambo kwa wanahabari jijini Arusha juzi, kuhusu ujenzi wa jengo la makao makuu ya umoja huo. **PICHA: WOINDE SHIZZA**

# Manyara yaijia juu Nida namba za vitambulisho

**Na Allan Isack,** SIMANJIRO

BAADHI ya wakazi wa mkoani Manyara, wamelalamika kuchelewa kupatiwa namba za vitambulisho vya Taifa na Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA).

Sintofahamu hiyo imesababisha baadhi ya wananchi kuchelewa kusajili laini za simu kwa mfumo wa kielektroniki.

Wakizungumza na Nipashe jana wakazi hao, wameiomba serikali kuangalia kwa jicho la tatu mchakato huo, kwa kuwa bado kuna kundi kubwa la watu hawajapata namba zao wakati walijaza fomu za usajili tangu miezi mitatu iliyopita.

Husna Shabani alisema bado wanashangaa hadi sasa hawajapata namba zao za Nida kwa ajili ya kukamilisha mchakato wa kusajili namba laini za simu.

"Wanawake wengine wana watoto kila wiki tunakuja ofisi za Nida kufuata namba zetu kama zimetoka, lakini hakuna kitu zaidi ya kuambiwa namba mpya hazijatoka," alisema.

Mkazi wa Kata ya Endiamtu, Isack Abraham, alisema suala hilo limechukua muda mrefu wakati walishakamilisha taratibu zote ikiwamo kupigwa picha na kuchukuliwa alama za vidole.

"Mkurugenzi wa Nida anapaswa kuja hapa Mirerani ili tumuhoji maswali kwa kuwa wananchi wengi bado wanasubiria namba zao kwa zaidi ya miezi mitatu na muda wa mwisho Januari 20 mwaka huu," alisema Abraham.

Selemani Juma, alisema wapo wananchi wenye namba za simu wanazotumia benki kufanya miamala ya fedha katika simu zao, hivyo watakuwa na wakati mgumu pindi laini zao zitakapofungiwa.

Hata hivyo, Mratibu wa Nida mkoani Manyara, Emmanuel Mrema, alisema shughuli ya usajili inaendelea kutolewa kwa wananchi kwenye wilaya zote tano za mkoa huo.

Alisema wananchi wanatakiwa kuwa na subira kwa ajili ya kupatiwa namba za usajili wakati wakisubiri mchakato wa kupewa vitambulisho vya Taifa.

"Hatuwezi kutoa takwimu sahihi za wananchi waliopatiwa namba kwa kuwa ukitaja idadi asubuhi ikifika jioni idadi inakuwa imeongezeka zaidi," alisema.

# Mwalimu matatani kwa tuhuma kuomba rushwa ngono mwanafunzi

**Na Allan Isack,** ARUSHA

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru) mkoani Arusha, imemkamata mwalimu wa Shule ya Sekondari Embarway iliyopo Kata ya Endulen wilayani Ngorongoro, kwa kosa la kushawishi na kuomba rushwa ya ngono kwa mwanafunzi wake.

Akizungumza na waandishi wa habari jana, Mkuu wa Takukuru Mkoa wa Arusha, Frida Wikesi, alisema kosa hilo ni kinyume cha kifungu cha 25, cha Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa namba 11 ya mwaka 2007.

Kwa mujibu wa Wikesi, mwalimu huyo ni William Sambwethi Moleli ambaye anafundisha somo la uchumi.

Alisema kwa nyakati tofauti mwalimu huyo, amekuwa akimnyanyasa mwanafunzi huyo, akiwa shuleni bila ya kuwa na sababu ya msingi.

Aidha, alisema siku moja mtuhumiwa alimwambia mwanafunzi huyo kuwa ili awe na amani shuleni, inabidi washiriki tendo la kimapenzi akiwa likizo.

Alisema mwanafunzi huyo (jina limehifadhiwa), baada ya kuelezwa hivyo na mwalimu wake, aliamua kwenda katika ofisi za Takukuru na kutoa taarifa hiyo.

Kamanda huyo alisema Takukuru ilimwekea mtego Januari 8, mwaka huu, na kumkamata mwalimu huyo akiwa na mwanafunzi huyo katika nyumba ya kulala wageni, kwa lengo la kutimiza nia yake.

Alisema taasisi yake inatoa onyo kwa walimu na watu wengine wanaotumia mamlaka yao vibaya kwa kunyanyasa wasichana na wanawake kwenye jamii.

# Mnyeti aagiza wananchi sasa walipwe fidia

**Na Allan Isack,** KITETO

WAKAZI wawili wa Kata za Bwawani na Matui, wilayani Kiteto, walionyang'anywa ardhi yao kwa ajili kujengwa shule za msingi, wameahidiwa maeneo yao, baada ya Mkuu wa Mkoa wa Manyara, Alexander Mnyeti kuingilia kati.

Wananchi hao, walifikisha kilio chao kwa Mnyeti kwenye mkutano wa hadhara kata za Matui na Bwawani, wilayani Kiteto kwenye ziara yake ya siku tano ya kukagua miradi ya maendeleo, kusikiliza kero na kero za wananchi na kutoa majawabu.

Mnyeti alisema kutokana na maeneo ya wananchi kuchukuliwa na taasisi za serikali, na kujengwa shule ingetakiwa wapewe maeneo mengine ili kufidiwa maeneo yao.

"Mkurugenzi, nakuagiza utoe maeneo mengine wapewe hawa wananchi waliochukuliwa maeneo yao kwa ajili ya kufidiwa hata kama ni suala la maendeleo, lakini wanapaswa kupata haki zao," alisema.

Alisema baadhi ya kero ambazo hazina sababu ya kuachwa zinapaswa kutatuliwa kwa kuwa wananchi wengine wataichukia serikali bila sababu ya msingi.

Mkazi wa kijiji cha Matui, Juma Masare, alilalamika kuporwa eneo lake hekari 12, na serikali ya kijiji wakajengwa shule ya msingi.

"Baada ya kupora eneo langu serikali ya kijiji ilijenga shule, lakini hawakunifidia sehemu nyingine japokuwa maeneo mengine yapo," alisema Masare.

Naye Mkazi wa Kijiji cha Wezamtima Kata ya Bwawani, Endeni Kilangi, alilalamika kwa Mkuu huyo wa Mkoa kuwa alinyang'anywa na serikali ya kijiji hicho hekari 70, kwa ajili ya ujenzi wa shule ya msingi.

"Shamba hilo, lilichukuliwa na serikali ya kijiji, lakini sikufidiwa eneo lingine ilihali kuna maeneo mengine wangeweza kunipa haki yangu," alisema Kiangi.

Alisema japokuwa wanapenda maendeleo ya kijamii, lakini wangefidiwa maeneo mengine kwa kuwa kijiji kina maeneo makubwa na ya kupitika.

# Waziri aagiza fedha mfuko wa jimbo Hai kufanya maendeleo

**Na Godfrey Mushi**, HAI

NAIBU Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), Mwita Waitara, ameagiza kiasi cha Sh. milioni 42 zinazotokana na fedha za Mfuko wa Jimbo la Hai mkoani Kilimanjaro ambazo hazikutumika katika mwaka 2018/2019 kupelekwa kwenye shughuli za maendeleo. Jimbo la Hai linaongozwa na Kiongozi wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni na Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), Freeman Mbowe.

Akizungumza na wakuu wa idara, watumishi na watendaji wa kata na vijiji wa wilaya hiyo, alisema fedha hizo zimekaa kwa muda mrefu hivyo zinapaswa kuelekezwa kwenye maendeleo.

Katika maelekezo yake, alisisitiza kuwa uamuzi wa Mkuu wa Wilaya ya Hai, Lengai Ole Sabaya, kuamuru kumegwa kwa Sh. milioni saba kati ya Sh. mil. 42 za fedha za mfuko wa jimbo hilo kwa ajili ya kutatua tatizo la vyoo vya walimu katika kijiji cha Mijongweni, Kata ya Mnadani lina baraka zote za Tamisemi. "Natoa maelekezo upya na mnisikilize, Mkurugenzi fedha za mfuko wa jimbo za mwaka 2018/19 ambazo hazijatumika zitumike. Vijiji viombee miradi na vipewe hizo fedha hata kama ni za vyoo," alisema Waitara.

Mwishoni mwa mwaka jana, Ole Sabaya, aliamuru Sh. milioni 42 ambazo ni za Mfuko wa Jimbo la Hai zimegwe Sh. milioni 7 na zipelekwe kujenga choo cha walimu wa Shule ya Msingi Mijongweni.

Ole Sabaya alitoa maelekezo kwa Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Hai, Yohana Sintoo, kutoa kiasi hicho cha fedha na kuzipeleka katika shule hiyo leo.



Mwongoza watalii kutoka Kampuni ya Kili Twende Adventures ya Moshi, Robert Woisso (katikati), akiwa na watalii katika kilele cha Mlima Kilimanjaro, eneo la Stella Point, jana. **PICHA: JAMES LANKA**

## Siha walia kukamilika kwa ujenzi zahanati

**Na Mary Mosha**, SIHA

WAKAZI wa jamii ya wafugaji katika Kijiji cha Sinai Kata ya Ormelili wilayani Siha, wameomba serikali kuongeza nguvu kukamilisha ujenzi wa zahanati ya kijiji.

Aidha, wamesema kukamilika kwa ujenzi huo kutapunguza adha kwa kinamama kujifungulia kwa wakunga wa jadi kutokana na umbali mrefu wanaotembea kutafuta huduma za afya hasa nyakati za usiku.

Wajawazito na watoto hulazimika kutembea umbali wa kilomita 10 hadi 15, ili kupata huduma za afya katika hospitali za wilaya ya Hai au Siha mkoani Kilimanjaro.

Wakizungumza mbele ya mkuu wa wilaya hiyo, Onesmo Buswelu, alipotembelea zahanati hiyo na kuona uchimbaji wa shimo la choo ukiendelea katika zahanati hiyo, walisema hali hiyo inawaweka kwenye wakati mgumu.

Mkazi wa eneo hilo Gloriani Shoo, alisema kuwa umbali huo unachangia ongezeko la kinamama kujifungulia nyumbani pamoja na kushindwa kwenda kliniki kama inavyoshauriwa kitaalamu.

"Tumejitahidi katika kuhakikisha zahanati hii inakamilika, lakini tunaomba serikali kuangalia mateso ya mama anayoyapata na athari zake ili kuongeza nguvu na kituo kukamilika kwa haraka zaidi," alisema Gloriani.

Jafari Mwalisu alisema hali hiyo ngumu ya kutafuta matibabu hupelekea kinamama wengi kujifungulia barabarani, huku wakisaidiwa na wakunga wa jadi.

"Ujenzi wa zahanati hiyo una zaidi ya miaka kumi haujakamilika, hivyo hutulazimu kutembea umbali mrefu kilometa 10 hadi 15 kwenda kufuata huduma katika Hospitali ya Wilaya ya Siha iliyopo Sanya Juu au kwenda Hospitali ya Wilaya ya Hai, hali inayotugharimu fedha nyingi na kuhatarisha maisha ya mama, mtoto na wazee hasa nyakati za usiku," alisema Mwalisu.

Dereva bodaboda Saimon Molel, anasema lipo tatizo la umbali limekuwa changamoto kwa wagonjwa licha ya wao kunufaika kwa kipato kikubwa.

"Ni kweli kuwa wakinamama wanapata changamoto kubwa wakati wa kujifungua hasa nyakati za usiku hulazimika kukodisha bajaji au bodabora kuanzia Sh. 30, 000 hadi Sh. 50,000 kumpeleka hospitali jambo ambalo ikiwa serikali malizia zahanati ya karibu nasi wataweza kupata huduma za kitabibu kwa haraka zaidi," alifafanua.

Mwenyekiti wa Kitongoji cha Kilusu, Jacob Mollel, alisema ujenzi wa zahanati hiyo ulianza mwaka 2012 na katika ujenzi huo imeshatumika kiasi cha Sh. milioni 59 kutoka serikali kuu, ili kukamilisha ujenzi huo inahitajika kiasi cha Sh. milioni 136.

Alisema zahanati hiyo imeshapauliwa lakini bado vitu mbalimbali ili kukamilika ikiwamo madirisha, milango na ujenzi wa choo, nyumba za watumishi na uzio.

Mkuu wa Wilaya hiyo, Buswelu alisema za zahanati hiyo ipo hatua za mwisho kukamilika na kuwa itaanza kutoa huduma Februari mosi, mwaka huu.

# Taa zaing'arisha Moshi, zaimarisha ulinzi

**Na Mary Mosha**, MOSHI

HALMASHAURI ya Manispaa ya Moshi, imeweka taa zinazotumia mwanga wa jua, kando kando ya barabara zake zote, zilizopo katikati ya mji, pamoja na kata zote zilizoko pembezoni ili kuimarisha ulinzi nyakati za usiku.

Hayo yamesemwa na Mstahiki Meya wa Manispaa hiyo, Raymond Mboya, wakati akitoa taarifa ya mwaka 2020, kwa waandishi wa habari ofisini kwake juzi kuhusiana na shughuli za maendeleo zilizofanywa na halmashauri hiyo. Mboya alisema lengo ni kuongeza usalama kwa watumiaji wa barabara hizo kwa maana ya wananchi wanaotoka na kuingia ndani ya mji wa Moshi.

Kwa mujibu wa Mboya, Manispaa ya Moshi ilitumia kiasi cha Sh. milioni 4.5 kila mwezi kwa ajili ya kugharamia huduma za uwashaji wa taa za barabarani ambazo zinatumia umeme wa Tanesco.

"Taa zilizokuwapo kwenye barabara zilikuwa zinatumia umeme wa Tanesco, hivyo halmashauri ikaja na mpango mkakati wa kuzibadilisha taa hizo na kuweka taa mpya zitakazokuwa zikitumia umeme wa jua, ambapo hadi sasa tayari zimesha fungwa taa zaidi ya 600," alisema Mstahiki Meya.

Alisema manispaa hiyo imeshafunga taa 650 zinazotumia mwanga wa jua (sola) katika maeneo mbalimbali ikiwamo eneo la ujenzi wa kituo kipya cha mabasi yaendayo mikoani kinachojengwa Kata ya Ngangamfumuni na Kata ya Kiusa.

Mboya alisema kwamba kufungwa kwa taa hizo zinazotumia mwanga wa jua zitawezesha kupunguza gharama kubwa ambazo Halmashauri ya Manispaa Moshi, ilikuwa ikilipa Tanesco kwa kila mwezi licha ya kwamba umeme huo ulikuwa ukikatika mara kwa mara na kusababisha mji wa Moshi kuwa giza.

"Lengo la kufunga taa hizi zinazotumia umeme wa jua ni mkakati wa kupunguza gharama za uendeshaji wa mradi wa taa za barabarani katika manispaa yetu ya Moshi, tunategemea ifikapo Aprili mwaka huu taa zote zilizokuwa zimebakia 250 zitakuwa zimekamilika kufungwa na hivyo kujiondoa kwenye mfumo wa utumiaji wa umeme wa Tanesco ambao umekuwa ni changamoto kubwa kwetu," alisema.

Aidha, alisema kufungwa kwa taa hizo, licha ya kupendezesha mji wa Moshi pia zitachangia wafanyabiashara kuongeza muda wa kufanyabiashara, na hivyo kujiongezea mapato.



Mhandisi Kakoko: Miradi ya JPM imetupaisha Bandari

Ukurasa 20



UCHUMI

Naibu Waziri alipotua Moshi kusaka jibu la kahawa 'kudoda'

Ukurasa 14

# BUFE

Ijumaa Januari 10, 2020
Nipashe

BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA



## NAIBU WAZIRI MALIASILI APIGIA DEBE HIFADHI MPYA ILIYOZINDULIWA KWAO

Ukurasa 18

UCHUMI Ukurasa 18
Biashara katika picha Ukurasa 17

UCHUMI

# Naibu Waziri alipot kusaka jibu la kaha

• TACRI wafunguka jitihada zao, wanakoishia • Ni 'mad

Na Mary Mosha, HAI

MKOA wa Kilimanjaro, ni miongoni mwa mikoa nchini Tanzania iliyokuwa iikisifika kwa uzalishaji wa kahawa bora na yenye kukubalika kimataifa.

Hiyo ilikuwa mbali na kuwa kahawa ilikuwa ikipatikana maeneo ya Uru, Kibosho, Marangu, Machame, Siha, Rombo.

Pia wazee wa Kichaga walilifanya kuwa zao la biashara lililowasaidia baadhi ya watoto kunufaika kwa kupata elimu bora iliyoleta tija katika taifa.

Katika miaka ya 1990, zao hilo lilianza kudorora kutokana na sababu mbalimbali zikiwemo za mabadiliko ya tabia nchi na mabadiliko ya kiuchumi yaliyochangia dawa kupanda, huku nguvu kazi ya vijana ikikimbilia mijini na kuwaachia wazee zao hilo.

Pia, soko la kahawa kutokana na ukosefu wa mpango mkakati, imekuwa likizalishwa chini ya kiwango na kusababisha kushuka kwa soko la umoja wa kimataifa.

Serikali iliamua kulivalia njuga kilimo cha kahawa, na vyama vya ushirika vilivyokuwa vikisimamia uzalilishaji ikibaini madudu.

Ni mkakati wa serikali wenye mchango mkubwa wa Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, imeweka msukumo mkubwa.

Katika kulitimiza, Naibu Waziri wa Kilimo, Omari Mgumba, alitua mkoani Kilimanjaro katika taasisi ya Tafiti ya Kahawa (Tacri), kupata ufafanuzi wa kinachoendelea.

**KUTOKA TACRI**

Mkurugenzi Mkuu wa Tacri, Dk. Deusdediti Kilambo, anasema wameshafanya utafiti na kubaini aina 23 za kahawa inayokabiliana na magonjwa na mabadiliko ya hali ya hewa.

Dk. Kilambo anazitaja aina 19 za Arabika zenye tija kukabili magonjwa kama chulebuni na kutu ya majani, yenye muonjo mzuri na aina nne za Robusta, zenye ukinzani na minyauko fuzari.

"Katika kulitekeleza hilo, tulishaweka mikakati pamoja Bodi ya Kahawa nchini (TCB), kubadilisha miche zaidi ya milioni 20 kwa kila mwaka, ili kuhakikisha wananchi wote wanapata miche ya kisasa," anasema.

Anasema, hadi kufikia sasa, Tacri ina uwezo wa kuzalisha miche milioni sita hadi saba kwa mwaka, hali ambayo haijafikia malengo ya kuondoa miche ya zamani na waliazimia kubadilisha miche milioni 20 kila mwaka.

Anasema, kulingana na takwimu zao hilo, bado kila mwaka tunamzigo wa kuzalisha miche bora zaidi ya milioni 14 au 13 ili tuweze kufikia lengo jambo ambalo limekuwa tatizo ingawa zipo baadhi ya halmashauri zinapewa miche mama, mbegu na wao wanajitegemea katika rasilimali fedha kwa ajili ya uanzishaji bustani.

"Zipo taasisi zinazo tuunga mkono ikiwamo vyama vya ushirika, halmashauri, mashirika binafsi na baadhi ya wakulima wadogo katika vikundi jambo ambalo ikiwa ushirikiano huo utaendelea kwa kasi tutaweza kufikia lengo na kubadilisha miche ya zamani ambayo itaweza kuleta maendeleo kwa mkulima mmoja mmoja na Taifa kwa ujumla," anasema.

Sophia Malinga ni mtafiti katika kitengo cha Usambazaji, Teknolojia na Mafunzo, anasema sababu za kutokuwapo mwitikio chanya wa miche wanayosambaza, ni baadhi ya wakulima kutokuwa na uelewa wa utunzaji miche hiyo.

"Ni kweli hakuna ufuatiliaji wowote kitaalamu unaofanywa na halmashauri, baada ya kutoa miche hiyo hali inayowafanya baadhi ya wananchi kutoipanda au kupanda bila uangalizi maalumu unaoleta matokeo chanja," anasema Mtafiti Sophia.



Naibu Waziri wa Kilimo, Omari Mgumba, akipewa maelezo na mtafiti kutoka Tacri, **PICHA ZOTE: MARY MOSHA.**

**NAIBU WAZIRI**

Naibu Waziri huyo anasema, mbali na kuwapo kwa mipango mikakati iliyoonyeshwa na taasisi hiyo, lakini bado matokeo hayaonekani kwa mkulima mmoja mmoja na taifa.

"Kwa miaka 10 mfululizo serikali inazalisha kati ya tani milioni 48 hadi 60 licha ya jitihada za serikali kuongeza mikakati katika kuongeza uwezo wa uzalishaji kwa watafiti wake kugundua miche bora ya kahawa inayostahimili magonjwa," anasema.

Anafafanua kuwa, inaonyesha kuwapo tatizo la usimamizi na ufuatiliaji wa miche hiyo mara baada ya kuzalishwa na Tacri kwenda kwenye halmashauri na vyama vya msingi, vinavyopewa bila malipo na kufanya miche hiyo kutotunzwa na kuleta matokeo yanayoweza kuleta mabadiliko kiuchumi.

> "Serikali haitakubali kwani malengo yake ni kutoka kwenye tani elfu 48 hadi 68 tuliyopo kwa sasa hadi tani 200,000 ya kahawa safi kwa mwaka baada ya miaka 5 ijayo.


Anafafanua: "Zipo taarifa za ndani zinazoonyesha kuwa miche hii ya kahawa bora pamoja na mbegu zinazotolewa hazitunzi ipasavyo licha ya kutolewa bure.

"Serikali haitakubali kwani malengo yake ni kutoka kwenye tani elfu 48 hadi 68 tuliyopo kwa sasa hadi tani 200,000 ya kahawa safi kwa mwaka baada ya miaka 5 ijayo.

"Naziagiza halmashauri kote nchini pamoja na vyama vya msingi na vikundi vyote vinavyopokea miche kutoka Tacri, kuhakikisha zinaboresha kitengo cha usimamizi na ufuatiliaji wa taarifa ya miche ya kahawa kule inapokwenda ikiwa ni pamoja na kufahamu, kitongoji, kjiji kata pamoja na namba za simu za mkulima wanaopewa mche hiyo,

# tua Moshi
# nwa 'kudoda'

## dudu' halmashauri hadi ofisa ugani



na ukubwa wa maeneo wanayopanda."

Agizo lake ni kwamba, mawasiliano hayo yasiishiwe kuweka kwenye halmashauri na vikundi, kwani zipo taarifa halmashauri nyingi zinakiuka malekezo ya Tacri, jambo ambalo serikali haitakubali.

Ushauri wake ni kuwapo kikosi cha ufuatiliaji kwa kila baada ya miezi mitatu hadi sita, kukagua matokeo ya upandaji na ushauri, kila kunakolimwa kahawa nchini.

"Tumepokea matatizo ya Tacri kuwa inakabiliwa na ufinyu wa bajeti na ukosefu wa eneo la uzalishaji (eneo lenye miundombinu rafiki ya kukuzia miche), tunayachukua kama serikali na tutayafanyia kazi," anasema.

**WAKULIMA & VYAMA**

Mkulima wa Kibosho wilayani Moshi, Agustino Kishumbuo, anasema serikali itafuatilia uhakika kufahamu maeneo miche hiyo inakoenda, kusaka mabadiliko katika uzalishaji wa zao hilo.

"Zipo baadhi ya halmashauri huchukua miche hiyo bila kufahamu hali ya halisi ya wakulima katika maeneo yao na kutokana na uzembe mkubwa unaofanya na maofsa ugani katika kila halmashauri, kwani hawana muda na kilimo.

Anasema, bado taasisi Tacri haina nguvu kubwa ya usimamizi kutokana na ukosefu wa rasilimali fedha na vitendea kazi. Anaendelea:

"Tunaiomba serikali kuangalia uwezekano wa kufanya usimamizi wa kutosha kutoka kwenye Tacri na mpaka kwa mkulima mwenye pia kuwepo na motisha kwa Mkulima atakayeweza kufanya vyema katika usimamizi na utunzaji wa kahawa."

Agustino Mlay, mkazi wa Old Moshi, anasema vipo baadhi ya vyama vya msingi viongozi wao huchukua miche na kuiacha kukauka au kuwapa wakulima bila ujuzi wa namna ya kulima na kuipanda.

Anasema mpango wa serikali wa kuzalisha kwa tija zao hili la biashara, unaweza kuleta matokeo bora ikiwa haitafanywa kwa ubabaishaji.



Mkurugenzi Mkuu wa Tacri, Dk. Deusdediti Kilambo, akitazama baadhi ya miche ya kahawa kwenye kituo chao. **PICHA ZOTE: MARY MOSHA.**



Maeneo yaliyoathirika kwa kombora nchini Iran. **PICHA: MTANDAO.**

# Shambulizi la Iran, bei mafuta yapanda

**Na Mwandishi Wetu**

GHARAMA za mafuta zimepanda nchini Iran, mara tu baada ya kambi mbili za majeshi ya Marekani nchini Iraq kushambuliwa na makombora.

Inaelezwa, bei ya mafuta ghafla imepanda kwa asilimia 1.4, sasa ikiuzwa kwa Dola za Marekani 69.21 (Sh.166,104) kwa pipa moja.

Wakati tukio linatokea hali ya mzozo katika ukanda wa Mashariki ya Kati, inaeleza gharama ya mafuta kwenye soko la dunia zilishuka kutokana na mzozo uliopo katika Ukanda wa Mashariki ya Kati.

Ni shambulio ilikuwa ni kisasi baada ya kuuawa kwa kamanda wa juu wa jeshi la nchi hiyo Qasem Soleimani, lilitokea baada ya shughuli za mazishi ya Soleimani, aliyeuawa na shambulio la Marekani siku ya Ijumaa.

Kifo chake kulisababisha wasiwasi kwamba mzozo kati ya Marekani na Iran, unaweza kuwa mkubwa zaidi.

Hali hii inaelezwa kuwa inaweza kuathiri usafirishaji wa mafuta kupitia lango la Hormuz linalotenganisha Ghuba ya Uajemi na Oman. Takribani asilimia 20 ya mafuta duniani, husafirishwa kupitia lango hilo linalounganisha eneo la Ghuba na Bahari ya Arabia.

Mlango wa Hormuz, ni muhimu kwa wasafirishaji wakubwa wa mafuta katika eneo la Ghuba - Saudi Arabia, Iraq, Umoja wa Falme za Kiarabu na Kuwait, ambazo uchumi wao unajengwa kutokana na uzalishaji mafuta na gesi.

Iran, pia inategemea kwa kiasi kikubwa njia hiyo kwa ajili ya kusafirisha mafuta, Taifa la Qatar, ambalo ni mzalishaji mkubwa duniani wa gesi, husafirisha karibu gesi yake yote kupitia lango hilo.

Baada ya mashambulizi, mamlaka ya anga ya Marekani yamezuia ndege za Marekani kuruka kwenye anga za Iraq, Iran na nchi jirani na marufuku hiyo pia inahusisha Ghuba ya Oman na maji ya Kati ya Iran na Saudia Arabia.

Mamlaka hiyo, imesema uamuzi umechukuliwa baada ya kuwapo mvutano wa kisiasa na shughuli za kijeshi katika eneo hilo.

Kabla ya mwongozo wa hivi karibuni, mamlaka hiyo ilishazuia ndege za Marekani kupaa umbali wa chini ya futi 26,000 katika anga la Iraq na kupita kwenye maeneo ya anga ya Iran, Ghuba na Oman tangu Iran ilipoidungua ndege isiyo na rubani ya Marekani, mnamo Juni mwaka jana.

Wakati huo huo shirika la ndege la Singapore, limesema ndege zake zote hazitapita kwenye anga ya Iran.

- **Kwa mujibu wa mtandao**

BIASHARA

# Naibu Waziri Bashe akanyaga Kahama awaachia mwongozo kilimo tumbaku

## • RC Shinyanga: Waziri tufikirie mahindi, mpunga

**Na Shaban Njia, KAHAMA**

TUMBAKU ni zao kubwa la kibiashara nchini Tanzania na hulimwa katika mikoa 11, ikiwapatia fursa wakulima kubadilisha maisha ikilinganisha na mazao kama mpunga na mahindi.

Mikoa hiyo inayolima zao hilo ni pamoja na Tabora, Mbeya, Kigoma, Geita, Shinyanga, Kahama, Iringa, Singida, Songwe, Mara na Mwanza. Inakadiriwa kuwa na wakulima zaidi ya 59,000 nchini.

Wilaya ya Kahama, ina zaidi ya walima tumbaku 8,900 wanaozalisha kati ya kilo milioni saba hadi 10 kila mwaka kutoka katika vyama vya msingi 48.

Mwaka jana wakulima hao walilima zaidi ya kilo milioni saba za tumbaku, kinyume na makubaliano yao na kampuni za ununuzi na kusababisha taharuki ya hatima ya tumbaku yao.

Serikali ilichukua hatua za haraka kuwatafutia soko kwenye kampuni ya Aliance One, JTI, Premium pamoja na Magefa, huku kampuni ya usambazaji wa pembejeo ya Petrobena ikijtosa kuanza kununua tumbaku msimu wa mwaka huu.



Shughuli za mavuno ya tumbaku.
**PICHA ZOTE: MTANDAO**

### WAZIRI BASHE

Hussein Bashe, Naibu Waziri wa Kilimo, akiwa kwenye mkutano wa mwaka wa Chama Kikuu cha Ushirika Kahama, (KACU), anasema kila mkulima anatakiwa kulima zao hilo bila kupangiwa na kampuni kwamba kiasi cha kulima, ingawa anakiri kikwazo cha kukosa la uhakika hujitokeza, wakulima wanapokuwa wamelima ziada.

Bashe anasema, viongozi wa vyama vya msingi wasiokuwa na sifa wamekuwa wakitumia madaraka yao vibaya kuwadidimiza wakulima wa tumbaku na pamba, hasa wakati wa urejeshaji fedha walizokopeshwa za pembejeo na mbegu.

Pia anawataka wakuu wa mikoa na wilaya nchini, kuwasimamia vyema viongozi wa vyama vya msingi na taifa na kuwawajibisha kisheria wanapokiuka.

"Kama wewe sio mkulima hauwezi kuwa kiongozi wa chama cha msingi. Tunataka kiongozi awe mkulima, anayejua changamoto na maumivu anayoyapata mkulima wakati wa kilimo.

"Wakuu wa mikoa na wilaya, mhakikishe mnahakiki vyama vya msingi kama viongozi wake wanasifa na nafasi zao," anasema Bashe.

Anasema, viongozi wa vyama vya msingi vya pamba wa maeneo mengi vamehujumu fedha za wakulima na wakulima bado hajawalipwa na wanadai fedha zao na hiyo ni kwa sababu ya kuchagua viongozi wasikuwa na sifa.

### MIKOPO & PEMBEJEO

Bashe anasema kuwa, ushirika ndio mwelekeo na njia sahihi ya kuwasaidia wakulima kuondokana na uchumi mdogo hivyo wanapokosa viongozi wenye sifa, safari ni kuwaumiza wakulima hasa wa chini.

Anasema, wakulima tumbaku na pamba, wamekuwa wakibebeshwa mizigo mikubwa ya madeni ya mikopo ambayo vyama vya msingi na vikuu vya ushirika, vimekuwa vikikopa kununua pembejeo na mbolea.

> **"Kama wewe sio mkulima hauwezi kuwa kiongozi wa chama cha msingi. Tunataka kiongozi awe mkulima, anayejua changamoto na maumivu anayoyapata mkulima wakati wa kilimo.**

"Tumekuwa tukitengeneza matatizo sisi wenyewe kwenye vyama vyetu, kampuni inalipa fedha za wakulima wa tumbaku, badala ya kuwalipa wakulima fedha zao, mnakwenda kununua pamba na mnazua migogoro ambayo inatupatia shida kuimaliza," anasema Bashe.

### KUFUFUA VIWANDA

Bashe anasema, serikali inatarajia kuvifufua viwanda vyote vilivyokufa kwa ukosefu wa mitaji na madeni, vinavyomilikiwa na vyama vikuu vya ushirika, ili kuwapatia uhakika wakulima wa zao la pamba kuwa na uhakika wa masoko yao.

Anasema, kiwanda cha ushirika kinatakiwa kuwa mfano wa kuchakata pamba, itakayokuwa imezalishwa na wakulima na akadai, viwanda hivyo vikapata fedha kutoka taasisi za kibenki kwa riba nafuu, wakulima wanaweza kupata faida.

Pia anasema moja ya viwanda vinavyoenda kufunguliwa hivi karibuni ni cha Masumbwe Lugulu na cha Chato, ambavyo vina uwezo wa kuchakata pamba kilo milioni mbili kwa mwaka.

Anasema mwaka huu, kiwanda hicho kinatakiwa kuanza kazi na wakulima waweze kuuza pamba yao kwa bei nzuri, ikiwa ni pamoja na kutengeneza mafuta ya pamba na mashudu.

Bashe anasema, wakulima wengi wa pamba wameshindwa kujiunga na vyama vya msingi na kuachana na kilimo hicho, baada ya viongozi wa vyama vya msingi kutafuna fedha za wakulima na kuona hawawasaidii katika matatizo yao.

### RC SHINYANGA

Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Zainabu, katika taarifa yake ya kilimo cha tumbaku na pamba Shinyanga, anasema chama kikuu cha ushirika wilayani Kahama kiweza kuuza tumbaku yenye thamani ya Dola za Marekani bilioni 13.2.

Anasema, fedha hizo zimezalishwa ndani ya Wilaya ya Kahama pekee na kuongeza wakulima wa zao la tumbaku wana mchango mkubwa kwenye halmashauri, wilaya, mkoa hadi taifa kwa kutoa ushuru na kuliingizia fedha za kigeni.

Telack, anasema mwaka jana kilo milioni za tumbaku zililimwa nje ya mkataba na kuzua taharuki kwa wakulima baada ya kukosa wanunuzi.

"Usimamizi mzuri wa zao la tumbaku katika mkoa huu chini ya KACU ukiwekewa umakini, wakulima wetu wataweza kunufaika na serikali itapata kodi ambazo zitasaidia katika kuleta maendeleo katika maeneo mbalimbali hapa nchini," anasema Tellack.

Mkuu wa Mkoa anamwomba Naibu Waziri Kilimo, kwamba wakulima wa mpunga na mahindi waweze nao kuingizwa kwenye vyama vya msingi na kuuza mazao yao kwa bei nzuri kama walivyo wa tumbaku na pamba.

Anasema wakulima wa mahindi na mpunga wanatumia nguvu nyingi wakati wa kuandaa mashamba, lakini hupata mavuno yao ni kidogo na wanauza kwa bei ya hasara, ikilinganisha na nguvu aliyotumia.

Tellack anasema, anaweza kuingizwa kwenye vyama vya ushirika wataweza kukopeshwa pembejeo na wakulima wa tumbaku na pamba na wanaweza kuuza mazao yao kwa bei nzuri na hii itasaidia hata kuongeza uzalishaji katika kilimo cha mpunga na mahindi.

Anasema, wakulima mpunga na mahindi wanatakiwa kuanzisha mabwawa ya maji ya kilimo ili mvua za masika zinapokatika waendelee na kilimo na kuzalisha mazao mengi ya biashara na chakula.

Tellack anasema kuna mikoa nchini wakulima wake wanavuna mavuno mara nyingi kwa mwaka.



Naibu Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe.

### TUMBAKU BORA

Stanley Mnozya ni Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa Bodi ya Tumbaku Tanzania, ansema, tumbaku bora nchini Tanzania inatoka wilayani Kahama katika Halmashauri ya Ushetu na anawataka wakulima wa tumbaku kuendelea kuendelea kushika dola kitaifa.

Anasema kuwa, kila mkulima anatakiwa kufuata kanuni za kilimo bora ili kupata tumbaku bora zaidi na itasaidia kuondokana na ukosefu wa masoko.

Stanley anawataka wakulima wa tumbaku kutowahusisha watoto katika kilimo hicho ili baadaye waweze kupata wataalamu wa kilimo kwa miaka ijayo.

Anasema nchi nyinginezo, mkulima tumbaku au pamba, anayebainika kuwatumikisha watoto katika shughuli za kilimo, mazao yake hayanunuliwi.

### KUPANDI MITI

Benson Ndengenye, ni Mrajisi wa vyama vikuu vya ushirika nchini, anayewataka wakulima wa tumbaku kuhakikisha wanapanda miti na kutumia matawi ya miti katika kukaushia tumbaku na kutengeneza mabani sanifu.

Anasema, kilimo cha tumbaku kinaenda sambamba na utunzaji mazingira, hivyo ni vyema wakulima tumbaku wakatumia matawi ya miti katika kukaushia tumbaku na sio kukata mti.

Pia anasema, kila Ofisa Mazingira wa Halmashauri, kunakolimwa tumbaku, anatakiwa kutoa elimu ya utunzaji mazingira, upandaji miti na namna ya kukata matawi ya kukaushia tumbaku.

Ndengenye anasema, vyama vikuu vya ushirika kwa baadhi ya maeneo vimejitenga na vyama vya msingi na kusababisha vyama hivyo kufanya vibaya katika kusimamia hazi za wakulima wake.

Anavitaka hata hivyo amevita vyama vikuu vya ushirika hapa nchini kujifunza namna ya kusimamia vyama vya msingi kutika Chama Kikuu cha Ushirika Kahama, hasa katika kuvielekeza namna ya kukopa na kurejesha fedha za bembejeo na utafutaji wa masoko.

### MWENYEKITI KACU

Mwenyekiti wa KACU Kahama, Emmanuel Charahani, anasema umefika wakati wa kuimarisha mfuko wa pembejeo za kilimo na fedha hizo zinatokana na kukatwa kwa kila kilo moja ya mkulima kiasi cha shilingi 400, ili wakulima wasiendelee kutegemea fedha za mikopo.

"Fedha hizi zitakaa kwenye akaunti za AMCOS zenu na zitatumika kwa kuzigatia maelekezo ya serikali na zitakuwa mali halali za wakulima na utaratibu huu utasaidia kuondokana na mikopo ambayo tumekuwa tukikopeshwa kila msimu," anasema Charahani.

Tahadhari yake, uongozi wa kampuni za usambazaji pembejeo kuelekea katika maeneo mengine kununua na kugawa pembejeo kwa wakulima kama Chunya, Kigoma, Mpanda na Serengeti.

# BIASHARA KATIKA PICHA



Meneja wa Wakala wa Vipimo Mkoa wa Mwanza (WMA), Albogast Kajungu, akionyesha fimbo ya kupimia ujazo wa lita za mafuta ya magari yanayobeba petroli, kwa waandishi wa habari waliotembelea kituo kipya cha upimaji kilichojengwa mkoani humo na serikali kwa ajili ya kuwapunguzia adha wafanyabiashara wa vituo vya mafuta wa Kanda ya Ziwa. **PICHA: ROSE JACOB**



Mchimbaji mdogo wa dhahabu kutoka mgodi wa Pamoja Mining Gold Rush, Lucas Sospeter, akiosha dhahabu kwa kutumia dhana duni, mgodini hapo, katika kijiji cha Wisolele, Kata ya Segese, Halmashauri ya Msalala wilayani Kahama, Mkoa wa Shinyanga, jana. Wachimbaji wadogo katika eneo hilo, wameiomba serikali kuwakopesha vifaa vya kisasa vya uchimbaji wa madini. **PICHA: SHABAN NJIA**



Rundo la nazi baada ya kushushwa katika Soko la Temeke jijini Dar es Salaam, jana. Nazi moja iliuzwa kwa bei ya 350/- hadi 500/-kulingana na ukubwa wake. **PICHA: JUMANNE JUMA**

BIASHARA



Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, Constatine Kanyasu (wa pili kutoka kulia), akifurahia jambo na wakuu wa wilaya nane, katika Hifadhi ya Taifa Buigiri Chato.

# Naibu Waziri Maliasili apigia debe hifadhi mpya iliyozinduliwa kwao

- Wakazi furaha 'mpaka basi', ombi lao elimu
- RC Geita aorodhesha neema uchumi kibao
- Mhifadhi Mkuu: Maajabu kibao, zahanati asili

**Na Alphonce Kabilondo, GEITA**

KATIKA kuimarisha uchumi na kuongeza pato la Taifa kupitia Sekta ya Utalii nchini, Rais John Magufuli, Julai mwaka juzi, alizindua rasmi hifadhi mpya ya Taifa ya Burigi Chato, katika kijiji cha Katente, wilayani Chato mkoani hapa.

Hapo aliibua shangwe kubwa na matumaini ya kipato kwa wananchi wa wilaya za Kyerwa, Karagwe, Muleba na Biharamulo, ambazo ni jirani na Chato.

Hifadhi hiyo mpya, kijiografia iko Kaskazini Magharibi mwa Tanzania katika mikoa ya Kagera na Geita. Pia, inadaiwa kuwa chachu ya kuinua uchumi kwa wananchi hao jirani, pamoja na pato la Taifa kwa ujumla kupitia utalii.

Hifadhi hiyo ina eneo la ukubwa wa kilomita za mraba 4707 na inatajwa kushika nafasi ya tatu kwa ukubwa, nyuma ya Hifadhi ya Taifa Ruaha.

Hifadhi hiyo inatokana na Wizara ya Maliasili na Utalii, kuyapandisha hadhi mapori ya akiba ya Burigi, Biharamulo, Kimisi (BBK) na Rumanyika, hatua iliyoidhinishwa kwa uzinduzi wa Rais Magufuli.

Sekta ya Utalii nchini inatajwa kuchangia pato la Taifa kwa takribani asilimia 17, kutoka kwa watalii zaidi ya milioni 1.5 wanaofika nchini kutembelea vivutio mbalimbali.

Baadhi ya vivutio vilivyopo nchini na kutambuliwa na Wizara ya Maliasili na Utalii na kusimamiwa na Shirika la Hifadhi za Taifa Tanzania (Tanapa) ni pamoja na Arusha, Gobe, Katavi, Mlima Kilimanjaro, Mahale, Mikumi, Manyara, Ruaha, Serengeti, Saadan,Tarangire, Uduzungwa, Kitulo, Mkomazi Saanane na Hifadhi ya Kisiwa cha Rubondo mkoani Geita hifadhi mpya ya Burigi Chato.

**WANANCHI**

Wakazi jirani wanaipongeza Wizara ya Maliasili na Utalii na Rais Magufuli, kwa kupandisha hadhi mapori hayo kuwa Hifadhi ya Taifa ya Burigi Chato.

Wakazi wa Biharamulo wanasema mapori hayo kupandishwa hadhi, pia kunawahakikishia usalama wao na kuendesha shughuli za ufugaji wa mifugo pamoja na kilimo bila kufuata taratibu za sheria.

"Tunaiomba serikali kupitia Wizara ya Maliasili na Utalii, kutupatia elimu kuhusu utalii kwa makundi ya vijana na wazee, jambo la utalii ni geni Kanda ya Magharibi," anasema mkazi wa Nyakahura Sizya kupatiwa elimu kuhusu utalii.

Juma Sizya, mkazi wa Nyakahura Wilaya ya Biharamulo, Kagera anaeleza matumaini walio nayo ni kunufaika na kuanzishwa kwa hifadhi hiyo, licha ya kutokuwa na elimu ya kutosha kuhusu masuala ya utalii naye akirejesha ombi kwa wizara mama kuwaelimisha kuhusu utalii.

Mateso Pius, mkazi wa kijiji na kata ya Nyakabango, wilayani Muleba, mkoa Kagera, kilichopo umbali wa kilomita 10 kutoka iliko hifadhi hiyo, anasema kuwa kitendo cha serikali kuyapandisha hadhi mapori hayo kuwa Hifadhi ya Taifa, ni mwarobaini dhidi ya matukio ya uhalifu kwenye barabara ya Mwanza, Geita Muleba Bukoba na Biharamulo.

Mateso anaongeza, ilhali utalii unakuja, kuna faida na hasara zake, kwa ni ajali kuna mashamba na makazi yanayoingia ndani ya eneo la hifadhi, itabidi kuhamishwa.

> **Mbunge huyo anakiri, kabla ya mapori kupandishwa hadhi kuwa Hifadhi ya Taifa, hali ya usalama ilikuwa si shwari sana, kutokana na mapori kukosa ulinzi sahihi, kuna matukio ya magari kukumbwa na uhalifu.**

**MBUNGE**

Mbunge wa Biharamulo, Oscsa Mkasa, anasema asilimia 54 ya eneo la wilaya hiyo ni hifadhi. Pia matumaini ya wananchi wake ni kuona uchumi wa wilaya hiyo na Taifa kwa jumla unapaa kupitia sekta ya utalii.

Anasema, wakazi wanaoishi kwenye vijiji vinavyozunguka hifadhi wanajishughulisha na kilimo cha mazao ya aina mbalimbali, pia Mamlaka ya Hifadhi za Taifa (Tanapa), kwa kushirikiana na Wizara ya Maliasili na Utalii wana wajibu wa kuhakikisha wanatoa elimu kwa wakazi wa wanaoishi kuzunguka hifadhi hiyo.

Mkasa anasema Tanapa wanatakiwa kutoa elimu kwa kushirikisha madiwani wa halmashauri za Biharamulo, Karagwe, Muleba, Kyerwa na Chato, ili kuwajengea uwezo wa masuala ya utalii, kwani wengi wao bado hawautambui vizuri utalii.

Anasema, kiu yake kubwa pindi mradi huo utakapoanza rasmi ni kuona Tanapa inawawezesha wakazi wa vijiji hivyo kwenye sekta ya kilimo kupitia fedha ya huduma ya jamii, kwa kuwa wakazi hao wanategemea kilimo cha mazao ya chakula na biashara, hali iyakayosaidia kujenga uhusiano mzuri kwa jamii inayozunguka hifadhi mpya.

Mbunge huyo anakiri, kabla ya mapori kupandishwa hadhi kuwa Hifadhi ya Taifa, hali ya usalama ilikuwa si shwari sana, kutokana na mapori kukosa ulinzi sahihi, kuna matukio ya magari kukumbwa na uhalifu.

Pia Mkasa anafafanua kwamba halmashauri jirani zilipoteza mapato ya ushuru wa mazao ya misitu.



**RC GEITA**

Mkuu wa Mkoa wa Geita, Mhandisi Robert Luhumbi, anasema Hifadhi ya Burigi Chato, katika ukanda wa Magharibi itachangia kuwepo idadi kubwa ugeni wa watalii kwa hifadhi, kutokana na kuwapo kiwanja kikubwa cha ndege cha kimataifa wilayani Chato.

Alipozinduliwa hifadhi hiyo, Rais Magufuli, alisema inafungua milango ya fursa kubwa kwa wafanyabiashara wa Geita na mikoa jirani, kuwekeza katika Sekta ya Maliasili na Utalii, ikiwamo ujenzi wa hoteli za kitalii, sambamba na utangazaji utalii.

Mkuu wa Mkoa Luhumbi, anasema mbali na hifadhi hiyo mpya ya Burigi Chato, mkoa wa Geita una Hifadhi ya Taifa ya Kisiwa Cha Rubondo, ambacho kiko pembezoni mwa Ziwa Victoria.

"Kwa wageni wasiokijua kisiwa hiki, kinaundwa na visiwa tisa vidogo. Kisiwa hiki pia ni makazi na mazingira ya kuzaliana samaki, wakiwamo sato na sangara wenye ukubwa wa uzito wa kilo zaidi ya 100," anasema Mkuu wa Mkoa.

Wanyama wanaopatikana katika hifadhi hiyo ni pamoja na kiboko, pongo, nzohe, fisi maji, mamba na pimbi, wanaobadilishana makazi na wanyama wengine waliohamishiwa katika hifadhi hiyo kama sokwe, tembo, mbega weusi na weupe na twiga.

**WAZIRI KANYASU**

Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii na Mbunge wa Geita Mjini, John Kanyasu, anaiambia Nipashe kuwa Tanzania inatajwa kushika nafasi ya pili duniani kwa kuwa na vivutio vya utalii, baada ya nchi ya Brazili.

Kanyasu anasema, hivyo idadi ya watalii hao wanatembelea hifadhi mbalimbali nchini bado haitoshi kutokana na uwepo wa vivutio vingi na anakiri kuwa Sekta ya Utalii.

Anasema, hifadhi hiyo mpya inatarajia kupata watalii wengi hata kutoka nchi za jirani za Kenya, Burundi, Rwanda.

Kanyasu anasema, nchi nyingi duniani zimefanikiwa katika Sekta ya Utalii, kutokana na wananchi wake kuwa na utamaduni wa kutembelea hifadhi zao.

Anasema wizara yake, imeanza kampeni ya kuwatumia viongozi wa serikali, kama wakuu wa wilaya na mkoa kuhamasisha wananchi kutalii kwenye vivutio jirani.

Niabu Waziri huyo, anasema viongozi hao wanapotembelea Hifadhi za Taifa, wakaelimishwa fursa zilizopo kwenye sekta ya utalii watakwenda kuhamasisha taasisi mbalimbali shule za sekondari msingi pamoja na wanafunzi wa vyuo vikuu, hali itakayosaidia kuongeza mapato katika sekta ya utalii.

Hata hivyo, anasema lengo la Wizara ya Maliasili na Utalii, ni kuhakikisha ifikapo mwaka 2020 idadi ya watalii wanaofika kutembelea hifadhi za Taifa inaongezeka na kufikia zaidi ya milioni mbili kwa mwaka, ili kuongeza pato la Taifa kupitia sekta ya utalii.

Naibu Waziri Kanyasu akatumia fursa hiyo, kutoa wito kwa wakazi wafanyabiashara wa mikoa ya Kagera, Geita na Mwanza pamoja iliyopo jirani, wabuni kuwekeza kwenye hifadhi mpya ya Burigi Chato.

Anasema, baada ya hifadhi hiyo kutangazwa kuwa Hifadhi ya Taifa Julai 5 mwaka juzi, Tanapa walitengeneza miundombinu ya barabara na viwanja vidogo vya ndege hifadhini, ikiwa ni hatua mojawapo kuweka mazingira mazuri kwa watalii.




Rais John Magufuli alipozindua Hifadhi ya Taifa Buigiri Chato.

Pia anaongeza, wizara hiyo huzingatia sheria kwa kuwapa kipaumbele ajira za muda na wakazi wanaoishi kuzunguka katika hifadhi.

**VIVUTIO**

Ofisa Mhifadhi Mwandamizi, Hera Haima, anasema Hifadhi ya Burigi Chato, inasifiwa kuwa 'Serengeti ya Pili' kutokana na wanyama wengi pamoja na mazingira mazuri ya kuvutia watalii, yanafanana.

Mhifadhi huyo anaelezea ndani ya Msitu wa Rumanyika, kuna kivutio cha maji moto kinachotumika kutibu magonjwa mbalimbali; Msitu wa Mutagata uliopo katika kijiji cha Kamuli Wilayani Kyerwa na kivutio cha maajabu cha kutibu tiba asilia.

"Msitu wa Rumanyika kuna kivutio cha maji moto kinachotumika kutibu magonjwa mbalimbali, pia katika Msitu wa Kijiji cha Mutagata, una kivutio cha maajabu kinachotumika kutibu watu wagonjwa pamoja na waliovunjika miguu," anasema Mhifadhi Mwandamizi Haima.

Anaongeza kuwa, wagonjwa mbalimbali wakiwamo watu waliovunjika miguu na wenye kifafa, wamekuwa wakifika kutibiwa na kupona kivutio hicho kimekuwa kimbilio kwa wagonjwa lukuki misiri ya hospitali ya rufani kwa wagonjwa wenye magonjwa sugu.

Tabibu Rubanda Kayanda, anasema kabla ya mgonjwa kupatiwa matibabu, ni lazima kufuata masharti yanayotakiwa, ikiwamo kufunga jiwe kwenye jani la mgomba na kisha kuliweka juu ya kisima na kunawa maji usoni mara tatu na kunywa mara tatu, kisha kuanza matibabu

Kayanda anasema, chanzo hicho cha maji kinatibu watu magonjwa mbalimbali eneo hilo kuna nyoka mkubwa ambaye amekuwa akitokea kwa nyakati tofauti, kutumia maji hayo na hairuhusiwi kumjeruhi wala kumuua kwa kuwa hana madhara kwa binadamu.

**MHIFADHI MKUU**

Mhifadhi Mkuu wa Burigi Chato, Damiani Saru, anataja vivutio vya wanyama ambao ni twiga pofu, pundamilia, nyati, swala, pala, nyemera, tohe,kuro,chui ,fisi pamoja na aina ya ndege wenye rangi za kuvutia wakiwemo ndege mwarabu ,hondohondo, tai, bata maji.

Aidha, anataja wanyama wa majini kama samaki, mamba na kiboko walioko ndani ya hifadhi hiyo, huku akiwahakikishia wawekezaji watalii usalama wao.

**DC ZIARANI**

Mkuu wa Wilaya ya Gairo, Mkoa Morogoro Siriel Shaidi, aliyekutwa na Nipashe hifadhini, anaishauri Wizara ya Maliasili na Utalii kuanzisha ufugaji nyuki kwenye hifadhi hiyo, kutokana na kuwa na eneo kubwa na mandhari ya kuvutia kwa watalii.



Wanyama ndani ya hifadhi hiyo. **PICHA ZOTE: MTANDAO.**

## 330 wafutiwa matokeo

**Na Mwandishi Wetu**

BARAZA la Mitihani (Necta) limefuta matokeo ya watahiniwa 333 waliobainika kufanya udanganyifu katika mitihani yake ya upimaji ya darasa la nne, kidato cha pili na kidato cha nne mwaka jana.

Akitangaza matokeo hayo jijini Dar es Salaam jana, Katibu Mtendaji wa baraza hilo, Dk. Charles Msonde, alibainisha kuwa kati ya watahiniwa hao, 142 ni wa darasa la nne, 29 ni wa kidato cha pili na 162 ni wa kidato cha nne.

Alisema baraza hilo pia limezuia kutoa matokeo ya watahiniwa 538 ambao walipata matatizo ya kiafya na kushindwa kufanya upimaji au mtihani kwa masomo yote au idadi kubwa ya masomo.

"Watahiniwa husika wamepewa fursa ya kufanya upimaji au mtihani kwa masomo ambayo hawakuyafanya kwa sababu ya ugonjwa mwaka huu.

"Waliopata fursa hii ni watahiniwa 78 wa upimaji wa kitaifa wa darasa la nne, 225 ni wa upimaji wa kitaifa wa kidato cha pili na 235 ni wa mtihani wa kidato cha nne.

Alisema takwimu za matokeo hayo zinaonyesha kuwa watahiniwa wamefanya vizuri zaidi katika masomo mengi ya msingi ambapo ufaulu wa masomo uko juu ya wastani kati ya asilimia 51.25 na 91.31.

"Takwimu za matokeo zinaonyesha kuwa watahiniwa hawakufanya vizuri katika masomo mawili ambayo ni Fizikia na Hesabu, japokuwa katika somo la Fizikia ufaulu umeendelea kuimarika kutoka asilimia 45.5 kwa mwaka 2018 hadi asilimia 48.38 mwaka 2019," alisema.

Dk. Msonde alitumia fursa hiyo kueleza kuwa matokeo hayo hayajachelewa kutolewa na kwamba yametoka kwa mujibu wa taratibu zao za baraza na kuitaka jamii kutumia mitandao ya kijamii inavyotakiwa badala ya kufanya upotoshaji.




Katibu Mtendaji wa Baraza la Mitihani la Taifa (Necta), Dk. Charles Msonde (wa pili kushoto), akizungumza na wanahabari, jijini Dar es Salaam jana, wakati akitangaza matokeo ya upimaji wa darasa la nne, kidato cha pili, na kidato cha nne. Kushoto ni Naibu Katibu Mtendaji wa Baraza hilo, Athumani Salum. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Kilio, kicheko matokeo kidato cha nne

**Na Mwandishi Wetu**

BARAZA la Mitihani (Necta) limetangaza matokeo ya mtihani wa kidato cha nne mwaka jana, yakionyesha sura mbili za 'kilio na kicheko' kwa wahusika.

Wakati wasichana wakiendelea kuongoza kwa ufaulu kitaifa, upande wa pili wa sarafu unaonyesha wavulana wamezidiwa tena katika nafasi 10 za watahiniwa bora kitaifa.

Katika kile kinachoonyesha hali si nzuri kwa watahiniwa wa kiume, safari hii wasichana wanane wameingia katika orodha ya watahiniwa 10 bora zaidi kitaifa.

Matokeo hayo yalitangazwa jana jijini Dar es Salaam na Katibu Mtendaji wa baraza hilo, Dk. Charles Msonde, yakionyesha kuwa kati ya wasichana wanane walioingia katika orodha ya wakali 10 kitaifa, saba wanatoka shule moja ya St. Francis Girls ya Mbeya.

Mtahiniwa Joan Ritte kutoka shule hiyo ndiye ayeibuka kidedea zaidi kitaifa kwa mwaka 2019. Baraza pia limeanika orodha ya shule 10 zilizoongoza ufaulu kwa miaka mitatu mfululizo ni Ibun Jazar Islamic (Pwani), St. Achilleus Kiwanuka Kijwire (Kagera), Mlalo (Tanga), Paramiho Girls (Ruvuma), Huruma Girls (Dodoma), St. Augustine Tagaste (Dar es Salaam), Nyaishozi ( Kagera), Waja Boys (Geita), Boniconsili Mabamba Girls (Kigoma) na St. Getrude Mlandizi Girls (Pwani).

Wakati shule hizo zikiendelea kufanya vizuri, baraza limetaja orodha nyingine ya shule 10 zilizoshuka ufaulu kwa miaka mitatu mfululizo kuwa ni Mbwego (Tanga), Mbezi Beach (Dar es Salaam), Maahad Istiqama (Kusini Unguja), Mwaniko (Mwanza), Nyamtelela (Mwanza), Gombe High School (Kigoma), Alliance Rock Army (Mwanza), Ndomba (Kagera), Glorious Academy (Mjini Magharibi) na Kirinjiko Islamic Seminary (Kilimanjaro).

Mikoa pia haijaachwa nyuma, Necta ikieleza kuwa mikoa mitatu iliyofanya vizuri zaidi kwa sasa ni Kilimanjaro, Arusha na Iringa na iliyoongeza ufaulu kwa kipindi cha miaka mitatu ni Iringa, Njombe na Ruvuma. Baraza pia limetoa orodha ya halmashauri 10 zilizoongoza ufaulu kwa miaka mitatu ambazo ni Madaba (Ruvuma), Mbinga (Ruvuma), Mafinga (Iringa), Bukoba (Kagera), Mpimbwe (Katavi), Pangani (Tanga), Kasulu (Kigoma), Iringa (Iringa), Njombe (Njombe) na Kilolo (Iringa).

Wakati viongozi wa halmashauri hizo wakifurahia taarifa hizo, sura nyingine ya huzuni iko kwa viongozi wenzao katika halmashauri 10 zilizoshuka kiufaulu kwa miaka mitatu.

Kwa mujibu wa Dk. Msonde, halmashauri hizo ni Mafia (Pwani), Kibiti (Pwani), Geita (Geita), Kondoa (Dodoma), Mpanda (Katavi), Kishapu (Shinyanga), Kiteto (Manyara), Bumbuli (Tanga) na Malinyi (Morogoro).

# Mwanafunzi aliyeongoza afunguka mazito

**Na Elizabeth Zaya**

MWANAFUNZI aliyeshika nafasi ya kwanza katika matokeo ya mtihani wa taifa wa kidato cha nne kutoka Shule ya Sekondari ya Mtakatifu Francis jijini Mbeya, Joan Ritte (17), ametoa ya moyoni baada ya kutangazwa matokeo hayo.

Akizungumza na Nipashe jana, Joan alisema siri ya kupata matokeo hayo mazuri ni kujituma kwenye masomo, jitihada za walimu katika kuwafundisha, jitihada za wazazi kumsimamia na msingi wa hofu ya Mungu.

"Sikutegemea kama ningepata matokeo haya leo. Safari ya elimu tangu nijiunge na shule hii haikuwa mbaya. Siku zote nilikuwa sitoki katika 'top four' (wanne bora) lakini sikutegemea kama leo hii ningekuwa mbele kuliko wenzangu. Nilikuwa naona hizo nafasi ni za watu wengine tu," alisema Joan na kuongeza:

"Kabla ya mtihani nilikuwa nimejiandaa kiasi nikajiamini kwamba nitafaulu, lakini ilipofika siku yenyewe ya mtihani, nilipatwa kidogo na hofu ya mtihani. Niliwaza kwamba huu ndio mwanzo wangu wa kuandaa maisha na je, nisipofanya vizuri itakuwaje?

Lakini nilikumbuka msingi wa imani ambao tumejengewa shuleni, nilimwamini Mungu nikapata nguvu, nikafanya mtihani wangu vizuri.

"Sitaisahau katika maisha yangu yote ile shule yangu. Mwanzoni wakati naingia pale nilikuwa si mtu wa kusali sana, lakini kutokana na misingi iliyoko pale nilijikuta ni mwombaji mzuri maana ilikuwa kama sehemu ya mambo muhimu pale na ilinisaidia kunijengea msingi mzuri wa maisha.

Nilifundishwa nidhamu ya hali ya juu na namna ya kuishi na watu wote na kujituma kwa kila jambo. Kwa hiyo ukichanganya na msaada mkubwa niliokuwa napewa na wazazi wangu vilinisaidia sana."

**USHAURI WA DADAYE**

Alisema jambo lingine ambalo lilichangia kufanya kwake vizuri ni dada yake ambaye naye katika mtihani wake wa mwisho wa kidato cha nne, aliingia katika nafasi ya wanafunzi 10 bora.

"Kitu kingine ambacho kiliniongezea nguvu na kuona hata mimi ninaweza, ni dada yangu ambaye aliwahi kufanya vizuri na kushika nafasi ya 10 kwa wasichana na waliokuwa wamefanya vizuri kitaifa katika

mtihani wao, nilihakikisha na mimi nakazana angalau nifike hapo, kwa sababu pia wazazi wangu na ndugu walikuwa wananihusia hivyo na kunitolea mfano huo kila mara.

"Lakini ninachoshukuru dada yangu naye alivyoona hivyo alijua nitapaniki, akanituliza kwa kuniambia nisisikilize maneno ninayoambiwa na watu kwamba nisipambanie matokeo wanayotaka wao, bali nihakikishe natumia uwezo wangu na kumtegemea Mungu. Nililishika sana lile neno na nilipoingia kwenye chumba cha mtihani nilitulia, niliomba Mungu anisaidie kuniondolea zile sauti nilizokuwa naambiwa kwamba lazima nifanye kama alivyofanya dada yangu," alisema.

**SAFARI YA MAISHA**

Joan alisema anatoka katika familia ya baba na mama ambao ni watumishi wa umma wenye

INAENDELEA UK. 8

BIASHARA

# Mhandisi Kakoko: Miradi ya JPM imetupaisha Bandari

## • Asema, kila alichokibuni kimekuwa 'dili' kwao TPA

**Na Elizabeth Zaya**

MKURUGENZI Mkuu wa Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (TPA), Mhandisi Deusdedit Kakoko, ana simulizi ya mambo makubwa ambayo mamlaka hiyo inajivunia kufanyika ndani ya miaka minne ya awamu iliyopo ya serikali.

Kakoko, anataja kwanza wanajivunia kukua kwa uwezo wa bandari zilizopo bahari kuu na maziwa makuu yote nchini na maboresho makubwa yaliyofanyika katika bandari zote nchini.

Pia anataja lingine ni maboresho makubwa ya mifumo ya utendaji kazi ambayo imechangia kuongeza idadi ya shehena zinazohudumiwa bandarini na ongezeko la mapato tofauti na miaka ya nyuma.

"Katika miaka minne ya kipindi cha serikali ya awamu ya tano mambo mengi yamefanyika TPA, ambayo tuna haki ya kujivunia, na katika kupima uwezo wa bandari ni pamoja na kuangalia tani za shehena ambazo tunazihudumia ukilinganisha na kipindi kilichopita.

"Kipindi cha nyuma, kuna hata baadhi ya watu walikuwa wanatudhihaki kwamba bandari haina mizigo, ni nyeupe na baadhi wakitamani hata kupiga picha, lakini kwa sasa wenyewe wanashuhudia mambo makubwa yanayofanyika bandarini, shehena zimeongezeka kwa kiwango kikubwa sana, hawana la kusema tena, kazi zinafanyika kwa uwazi na ubora.

"Mafanikio yaliyopo TPA kwa sasa ni sawa na mtu ambaye alilima shamba na kutarajia kuvuna, hayajaja kwa bahati mbaya, ni mipango madhubiti ambayo tumejiwekea ndiyo imesaidia kufanikisha yote haya."

Kakoko anasema, sasa, tayari imeimarisha pia ushirikiano na taasisi nyingine kufufua miundombinu yote ambayo kwa namna moja ama nyingine ina uhusiano wa kufanikisha shughuli za biashara za bandari ikiwamo kufufua meli kwa ajili ya kutumika kubebea shehena na mizigo.

"TPA imekuwa ikishirikiana na taasisi nyingine ili kufufua meli na miundombinu ya bandari nchini na kazi hii imekuwa ikifanyika kwa mafanikio makubwa. Kwetu sisi tukiona kuna meli nyingi tunapata usingizi, lakini meli zikikosekana hata usingizi hauji kabisa," anasema Kakoko.

"Na ushirikiano huu umeanza kuzaa matunda, meli kwa sasa ni nyingi katika bandari zetu za Tanga, Mtwara nyinginezo na zina uwezo mkubwa, kwa hiyo tukiona mafanikio ya namna hiyo ndiyo na sisi tunapata usingizi, kadhalika zikipungua hata kulala na ukapata usingizi inakuwa shida."

KULIVYOKUWA

Kakoko anasimulia wakati wanaanza kazi katika kipindi cha kwanza na bodi mpya mwaka 2016, meli zilikuwa chache sana na hali hiyo ilianza mwaka 2014/2015 na kwamba ndicho kipindi mzigo wa shehena ulipungua.

Kakoko anasema, ili kutoka katika hali hiyo, TPA ililazimika kujitoa na kuhakikisha inaweka mipango madhubuti ya kuondokana na changamoto hiyo.




Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (TPA), Mhandisi Deusdedit Kakoko.

> **"Tunamshukuru sana Rais Magufuli kwa kufufua viwanda kwa sababu hivyo kwetu kama bandari ni faida," anasema Kakoko na kuongeza:**

Anasema mwanzoni walianza kwa kuhudumia tani milioni 14.7 kwa mwaka, lakini walipoanza kuimarisha zaidi huduma bandarini wakafanikiwa kufikia tani milioni 18.1 hali ambayo iliwapa nguvu ya kuendelea kujiimarisha katika mifumo ya utoaji huduma.

Anataja jitihada hizo zilianza kuzaa matunda na hivyo kufikia hatua ambayo waliiona kwamba ndiyo inafaa kwenda nayo.

Kakoko anasema walihakikisha wanaendeleza mapambano hayo mpaka sasa ambapo wanaona wana haki ya kujivunia na kile kinachofanyika japokuwa wanaendelea kujiimarisha.

Kakoko anasema mbali na kuongezeka kwa shehena ambazo zimetokana na jitihada hizo, pia kumekuwa na ongezeko la ukusanyaji wa mapato ambayo yamepanda ikilinganisha na huko nyuma na kwamba kwa upande wa shehena walikuwa na ongezeko la asilimia 6 hadi 7 kipindi cha kwanza na sasa wamefikia asilimia tisa hadi 11 kwa mwaka.

"Katika upande wa makusanyo ya fedha nako wakati tunaingia tulikuta wanakusanya Sh. bilioni 300 hadi 320, ikabidi tujiwekee malengo ambayo tulifanikiwa kukusanya Sh. bilioni 608 , na mpaka sasa tunavyozungumza tumepanda hadi kufikia Sh. bilioni 940 na mkakati wetu ni kufikia Sh. trilioni 1.40 kila mwaka."

Pia anasema mafanikio hayo ni zao la mikakati mipya na imara waliojiwekea, ikiwamo kuongeza shehena na utoaji huduma kwa wateja wao.

Anaeleza mafanikio hayo yanatokana na mfumo wa upimaji wa utendaji kazi na ukusanyaji wa mapato kwa kila bandari na kwa kila mfanyakazi katika kila eneo.

Kwa mujibu wa Kakoko, TPA wanajivunia kipindi cha miaka minne ya serikali ya awamu ya tano ni kuwa na uwezo wa kutoa gawio kwa serikali.

"Kwa hiyo mapato ya fedha ambayo yanapatikana sasa TPA yanawiana kabisa na shehena tunayoihudumia, tunataka kujihakikishia kuendelea kuhudumia shehena nyingi zaidi siku hadi siku.

"Tunamshukuru sana Rais Magufuli kwa kufufua viwanda kwa sababu hivyo kwetu kama bandari ni faida," anasema Kakoko na kuongeza:

"Miradi inayoendelea nchini kwetu inatuinua sana sisi kama TPA, kwa mfano mradi wa reli kuna vyuma ambavyo vinaingia nchini, pamoja na mitambo mingine ambavyo vinapoletwa kwa kupitia kwenye bandari zetu, tunapata fedha.

"Hata mradi wa umeme wa Bwawa la Mwalimu Nyerere nako tutapata fedha kwa sababu malighafi za ujenzi zitapita kwenye bandari yetu."

Pia anasema muda wa upakuaji na upakiaji wa shehena kwa sasa unatumika kwa usahihi na hivyo kuruhusu au kutoa mwanya wa kuhudumia mizigo mingi bandarini.

"Muda gani meli inakaa kwenye gati. Tangu unapofungua kamba ya kwanza hadi unapoifunga na kuanza kuondoka. Tunajitahidi kuhakikisha tunaanza kuhesabu muda tangu ilipofungwa kamba ya kwanza maana ile ni huduma, ukichelewa kufunga kamba ni kupoteza muda," anasema Kakoko.

"Pia muda unaotumika kupakia na kushusha shehena nao unahesabiwa na inatakiwa muda uwe mdogo hata kama mzigo ni mkubwa kwa sababu hiyo nayo inasaidia kupima uwezo wako wa kutoa huduma, eneo ambalo tumefanikiwa kwa sasa," anasema Kakoko.

Kwa mujibu wa Kakoko, wamefanikiwa katika kipindi ambacho kuna amani kwa nchi, pamoja na uhusiano mzuri kati yao na wadau wa bandari.

"Amani iliyopo nchini na uhusiano mwema kwa jamii kupitia biashara hurudisha wateja, kwa sababu hakuna mteja anayekubali kuleta vitu vyake mahali penye kelele au katika eneo ambalo muda wowote kuna uwezekano wa kutokea vita na mzigo ukapotea," anasema Kakoko.



Sehemu ya bandari Dar es Salaam. **PICHA ZOTE: MTANDAO.**





# Barabara Mbeya-Tabora yafunguliwa

**Na Nebart Msokwa,** CHUNYA

SERIKALI imeifungua barabara ya Mbeya-Tabora iliyokuwa imefungwa kwa muda wa wiki mbili kupisha ukarabati wa daraja la Mto Lupa ambalo lilibomoka na kukata mawasiliano kati ya mikoa hiyo katika Kata ya Matundasi wilayani Chunya.

Daraja hilo lilikatika Septemba mwaka jana, baada ya gari la mkandarasi anayejenga barabara ya Chunya- Makongolosi lenye uzito mkubwa kupita, hivyo likatengenezwa daraja la muda ambalo lilikuwa linatumika mpaka Desemba 27, mwaka jana lilipofungwa.

Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Mkoa wa Mbeya iliifunga barabara hiyo na kuamuru magari yote yapite barabara ya Mkwajuni kufuatia watu wawili kudaiwa kufa maji walipolazimisha kuvuka mto huo kwa miguu wakati umejaa.

Akifungua daraja hilo ambalo limekarabatiwa na Wakala wa Barabara nchini (Tanroads) Mkoa wa Mbeya, Mkuu wa Wilaya ya Chunya, Maryprisca Mahundi, alipiga marufuku magari yenye uzito wa zaidi ya tani 10 kupita.

Alisema magari yanye uzito huo yataendelea kupita kwenye daraja la chini na endapo mto utakuwa umejaa yatalazimika kusubiri mpaka maji yapunguwe ndio yapite.

Alisema magari mengine yote yaendelee kupita katika daraja hilo ambalo limekarabatiwa huku akilitaka Jeshi la Polisi kusimamia daraja hilo ili lisibomoke tena.

"Namwagiza Mkuu wa Kikosi cha Usalama Barabarani wa Wilaya ahakikishe anapanga askari katika eneo hili kila siku kwa ajili ya kutoa maelekezo kwa madereva wanaopita katika eneo hili, kuna wengine hawajui kilichokuwa kinaendelea hapa," alisema Mahundi.

Alisema baada ya barabara hiyo kufungwa baadhi ya shughuli za uzalishaji mali katika wilaya hiyo zilikwama kutokana na kukosa usafiri na kwamba baadhi ya watu waliacha kufanya kazi kwa kuepuka kuongezeka kwa gharama za uendeshaji wa shughuli zao ikiwamo uchimbaji wa madini.

Akitoa taarifa ya ukarabati wa daraja hilo, Kaimu Meneja wa Tanroads Mkoa wa Mbeya, Mhandisi Magesa Mwita alisema daraja hilo limekamilika ndani ya wiki mbili kama walivyokuwa wameagizwa na Kamati ya Ulinzi na Usalama.

Alisema kwa sasa daraja hilo liko imara na linafaa kuendelea kutumika, lakini kwa magari yasiyozidi tani 10 na akamwomba Mkuu wa Wilaya kuwasaidia kulinda daraja hilo.

Alisema daraja hilo kwa sasa litakuwa linatumika kwa muda kabla daraja la kudumu linalojengwa na Mkandarasi anayejenga barabara ya Chunya- Makongolosi likiwa bado halijakamilika.

"Kwa sasa mkandarasi anaendelea kujenga barabara hii kwa kiwango cha lami na kuna daraja la kudumu na imara ambalo linajengwa upande wa juu, likishakamilika tutaachana kabisa na hili," alisema Mwista.

Nao baadhi ya wananchi wa Kata ya Matundasi waliishukuru serikali kwa kuifunga barabara hiyo kwa muda wakidai kuwa endapo wangeendelea kuvuka chini maafa yangetokea mengi zaidi.

Mmoja wa wananchi hao, Amos Simon, alisema kabla ya kufungwa kwa barabara hiyo kuna wananchi walizama na wakafa na wengine wakaokolewa hali ambayo ilikuwa inahatarisha maisha ya watu wengi.

Alisema hata gharama za usafiri ziliongezeka katika wilaya hiyo kutokana na kwamba walikuwa wanalazimika kutumia barabara ya Mkwajuni wanapotaka kwenda Mbeya Mjini.



Kaimu Meneja wa Wakala wa Barabara Tanzania (Tanroads), Mkoa wa Mbeya, Magesa Mwita (wa pili kulia), akitoa maelezo kwa Mkuu wa Wilaya ya Chunya, Maryprisca Mahundi, namna daraja la Mto Lupa, lililokuwa limefungwa kwa wiki mbili lilivyokarabatiwa. **PICHA: NEBART MSOKWA**

## TFS yafunguka ukataji wa miti

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

UONGOZI wa Wakala wa Misitu Tanzania (TFS) Mkoa wa Mbeya, umesema unakabiliana na tatizo la kasi kubwa ya ukataji wa miti kwenye misitu ya hifadhi unaofanywa na wananchi, hali ambayo inahatarisha ustawi wa misitu hiyo.

Hayo yalisemwa juzi na Meneja wa TFS Mkoa wa Mbeya, Innocent Lupembe, wakati alipokuwa anazungumza na gazeti hili kuhusu uhifadhi wa misitu katika mkoa huo.

Lupembe alisema mkoa huo una hifadhi 23 zinazosimamiwa na TFS na kwa sasa wako mbioni kuongeza ya 24 ambayo ni ya Msitu wa Kambikatoto wilayani Chunya ambayo inadaiwa kuwa itakuwa kubwa kuliko zote.

Alisema misitu hiyo inapatikana katika wilaya tano za Mbeya, Chunya, Rungwe, Mbarali na Kyela na kwamba tatizo kubwa linalozikabili hifadhi hizo ni kasi ya uvamizi na ukataji wa miti unaofanywa na wananchi wasiokuwa waaminifu.

"Tatizo linalosababisha yote haya ni ushiriki mdogo wa wananchi katika usimamizi wa rasilimali za misitu na nyuki, hii inaifanya jamii kukata miti kwa kiasi kikubwa na hivyo kuhatarisha uwepo wa raslimali hii muhimu," alisema Lupembe.

Alisema kwa sasa wanaendelea kutoa elimu kwa wananchi juu ya umuhimu wa kuhifadhi misitu kwa kufuga nyuki na kuwagawia mizinga ili kuwashawishi kuwa sehemu ya wahifadhi wa misitu.

Hata hivyo, alisema misitu mingi iliyohifadhiwa ni vyanzo vya mito inayotumika kwa ajili ya kunywa na kutumika kwenye shughuli za kilimo na ni muhimu kwa ajili ya kukabiliana na mabadiliko ya tabia nchi.

# Waomba maofisa kilimo kukabili wadudu

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

BAADHI ya wakulima wa mahindi, wamewaomba maofisa kilimo kuwasaidia kukabiliana na wadudu walioanza kushambulia mahindi yakiwa shambani na kusababisha yasikue hali ambayo inaweza ikawaingiza hasara.

Wakizungumza na Nipashe kwa nyakati tofauti, wakulima hao walisema wadudu hao aina ya Kanitangaze, wanakula mahindi kuanzia yakiwa madogo mpaka yatakapokuwa yamezaa na hawasikii dawa ya aina yoyote.

Mmoja wa wakulima hao, Joseph Mwashitete, mkazi wa Utengule katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya, alisema ili kuwadhibiti wadudu hao inatakiwa kupulizia dawa kila wiki na kwamba ukichelewa wanakula kiini cha mhindi na kuufanya udumae.

Alisema hakuna dawa ambayo imethibitishwa na wataalamu kuwa inawaua wadudu hao na hivyo wakulima wanalazimika kwenda kununua sumu za aina yoyote kwenye maduka na kupulizia hali ambayo wakati mwingine hazileti matokeo.

"Hawa wadudu mwanzoni walikuwa wanakula zaidi nyanya na wakulima tumeingia hasara sana na baadhi waliacha kabisa kulima nyanya, sasa hivi wamevamia mahindi, kila ukipiga dawa ni lazima ufanye kazi ya kwenda kuchunguza kama wamekufa," alisema Mwashitete.

Alisema wadudu hao wanashambulia zaidi mazao wakati huu ambao mvua inanyesha kwa kufululiza kwa madai kuwa mvua inapunguza nguvu ya dawa wanazotumia.

Naye Jerome Mbozyo, kutoka Ilota katika Kata ya Mshewe Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya, alisema wataalamu wa kilimo hawawatembelei katika maeneo yao kwa ajili ya kuangalia changamoto wanazokabiliana nazo kwenye kilimo.

Alisema kutokana na hali hiyo, wanaamua kuanza kubuni wao wenyewe namna ya kukabiliana nazo hali ambayo wakati mwingine wanashindwa kutokana na kutokuwa na elimu ya kutosha juu ya njia za kupambana na visumbufu vya mimea.

"Kipindi hiki ambacho serikali inasisitiza mapinduzi ya viwanda ndicho kilifaa tuwe na maofisa kilimo katika kila kijiji, lakini sasa bado hawapo na sisi tunalima kwa kutumia uzoefu wetu hali ambayo inatufanya tusipate tija," alisema Mbozyo.

Hata hivyo alisema wadudu aina ya Kanitangaze walianza miaka ya hivi karibuni, na kwamba kabla ya hapo walikuwa wanakabiliana na changamoto za kawaida.

Mmoja wa maofisa kilimo wastaafu anayeishi katika Kata ya Nsalala kwenye Mamlaka ya Mji Mdogo wa Mbalizi ambaye hakutaka kutaja jina lake, alisema kwa sasa maofisa kilimo wana utaalamu wa nadharia badala ya vitendo na hivyo hawawezi kuwasaidia wananchi.

Alisema baadhi ya maofisa hao wanashindwa hata kulima mashamba yao na kwamba ikitokea akalima hatumii utaalamu unaotakiwa na hivyo kuwafanya wakulima kushindwa kujifunza kwao.

Alisema kwa sasa wakulima wanaona ni vema wakajifunze kwenye mashamba darasa ya kampuni za kuzalisha na kusambaza pembejeo za kilimo kuliko kwa hao maofisa kilimo.





# Waziri ataka udhibiti mabasi usafirishaji wa vifurushi

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

NAIBU Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Atashasta Nditiye amesema kuna mabasi ya abiria yanayosafirisha barua, vifurushi na vipeto bila kuwa na leseni ya kutoka huduma hiyo.

Aidha, ameitaka Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) kufanya ukaguzi wa kushtukiza na kuchukua hatua dhidi ya wahusika.

Akifungua mkutano wa siku tatu wa Baraza la Wafanyakazi na Postamasta, Nditiye alisema pamoja na mwaka jana kukataza mabasi ya abiria ambayo hayana leseni kufanya biashara hiyo bado yanaendelea.

"Mwaka jana nilipiga marufuku mabasi ya abiria ambayo hayana leseni ya kufanya huduma ya kusafirisha barua, vifurushi na vipeto kuacha biashara hiyo, lakini nimebaini kuwa baadhi ya mabasi bado yanaendelea kufanya hiyo biashara, ni marufuku kampuni ambayo inafanya huduma hiyo bila leseni," alibainisha.

"Nawaagiza TCRA, kufanya ukaguzi wa kushtukiza kwenye mabasi hayo, wanatakiwa kufanya kama Mamlaka ya Usafiri Ardhini (Latra) ambao wanaamka asubuhi na kwenda kufanya ukaguzi, kampuni yoyote ikikutwa inafanya shughuli hizo kinyume na sheria, ichukuliwe hatua za kisheria haraka," alisisitiza.

Aidha, Nditiye aliwataka wafanyakazi wa Shirika la Posta Tanzania kuongeza ufanisi na tija kwenye shirika lao ili kuongeza gawio serikalini na kuongezeka kipato cha wafanyakazi.

"Napenda kuona kuongezeka kwa gawio serikalini kunakoenda sambamba na kuongezeka kwa pato la kila mfanyakazi kila mwaka na ili kuwezesha hili ni lazima utendaji mahiri unahitajika na ufanisi wa utendaji kazi uwepo," alisema.

Naye Postamasta Mkuu wa Shirika hilo, Hassan Mwang'ombe alisema mwanzoni mwa mwezi ujao shirika litaingia rasmi kutoa huduma kidijitali.

Alisema tayari mifumo yote ya Tehama imefungwa na kuungaisha ofisi zote za shirika hilo la na kuwa kwa sasa wapo katika majaribio.

"Mwishoni mwa mwezi huu au mwanzoni mwa mwezi ujao, Shirika la Posta Tanzania litaingia kiditijatili, tutakuwa tunatoa huduma zetu kwa mtandao, kwa sasa tuko katika majaribio," alisema.

Alisema pia shirika liko katika mkakati wa kufanya mabadiliko makubwa ya kimuundo na mfumo wa utendaji ambao umelenga kuboresha shughuli kwa kufanya kazi kwa ujuzi na tija zaidi.



Mratibu wa shirika lisilo la kiserikali Kisedet lililopo mkoani Dodoma, Madango Mukama, alizungumza na wadau mbalimbali wakiwamo mahakimu, polisi magereza na maofisa ustawi wa jamii, kwenye semina ya utetezi wa haki ya watoto wanaofanyiwa ukatili iliyofanyika jana jijini Dodoma. **PICHA PETER MKWAVILA**

# Serikali yaimarisha mkakati wa kuwezesha makandarasi wazawa

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

SERIKALI imeweka mikakati ya kuhakikisha inawezesha na kuwajengea uwezo makandarasi wazalendo, ili watekeleze miradi mikubwa badala ya kusubiri makandarasi kutoka nje.

Aidha, makandarasi wa kigeni ambao wanatekeleza miradi mikubwa hapa nchini wanatakiwa kufanya kazi na wazawa ikiwa ni pamoja na kuwapatia ujuzi.

Hayo yalisemwa na Katibu Mkuu wa Wizara ya Ujenzi, Elius Mwakalinga, wakati akifungua kikao cha mashauriano baina ya Wizara ya Ujenzi na makandarasi wazalendo waliosajiliwa nchini kuhusu ushiriki wa makandarasi wazawa katika miradi ya ujenzi.

Mwakalinga alisema kutokana na kuwapo kwa upungufu mbalimbali katika sheria ya kuwatambua makandarasi wa ndani na kuonekana kuwa bado hawawezi kufanya kazi na makandarasi wa nje, ndiyo maana kuna kuwapo na mazungumzo juu ya kutaka kurekebisha sheria.

"Kutokana na kuwapo upungufu katika sheria ya kuwatambua makandarasi wa ndani tunajitahidi kufanya namna ili waweze kutambulika," alisema Mwakalinga. Alisema kuwa makandarasi wa ndani wamekuwa wakikumbana na changamoto mbalimbali, ikiwa ni pamoja na kutowezeshwa kiuchumi jambo ambalo limesababisha makandarasi wa ndani kushindwa kufanya kazi zao.

Aidha, alisema kuwa kutokana na kuwa na sera ya kuitaka Tanzania kuwa na uchumi wa kati ni lazima makandarasi wa ndani wajengewe uwezo wa kitaalamu, kiuchumi na kielimu ili nao waweze kutoka nje ya nchi ili watekeleze miradi mikubwa kama inavyotekelezwa na wageni. Mbali na hilo kwa sasa makandarasi kutoka nje ni lazima washikiliane na kwa kupeana majukumu ili kila mkandarasi aweze kushughulikia sehemu mbalimbali ya kitaalamu.

Katika hatua nyingine, Mwakalinga alisema kuna haja kubwa ya kuwa na taarifa sahihi za makandarasi ili wote ambao wanakidhi vigezo wawe moja kwa moja katika mtandao ili mkandarasi wanaotoka nje wajuwe ni makandarasi gani ambao watafanya nao kazi za kutekeleza miradi hapa nchini.

"Tunachotaka kufanya sasa ni kuhakikisha makandarasi wa kigeni pamoja na makandarasi washauri wanapokuja katika kutekeleza miradi yao mikubwa ni lazima watoe elimu ya matumizi ya mitambo mikubwa wanayoitumia na kutoa elimu kwa makandarasi wa ndani katika maeneo ambayo hawajaweza kuyajua ili kuwawezesha makandarasi wa ndani kupata uelewa wa kutosha.

"Makandarasi wa wazalendo wakiisha jengewa uwezo wa kiuchumi na kielimu itakuwa rahisi hata wao kutoka nchini na kwenda kutekeleza miradi mikubwa jambo litakalosaidia kuwawezesha kipato na kufanya taifa kupata fedha badala ya fedha zetu kutoka ndani na kwenda nje ya nchi," alisema Mwakalinga.

Naye Kaimu Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Barabara Tanzania (Tanroads), Crispianus Ako, katika kikao hicho alisema licha ya kushirikiana vyema na makandarasi wa ndani, aliwataka waache kulalamika na badala yake waangalie namna ya kutoa ushauri ambao utakuwa na manufaa kwa serikali.

Katika hatua nyingine Ako, aliwataka makandarasi kuwa makini na waaminifu wanapewa miradi waitekeleze kwa kiwango ili kuondoa dhana ya kutokuamini watu wa ndani na badala yake kuwaona wa nje kama ni bora zaidi.

Aidha, aliwataka makandarasi kubadili mtazamo na kuona ni namna gani ya kuweza kupata miradi mikubwa ambayo wanaweza kuitekeleza badala ya kusubiri wapatikane makandarasi wasiokuwa wazalendo.

Wakichangia katika kikao hicho baadhi ya wakandarasi wazawa walisema kuwa wakati mwingine wanashindwa kutekeleza miradi ambayo wanaipata kutokana na kukosekana uwezeshwaji na wakati mwingine wanapokwenda kukopa kwenye taasisi za kifedha wanajikuta wanakuwa na riba kubwa na wakati mwingine kucheleweshewa mikopo.

# Wenyeviti mitaa bado walilia mihuri

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

MWENYEKITI wa wenyeviti wa serikali za mitaa 222, Matwiga Kyatya, wameitaka Tamisemi kutoa tamko kuhusu malalamiko ya viongozi hao kunyimwa vitendea kazi tangu walivyoapishwa Novemba 28, mwaka huu.

Aidha, viongozi hao wameitaka Tamisemi kueleza umma ni nani ambaye anazuia wenyeviti hao kupata mihuri kwa ajili ya kuwahudumia wananchi.

Kwa muda sasa kumekuwa na mvutano baina ya Naibu Waziri wa Tamisemi, Mwita Waitara, Katibu Mkuu wa Tamisemi, Joseph Nyamhanga na Mkurugenzi wa Jiji la Dodoma, Godwini Kunambi, wote wakidai kuwa hawajui kwanini viongozi hao hawajapewa vitendea kazi.

Kyatya ambaye ni Mwenyekiti wa Mtaa wa Mnadani, alisema tangu waapishwe ni mwezi mmoja na siku 12 wananchi hawajapatiwa huduma jambo ambalo linasababisha watu wengi kushindwa kupata haki zao ambazo wanatakiwa kuzipata kutokana na kukosa huduma ya mihuri.

Mwenyekiti huyo alisema kitendo cha uongozi wa Jiji kushindwa kuwapatia mihuri wenyeviti hao kumesababisha huduma za kijamii kushindwa kuendelea.

Alizitaja kuwa ni pamoja na wajasiriamali kukosa mikopo kwa wakati, watu wanaokata kuwathamini ndugu zao polisi kushindwa kufanya hivyo, wanafunzi wanaotakiwa kujiunga na masomo hata wale ambao wanatakiwa kupata uthibitisho kutoka mtaani ili kupata ajira wanakwama.

Kutokana na hali hiyo Kyatya alisema uongozi wa Tamisemi unatakiwa kutoa tamko kwa umma ili ujue nini kinakwamisha, ili wananchi waondokane na dhana kuwa wenyeviti waliopo madarakani hawataki kuwapatia huduma muhimu na wakati mwingine kudhani kuwa wenyeviti hao hawataki kutoa huduma kwa lengo la kutumia mwanya huo kupata rushwa.

Hivi karibuni, wenyeviti walitoa siku saba kwa Mkuu wa Wilaya ya Dodoma Mjini, Patrobasi Katambi, kutoa ufafanuzi na kuondoa utata juu ya wenyeviti hao kutokuwa na vitendea kazi hususani mihuri ambayo ni muhimu kwa watendaji hao.

Siku saba ziliisha bila kupata ufumbuzi na kulazimika kurudi katika ofisi kwa DC na majibu ya kiongozi huyo yalikuwa ya kuwatuliza na kuwaeleza kuwa suala hilo atalipeleka kwa katibu mkuu Tamisemi ili kulipatia ufumbuzi.

Siku chache baadaye Waziri, Katibu Mkuu Tamisemi na Mkurugenzi wa Jiji la Dodoma kwa nyakati tofauti walisema hawajui tatizo hilo.





# Karume asisitiza elimu kwa watoto

Na Rahma Suleiman,
ZANZIBAR

RAIS mstaafu, Amani Abeid Karume, amewataka wazazi na walimu kuendelea kuunganisha nguvu zao kuhakikisha watoto wao wanalitumia ipasavyo jengo jipya la ghorofa la Shule ya Uweleni Pemba.

Akizungumza kwa niaba yake na kufungua jengo jipya la Shule ya Sekondari ya Uweleni iliopo Wilaya ya Mkoani Pemba, Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa pili wa Rais, Mohammed Aboud Mohammed, aliwataka wazazi na walimu kushirikiana kuhakikisha watoto wanapata taaluma.

Alisema kuna umuhimu mkubwa kwa wazazi na walimu kuhakikisha wanasimamia malezi ya watoto ili kulinda mila na desturi za nchi kutokana na mmomonyoko wa maadili wa sasa unaochangiwa na utamaduni wa kigeni.

Aliwasihi watoto wao kuzitumia vizuri fursa zilizopo kwa kujisomea kwa kuwa serikali inatumia gharama kubwa katika kuwawezesha wanafunzi katika elimu ili Taifa liweze kuwa na wataalamu wake.

Aliwataka wanafunzi kutojiingiza katika matumizi ya dawa za kulevya na kuepukana na maambukizi mapya ya Ukimwi pamoja na vitendo vya udhalilishaji.

Alisema serikali chini ya Rais Mohamed Shein itaendelea kutoa elimu bure kwa wote pamoja na kujenga majengo mapya ya shule ili kusaidia upungufu wa madarasa na madawati kwa lengo la kuwafanya wananchi wake wanasoma katika mazingira mazuri na ya kisasa.

Naye Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, Riziki Pembe Juma, aliwapongeza wananchi wa Uweleni kwa moyo wa uzalendo waliouonyesha katika kuchangia ujenzi wa jengo hilo na kukamilika kwa haraka.

# Shein atunuku nishani za Mapinduzi

Na Rahma Suleiman,
ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar, Dk. Ali Mohamed Shein, ametunuku nishani ya Mapinduzi, ya Utumishi uliotukuka na ya Ushujaa kwa viongozi, watumishi wa umma, maofisa na wapiganaji wa Idara Maalum za SMZ na wananchi mbalimbali wenye sifa maalum.

Hafla hiyo ilifanyika juzi katika viwanja vya Ikulu Mjini Zanzibar, ambayo ni mwendelelezo wa maadhimisho ya Miaka 56 ya Mapinduzi ya Zanzibar ya Januari 12, 1964. Akizungumza katika hafla hiyo, Katibu Mkuu Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Salum Maulid Salum, alisema Rais Dk. Shein

ametunuku nishani 37 ya Mapinduzi, nishani 10 ya Utumishi uliotukuka na 25 ya Ushujaa kwa viongozi, watumishi wa umma, maafisa na wapiganaji wa Idara Maalum za SMZ pamoja na wananchi mbalimbali.

Sherehe hiyo ilihudhuriwa na watunukiwa 72 ambao kati ya hao 22 ni marehemu ambao nishani zao zimepokelewa na wawakilishi wao na 50 wako hai ambapo nishani zao walipokea wenyewe au kwa niaba yao.

Alisema watunukiwa wote sifa zao zimekidhi matakwa ya nishani hizo ambapo nishani ya Mapinduzi hutolewa kwa mtu ambaye aliasisi, alishiriki au aliyatukuza na aliyaenzi Mapinduzi ya Zanzibar.

Katika hafla hiyo, Dk. Shein alitoa nishani ya Mapinduzi kwa viongozi na wananchi wenye sifa husika akiwamo Asha Abdalla Juma, Meja Jenerali mstaafu Khamis Rajab Semfuko, Kamishna wa Polisi mstaafu marehemu Mussa Khamis Ramadhan, Kanali mstaafu Ahui Hassan Ahui, Kapteni mstaafu

Mohammed Mahamoud Juma, Kamanda mstaafu Abdi Makame Mbai, Msaidizi Mwandamizi Kamishna wa Polisi mstaafu Saada Ibrahim Makungu.

Wengine ni Msaidizi Kamishna wa Polisi mstaafu marehemu Issa Haji Pandu, Luteni Kamanda mstaafu Ali Yussuf Mohamed, Luteni Kamanda mstaafu Shafi Mohamed Hanif, Kapteni mstaafu marehemu Hassan Juma

Reli, Mrakibu Mwandamizi wa Polisi mstaafu Sofia Hebber Masewa na Khatib Mwinyichande. Rais Shein pia, amewatunuku Profesa Ali Seif Ali Mshimba, Amour

Abdalla Khamis, Said Salim Bakhresa, Ahmada Yahya Abdulwakil, Haji Mbarouk Ameir, Haji Nasibu Haji Nyanya, Khalid Ali Kombo, Khatib Haji Khalid, Hassan Juma Khamis, Simai Jafar Bai, Zaidu Juma Ussi, Salmin Juma Jecha, Haji Seti Haji.

Wengine ni Lela Nassor Khamis, Songoro Omar Kiroboto, Khadija Hassan Aboud, Fatuma Issa Juma, Daud Suleiman Ali, marehemu Kheir Idd Milao, marehemu Ahmada Ali Shamata, marehemu Hassan Juma Hassan, marehemu Khamis Haji Mpera, marehemu Ame Vuaa Ame na marehemu Abdi Ramadhan Shemhaji.

Rais Dk. Shein pia, ametoa nishani ya Utumishi uliotukuka kwa watumishi wa serikali, Mahakama na Baraza la Wawakilishi wakiwemo Maryam Abdallah Yussuf, Zuleikha Kombo Khamis, Janeth Nora Sekihola,

Saleh Ali Salim, Luteni Kamanda Subira Mohamed Hassan, marehemu Juma

Ali Juma, marehemu Silima Mkindwi Khamis, marehemu Abdallah Waziri Ramadhan, marehemu Balozi Ali Othman Korosheni na marehemu Abel Anthony De Silva.

Pia ametunuku nishani ya Ushujaa kwa Watumishi wa Idara Maalum za SMZ akiwamo Luteni Kanali Mstaafu Ali Ussi Ali, Luteni Kanali mstaafu Justice Issack Anthony, Meja mstaafu Mohamed Hamza Yussuf, Kapteni mstaafu Fatma Abdalla Mussa, Kapteni mstaafu Juma Ali Jongo, Kapteni mstaafu Ramadhan Mango Jilungui,

Luteni mstaafu Abdalla Hassan Rehani, Waranti Ofisa Mteule Daraja la I mstaafu Kona Haji Juma, Ofisa Mteule Daraja la 2 mstaafu Othman Bakari Kwae.

Wengine ni Ofisa Mteule Daraja la 2 mstaafu Abdallah Ali Abdallah, Sajin Taji mstaafu Suleiman Mgeni Suleiman, Sajin Taji mstaafu Rehani Uled Khamis, Sajin mstaafu Iddi Khamis Omar, Sajin Mstaafu Ali Khatib

Ali, Koplo mstaafu Ali Haji Issa, Sea 1. Ali Mossi Haji na Hija Hassan Hija.

Kadhalika, Rais Shein alimtunuku Koplo Marehemu Said Abdulrahman Juma, Private marehemu Sharif Salim Suleiman, Constebo wa Polisi marehemu Haji Muslim Simai, marehemu Bakari Juma Hussein, marehemu Ali Juma Ame, Marehemu Hafidh Silima Kona, marehemu Issa Daud Omar na marehemu Mohamed Abdallah Mohamed.



Rais wa Zanzibar, Dk. Ali Mohamed Shein, akimvisha Nishani ya Mapinduzi, Mzee Haji Nasibu Nyanya, katika hafla ya kuwatunukia nishani viongozi na wananchi mbalimbali iliyofanyika Ikulu mjini Zanzibar juzi. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Agizo mapato ya soko kulipiwa benki

Na Rahma Suleiman,
ZANZIBAR

WAZIRI wa Kazi, Uwezeshaji Wanawake na Watoto, Maudline Cyrus Castico, ameliagiza Baraza la Manispaa Mjini Zanzibar kuhakikisha kuwa mapato yote yatayokusanywa katika soko la machinjio ya kuku Darajani kuwa yatalipiwa benki.

Akizungumza wakati wa uzinduzi wa soko jipya la kisasa la kuku huko Darajani, alisema manispaa ina mambo mengi ya kufanya kazi hiyo ikiwamo kuweka mji katika hali ya usafi, kujenga majengo mapya na ya kisasa na masuala mengine, hivyo utunzaji wa fedha uzingatiwe kuepuka uvujaji ili malengo ya manispaa yafikiwe.

"Mpunguze kutegemea hazina, ujenge utamaduni malipo ya pesa za soko la kuku mlipie benki," alisema Waziri Castico.

Alisema malengo yao yatatimia iwapo pale malipo ya kodi na makusanyo mengine yatalipiwa moja kwa moja benki kwani ndiko kwenye dhamana ya utunzaji wa fedha za serikali na mashirika.

Aidha, waziri huyo aliliambia baraza hilo kuwa kwa kazi nyingine za manispaa waingie ubia na watu kwani kufanya hivyo ni kutoa fursa ambazo zinahitajika na kulifanya baraza lijiendeshe lenyewe

Naye Naibu Waziri Ofisi ya Rais na Tawala za Mikoa na Idara Maluum za SMZ, Shamata Ame, aliitaka Baraza la Manispaa kufanya kazi ipasavyo ili juhudi zao ziweze kutambuliwa na kuthaminiwa.

Alisema serikali itahakikisha masoko yote yatatengenezwa katika mifumo inayokubalika duniani bila ya kuangalia maeneo au mahali yalipo. Mkurugenzi wa Baraza la Manispaa ya Mjini, Said Juma Ahmada, alisema wameandaa mikakati ya kuhakikisha mapato yanapatikana katika soko hilo.

# Waomba kuuza mabondo kwa leseni za uvuvi

**Na Neema Emmanuel,**
MWANZA

WAVUVI wa Mwalo wa Butuja wilayani Ilemela mkoani Mwanza, wameiomba serikali kuwaruhusu kuuza mabondo kwa kutumia leseni zao za uvuvi.

Wakizungumza na Nipashe jana kwa nyakati tofauti wavuvi hao walisema ili mabondo, ambayo ni sehemu ya ndani ya tumbo la samaki, yaweze kuwanufaisha, serikali iwaruhusu kutumia leseni ya uvuvi kuyauza mabondo hayo, badala ya utaratibu wa sasa kuwa na leseni mbili za uvuvi.

Emmanuel Nyagwes alisema changamoto inayowakwamisha ni kukamatwa na kupigwa faini na maofisa wa uvuvi wanapokutwa wanauza mabondo bila ya leseni ya kuuzia wakati wanakuwa nayo ya uvuvi.

"Niiombe serikali itambue leseni ya uvuvi ili tuweze kutumia hata kuuza mabondo kwani samaki zinakuwa zetu na tunaamua kuzipasua ili tuuze mnofu pekee yake," alisema na kuendelea:

"Kwa nini waje watukamate wakati tunakuwa tunatambulika kisheria na vielelezo vya kuwa mimi ni mvuvi ninakuwa navyo."

Pia alisema kumekuwa na changamoto ya wenye viwanda kujipangia bei ya mabondo hasa pale samaki wakipatikana kwa wingi. Mfano, unakuta kilo ya= bondo wanauza Sh. 320,000, lakini wao wanakuambia Sh. 240,000.

"Hivyo ili kuondokana na hali hiyo, serikali iweke mfumo wa kuwa na bei elekezi pamoja na kuwapo na viwanda vya mabondo vya wazawa, na hata vya wageni ambao bei yao imnufaishe mvuvi na iendane na nchi za jirani kama Uganda," alisema.

Mwita Chacha alisema, serikali ifanye jitihada za kuhakikisha wadau wa sekta ya mabondo wanafahamu bei za mabondo katika soko la ndani na nje, huku wakitoa fursa ya wao kuuza nje ya nchi.

Alisema, pia kuwe na bei au utoaji wa taaarifa kuhusu bei za samaki sokoni kwani inapelekea wao kupata hasara kwani wanaweza kununua samaki kwa Sh. 200,000 na kuuza mnofu Sh. 50,000 wakitegemea kuwa bondo litamsaidia kupata faida na kurejesha mtaji, lakini badala yake anakuta bei ya bondo inakuwa chini ya hapo.

Kaimu Ofisa Mfawidhi wa Ulinzi wa Rasilimali za Uvuvi Kanda ya Ziwa, Roman Mkenda, alisema kwa mujibu wa Sheria ya Uvuvi ya mwaka 2003 na kanuni zake za mwaka 2009, zinamtaka mtu anayekusanya mazao ya samaki kuwa na leseni inayohusiana na aina ya mazao husika anayokusanya.

"Hivyo mvuvi atapaswa kuwa na ya uvuvi na wa mabondo anatakiwa kuwa na leseni ya mabondo, kwa vile wa mabondo anakuwa anafanya biashara anapaswa kukata pia leseni ya biashara kwa mujibu wa sheria," alisema.

Hivyo kama mvuvi kwa maana anayetoa samaki ziwani anapotaka kukusanya na mabondo mbali na kuwa na leseni ya uvuvi lazima awe nayo leseni ya mabondo kwani kitendo cha kutoa bondo kwenye samaki huo ni uchakataji," alisema Mkenda.

Hata hivyo alisema, suala la bei elekezi kuhusiana na mabondo serikali bado inalifanyia kazi ili kupata muafaka wa kuondoa mkanganyiko na changamoto iliyopo sasa.



Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Mary Mwanjelwa (kushoto), akizungumza na mama mzazi wa mnufaika wa Tasaf, Upendo Shila Mashantala, alipomtembelea nyumbani kwake kukagua utekelezaji wa mradi wa Tasaf, katika kijiji cha Kisiriri, kilichopo Halmashauri ya Wilaya ya Iramba, mkoani Singida juzi. **PICHA: UTUMISHI**

# Maduka kuwapa ajira Watanzania

**Na Mwandishi Wetu**

WATANZANIA wameahidiwa kuendelea kunufaishwa kwa fursa ya ajira za maduka.

Fursa hiyo imeahidiwa na maduka makubwa ya kitanzania yajulikanayo kama Mr Discount Hyper Supermarkets ya jijini Dar es Salaam.

Aliyetoa ahadi hiyo ni Mkurugenzi Mtendaji wa maduka ya Mr Discount, Khalid Salim, alipokuwa akizungumza jijini Dar es Salaam wakati wa maandalizi ya ufunguzi wa tawi jipya la Mr Discount lililopo katika Mtaa wa Samora.

Salim alisema kwamba kampuni hiyo itaendelea kutoa kipaumbele cha ajira kwa Watanzania.

"Sera yetu tunataka watu wetu wapate unafuu wa bei kuliko sehemu nyingine yoyote. Tunataka biashara yetu ifanane na jina lenyewe Mr Discount (bwana punguzo)," alisema.

Alisema walipata wazo la kuanzisha maduka hayo mapya mwaka 2017, baada ya kugundua kwamba maduka makubwa kwa wakati huo yalikuwa ya watu kutoka nje ya nchi, na ajira nyingi zilikuwa zinachukuliwa na wageni.

"Baada ya kugundua kwamba maduka makubwa ni ya wageni tuliona fursa tukaanzisha ya kitanzania ambayo kwa muda wa miaka zaidi ya miwili tumetoa ushindani mkubwa kwa kutoa huduma bora na zenye uhakika kwa punguzo la bei," alisema.

Aidha, mkurugenzi huyo alisema kwa sasa wananunua bidhaa kutoka kwa wasambazaji mbalimbali na wazalishaji kutoka nje ya nchi na ndani ya nchi na wanataka kuona faida inayopatikana kwenye biashara yao inawanufaisha Watanzania na kujenga uchumi wa nchi.

"Hivi sasa tumeajiri Watanzania wenzetu zaidi ya miamoja kwenye matawi yetu yote, na tunatarajia kupeleka huduma zetu katika majiji mengine kama ya Mwanza, Mbeya ila tutaanza na Dodoma kwanza," alisema.

# Bawacha sasa yataka mabadiliko sheria ndoa

**Na Mwandishi Wetu**

BARAZA la Wanawake wa Chadema (Bawacha), limesema litaendelea kusemea masuala mbalimbali ya wanawake ikiwamo kuitaka serikali kupeleka muswada wa marekebisho ya sheria ya ndoa kama ambavyo mahakama imeamuru. Akizungumza jijini Dar es Salaam, Mwenyekiti wa Bawacha Taifa, Halima Mdee, alisema Bawacha imekuja na agenda maalum za kusukuma ambazo zitakwenda kuleta mabadiliko makubwa mwa wanawake.

Alisema mwaka huu ni wa uchaguzi na kwamba hakuna mtu wa kuwapangia namna gani bora ya kuzungumza na wananchi, na kwamba wataiandaa wenyewe.

Mdee ambaye ni Mbunge wa Kawe, alisema wananchi wengi wameingia kwenye woga wa kufikiri kwamba kuna Mtanzania mwenye wajibu wa ziada kwa ajili yake, na kwamba wanapaswa kujisemea.

Aidha, Mdee alikumbusha mambo mbalimbali yanayowakabili Watanzania kwa sasa kama kubambikiwa kesi, watu kupotea, watu kushindwa kukosoa na kukosekana kwa demokrasia kwa vyama vya siasa na asasi za kiraia kufanya mikutano mbalimbali.

Aidha, walipinga na kukemea uwepo wa vurugu na matumizi ya silaha za moto wakati wa uchaguzi mkuu, ikiwamo kuonyesha njia.

Kwa mujibu wa Mdee, wanawake wameachwa nyuma kwenye mfumo wa maendeleo na agenda zao hazipewi kipaumbele halisi, na kutaka viongozi wa Bavicha kuwa karibu na waandishi wa habari wanawake kwa ajili ya kuwezesha habari za wanawake kuandikwa kwa wingi.

Alisema dhamira ya Bawacha ni kupigania haki za wanawake na kwamba wengi wanakufa kutokana na matatizo ya uzazi na kujifungua, watoto waliochini ya siku 28, huku bajeti ya eneo hilo ikiwa finyu.

Aidha, alizungumzia Bima ya Afya kuwa wapo Watanzania maskini kabisa hawapati huduma muhimu za afya kutokana na kukosa uwezo wa kulipia kadi hizo na kumudu gharama za matibabu.

Mwenyekiti huyo, alisema zipo sheria ambazo zimekuwa kikwazo kwa maendeleo yake, ikiwamo za kimila zinazomkataza mjane kurithi ardhi ya ukoo.

Alisema mtoto chini ya miaka 15 kuolewa iwapo Mahakama na mzazi ameruhusu jambo ambalo siyo sahihi na kwamba zinatakiwa kufanyiwa marekebisho kama ambavyo uamuzi wa Mahakama Kuu uliopinga umri wa mtoto kuolewa.

"Mahakama Kuu ikishatoa maelekezo ni wajibu wa bunge kutunga sheria ili kutoa katazo. Bawacha tunaitaka serikali kumjali mtoto wa kike kwa kuleta mabadiliko ya sheria ya ndoa, kusoma. Uwepo wa Sheria ya Ndoa kunamdidimiza mtoto wa kike," alisema.

## HABARI KIMATAIFA

# Uganda yawaachia huru raia 9 wa Rwanda

**KAMPALA, Uganda**

UGANDA imewaachilia huru wafungwa tisa raia wa Rwanda ambao walikuwa wanazuiliwa nchini humo kwa mashtaka ya kufanya ujasusi kwa niaba ya serikali ya Rwanda na kumiliki silaha kinyume cha sheria.

Serikali ya Uganda inasema hatua hiyo imechukuliwa ili kurejesha uhusiano mwema na Rwanda, huku juhudi za kidiplomasia zikiendelea kati ya nchi hizo mbili jirani.

Katika hafla ya kuwapokea raia hao tisa kwa balozi wa Rwanda nchini Uganda, Frank Mugambage, Waziri wa Mambo ya Nje wa Uganda, Sam Kutesa amesema kuachiliwa kwa raia hao tisa, sio kwa sababu hawana makosa na kufutilia mbali madai kwamba walikamatwa kiholela inavyodai serikali ya Rwanda.

Kutesa alisema kwamba raia hao wanaweza kukamatwa tena endapo maofisa wa Uganda watahisi wanastahili kuwajibishwa.

Hatua hiyo ni ishara ya nia njema ya kutaka uhusiano mwema kati ya nchi hizi mbili.

Alisema Uganda inamatumaini kwamba Rwanda itafuata njia hiyo katika kurejesha uhusiano mwema kama ilivyokuwa awali.

Miongoni wa walioachiliwa huru na mahakama ya kijeshi ya Makindye, jijini Kampala, ni pamoja na Sagenti Rene Rutagungira, ambaye amekuwa akitajwa sana katika mgogoro wa Rwanda na Uganda, aliyekamatwa kwa madai ya kumkamata na kumrejesha Rwanda aliyekuwa mmoja wa walinzi wa Rais Paul Kagame, Luteni Joel Mutabazi.

Wengine ni Bahati Mugenga, Emma Rwamuco, Augustine Rutisiri, Etiene Nsanzabahizi, Charles Byaruhanga na Claude Iyakaleme.

Watu hao walikuwa wakikabiliwa na mshtaka ya kuifanyia ujasusi Rwanda, kumiliki silaha kinyume cha sheria, na kupanga njama za kuipindua serikali ya Rais Yoweri Museveni.

Serikali ya Rwanda inasema bado kuna idadi kubwa ya raia wake wanaozuiliwa Uganda.

**VOA**

**Kutesa alisema kwamba raia hao wanaweza kukamatwa tena endapo maofisa wa Uganda watahisi wanastahili kuwajibishwa.**

# Uchunguzi wabaini chanzo cha ndege kuanguka Iran

**TERHAN, Iran**

UCHUNGUZI wa awali umebaini kuwa ndege iliyoanguka na kuua abiria wote 176 nchini Iran, ilijaribu kugeuza na kurudi uwanja wa ndege kabla haijapata ajali.

Ndege hiyo aina ya Boeing 737-800 ilianguka muda mfupi baada ya kuanza safari kutoka uwanja wa ndege wa Tehran.

Uchunguzi uliofanywa umebaini kuwa ndege ilikuwa na hitilafu wakati inaanza safari yake, na moto ukaanza kushika.

Awali Iran ilisema kuwa haitakabidhi kisanduku cha kunakili safari ya ndege hiyo ama ''Black box'' kwa kiwanda kilichotengeneza ndege hiyo au kwa Marekani.

Kwa mujibu wa sheria za anga za kimataifa, Iran ina haki ya kufanya uchunguzi kuhusu ajali hiyo.

Lakini watengenezaji wa ndege hiyo kwa ushirikiano na wataalamu kutoka nchi kadhaa wanaweza kuchunguza kisanduku hicho.

Ajali hiyo imetokea wakati ambapo kuna mvutano mkubwa kati ya Marekani na Iran, muda mfupi baada ya Iran kushambulia kwa makombora kambi mbili za kijeshi za Marekani zilizopo Iraq.

Aidha, hakuna ushahidi kuwa matukio haya mawili yanahusiana na kuanguka kwa ndege hiyo.

Kwa kawaida, bodi ya Marekani ya usafirishaji salama ina jukumu la kuchunguza masuala yoyote ya kimataifa yanayohusisha ndege aina ya Boeing iliyotengenezwa Marekani kwa idhini ya sheria za nchi husika.

Kiongozi wa Shirika la Anga Iran, Ali Abedzadeh, alinukuliwa katika vyombo vya habari nchini humo akisema: "Hatutawapa kisanduku cheusi kampuni iliyotengeneza ndege hiyo au Wamarekani, tukio hilo litachunguzwa na shirika la anga la Iran, lakini Ukraine itaruhusiwa kushiriki katika uchunguzi huo."

Abedzadeh alisema kwamba hana uhakika ni nchi gani zitaweza kufanya uchunguzi wa kisanduku hicho cheusi kinachotunza sauti zilizonaswa katika ndege.

Shirika la Boeing lilisema kuwa liko tayari kusaidia kwa namna yeyote itakayohitajika.

Wakati huohuo, Waziri Mkuu wa Canada, Justin Trudeau, alisema kuwa alitarajia nchi yake ina wajibu wa kufanya uchunguzi kuhusu ajali hiyo na iko tayari kutoa msaada wowote wa kiufundi.

***BBC***




Wanajeshi wa Marekani wakielekea Iraq. **PICHA: ALLIANCE**

# Mtoto akutwa kwenye tairi la ndege amefariki

**PARIS, Ufaransa**

MWILI wa kijana mdogo uligunduliwa umekufa ukiwa kwenye sehemu ya gurudumu la ndege ya Boeing 777 ya Shirika la Ndege la Air France iliyokuwa ikitokea Abidjan, Ivory Coast kwenye uwanja wa ndege wa Roissy, nchini Ufaransa.

Shirika la Ndege la Air Ufaransa limethibitisha kifo cha mtoto huyo aliyekuwa anaingizwa nchini humo kwa njia haramu.

Mwili wa mtoto huyo ulipatikana juzi katika sehemu ya gurudumu la ndege yenye chapa AS703, iliyowasili kwenye uwanja wa ndege wa Roissy-Charles de Gaulle, karibu na mji wa Paris, ikitokea Abidjan.

Waziri wa Mawasiliano wa Ivory Coast, Sidy Touré, alisema kuwa kijana huyo alikuwa na umri kati ya miaka 15 na 17 na kueleza kuwa uchunguzi bado unaendelea.

Alisema serikali itafuatilia kwa karibu suala hilo na kwamba Tume ya Uchunguzi kwa sasa inakutana chini ya usimamizi wa mamlaka ya uwanja wa ndege ili kujua namna kijana huyu aliweza kupatikana akiwa amefariki katika sehemu hiyo hatari.

Nchini Ufaransa nako uchunguzi umeanzishwa na unaendeshwa na polisi wa usafiri wa anga kwenye uwanja wa ndege wa Charles de Gaulle.

Vipimo vya mwili wa kijana huyo vilitakiwa kufanyika jana Jumatano. Wengi wanaamini kwamba kijana huyo alikufa kutokana na kukosa hewa au baridi.

***RFI***

# Bunge lapiga kura kumdhibiti Trump

**WASHINGTON, Marekani**

BARAZA la Wawakilishi la Bunge la Marekani, jana, lilipiga kura ya kudhibiti uwezo wa Rais Donald Trump kuchukua hatua za kijeshi dhidi ya Iran.

Hatua hiyo ilifanyika wakati shutuma za Wademocrat dhidi ya mashambulizi ya Marekani yaliyomuua jenerali wa ngazi ya juu ya Iran zikiendelea.

Spika wa Baraza hilo, Nancy Pelosi, alitangaza kura hiyo katika taarifa ambayo inasema shambulio la wiki iliyopita la ndege isiyo na rubani ambalo lilimuua Jenerali Qassem Soleimani ni la uchokozi na limevuka mipaka.

Azimio la chama cha Democratic la madaraka ya vita linaonekana litapitishwa dhidi ya upinzani mkali wa chama cha Republican.

Pendekezo kama hilo la Seneta, Tim Kaine wa chama cha Democratic, linakabiliwa na mapambano makali katika Baraza la Seneti kutoka kwa maseneta wa Chama cha Republican.

Kutokana na mzozo wa kiutendaji baina ya vyama hivyo viwili, haijafahamika bado iwapo kura hiyo itakuwa hatua kuelekea kumzuwia Rais Trump kuhusu Iran ama itakuwa ni ishara tu ya upinzani wa Wademocrat.

***DW***

## 366 wasiostahili wapeleka tamko la mali na madeni

**Na Renatha Msungu, DODOMA**

SEKRETARIETI ya Maadili ya Viongozi wa Umma imesema imebaini matamko 366 ya mali na madeni, yaliyowasilishwa kwake na watu ambao siyo viongozi, hivyo hawapaswi kuwasilisha matamko hayo.

Akizungumza na waandishi wa habari jijini hapa jana, Kamishna wa Maadili, Jaji mstaafu Harlod Nsekela, alisema mawaziri na manaibu wao, makatibu wakuu, viongozi wa vyombo vya dola, majaji na wakuu wa mikoa wote wamepeleka matamko yao isipokuwa Naibu Katibu mkuu mmoja ambaye hajawasilisha tamko lake kutokana na sababu zake ambazo hakuzitaja.

"Hata mimi, Kamishna wa Maadili ya Sekretalieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma, nimewasilisha tamko langu la rasilimali na madeni ila mimi nawasilisha moja kwa moja kwa Rais, msije kuniuliza kuwa mimi nawasilisha wapi," alisema.

"Sisi tunashughulikia viongozi, kwa hiyo ukiniletea tamko wewe ambaye siyo kiongozi, ni kukiuka kifungu cha 9(c) cha sheria ambacho kinamtaka kila kiongozi ifikapo mwisho wa mwaka, anatakiwa kuwasilisha matamko yake," alisema.

Alikiri kuwa ofisi yake imekuwa ikipokea matamko mengi ambayo hayatakiwi kupelekwa kwao, hivyo kuwataka watu kusoma vizuri sheria.

"Sisi kazi yetu siyo kupokea tu hayo matamko, bali lazima tuyaangalie kama yamejazwa vizuri, na kama yana makosa, basi tunamrudishia ili kurekebisha.

"Kwa hiyo, haya matamko 366 tuliyoyapata ambayo siyo ya viongozi, hatuwezi kuyaweka kwenye hesabu zetu, na matamko ya watu ambao siyo viongozi hatuyataki," alisema.

Alisema kwa viongozi ambao hawakuwasilisha matamko yao katika tarehe ya mwisho ya mwaka jana, wanapaswa kuyapeleka lakini lazima wawe na barua inayoonyesha sababu za msingi za kuchelewesha kupeleka matamko yao.

Hata hivyo, kiongozi huyo alikiri umbali wa ofisi yao, umechangia watu wengi kushindwa kuwasilisha matamko yao kwa wakati, lakini akaweka wazi kuwa licha ya kikwazo hicho, uwasilishaji wa matamko ya mali na madeni kwa viongozi wa umma kwa ngazi ya kuu umekuwa wa kuridhisha.

**"Kwa hiyo, haya matamko 366 tuliyoyapata ambayo siyo ya viongozi, hatuwezi kuyaweka kwenye hesabu zetu, na matamko ya watu ambao siyo viongozi hatuyataki," alisema.**

# Ndege wateketeza mahindi, alizeti, mtama ekari 69,264

**Na Jumbe Ismailly, IKUNGI**

NDEGE waharibifu wa mazao aina ya 'love birds', wameshambulia mahindi, uwele, mtama na alizeti katika vijiji vya Mlandala, Mduguyu na Kaugeri, wilayani Ikungi mkoani Singida.

Imeelezwa kuwa imekuwa vigumu kumteketeza ndege huyo kutokana na kuwa ni nyara ya serikali.

Akizungumza na Nipashe, Ofisa Kilimo wa Halmashauri ya Ikungi, Senkoro Mjema, alisema uteketezaji wa ndege huyo ni hadi kibali maalum, na kwamba uharibifu anaofanya ni mkubwa kuliko ndege aina ya kweleakwelea.

Ndege hao waharibifu wanaotambulika kwa jina jingine la silingwa wameharibu jumla ya ekari 69,264 za mazao aina ya mahindi na alizeti katika msimu wa kilimo cha mwaka 2018/2019.

"Ndege huyu huweka makazi chini ya matawi ya mipama na yupo chini ya Wizara ya Maliasili na Utalii kama tunu ya Taifa, kumteketeza kwake hadi upate kibali maalum," alifafanua Mjema.

Aidha, kutokana na hali hiyo upo uwezekano mkubwa wananchi kukosa chakula na uchumi wao kuyumba tofauti na miaka mingine.

Akimkaribisha Mkuu wa Wilaya ya Ikungi kuzungumza na wakulima wa pamba, Diwani wa Kata ya Mwaru, Iddi Makangale, alisema uteketezaji wa ndege huyo imekuwa ngumu huku wakulima wakipata hasara.

"Lakini wakulima hawa leo hawalimi zao la alizeti kwa sababu ya huyu ndege, kwa sasa anakula mahindi na anatupa hasara kubwa sana katika kijiji cha Mlandala," alisema na kuongeza:

"Tunaomba Mkuu wa Wilaya uiombe serikali ili ndege huyu aweze kuangamizwa ili wana Mlandala nao waweze kufaidi matunda ya alizeti."

Alisema wakulima wa eneo hilo hulima mahindi, mtama pamoja na mpunga, lakini kwa kiasi kikubwa mbuga hiyo hustawisha zaidi mahindi, isipokuwa kikwazo kikubwa cha kilimo cha mazao hayo ni ndege waharibifu wa mazao aina ya silingwa na ndege huyo ni kero kubwa.

Kuhusu kilimo cha pamba, diwani huyo alimuomba mkuu wa wilaya hiyo kuishawishi kampuni inayonunua pamba iweze kuangalia uwezekano wa kujenga maghala yasiyopungua mawili ya kuhifadhia pamba.

"Ni kwamba pamba hii tunayoihamasisha leo, lakini hatuna maghala ya kuhifadhia pamba kwa hiyo nikuombe, kampuni hii ambayo kama kuna uwezekanao iweze kujenga hata maghala mawili ikiwezekana," alifafanua.

Meneja uzalishaji wa kampuni ya Biosustain, Paul Deogratius licha ya kulikubali ombi la kupeleka mbegu za pamba haraka iwezekanavyo, kampuni hiyo ina uwezo wa kuchambua kilo milioni 20 za pamba kwa mwaka, lakini tangu kiwanda hicho kilipoanza uzalishaji mkoani Singida mpaka sasa kinazalisha kilo milioni sita kwa mwaka.

Alisema kiwango cha uzalishaji kimepanda kutoka kilo milioni 2 kwa mwaka juzi hadi kufikia kilo milioni 6 mwaka huu, na kwamba kwa wilaya ya Ikungi uzalishaji wa zao la pamba umeongezeka kutoka kilo 800,000 zilizozalishwa mwaka juzi hadi kufikia zaidi ya kilo milioni moja mwaka huu.

Akizungumza kuhusu masuala hayo, Mkuu wa Wilaya ya Ikungi, Edward Mpogoro, aliahidi kutoa taarifa hizo kwa Wizara ya Maliasili na Utalii na Wizara ya Kilimo ili wataalamu waweze kupelekwa kushughulikia suala hilo.



# TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## VIWANJA /MASHAMBA

**Viwanja vinauzwa** Kibaha Misugusugu. Ukubwa ni mita 20 kwa 20 (400m2). Bei ni 2,000,000/- Milioni mbili tuu. (5,000/=1m2). Unaweza kulipa kwa awamu ndani ya miezi mine. Huduma zote zipo. Kwa mawasiliano: 0714 090009 / 0767 090008. Vimepimwa.

## MATANGAZO MCHANGANYIKO

**MKOPO WA HARAKA KUTOKA ENTERPRISE FINANCE LIMITD (EFL).** Kwa mahitaji kama kulipa ada ya shule, kodi, kuboresha biashara, kumalizia tenda etc. Kwa maelezo zaidi piga 0758 112 332. Karibu EFL.


NIPASHE NI JIBU LAKO

NJOO UTANGAZE NASI BIDHAA YAKO KWA BEI NAFUU SANA

Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz, au piga simu: 0782253676


## KUPOTEA KWA CHETI



**LAMECK MICHAEL** amepotelewa na cheti cha elimu ya kidato cha nne alichosomea ktk shule ya secondari PUGU, Chenye index namba S.0147/0148 na alimaliza mwaka 2007 na chenye rb namba MOR/RB/6248/2018.

115570302

## KUPOTEA KWA CHETI



**JEROME M KUNDI** anatangaza kupotelewa kwa cheti cha Kidato cha nne Shule ya Sekondari Namfua chenye index No S0401-0061 kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa 2011.

Yeyote atakaye kiona atoe taarifa kituo cha polisi.

Taarifa polisi: KIL/MOS/RB/545861/19.

115578802

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**

**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA)**
**YA 5 KANUNI YA 2**

**Katika mahakama ya mwanzo: MJINI MOROGORO**

**Usimamizi wa mirathi No;7/2020**

**Ombi la GEORGE PAULO MSEGEYA Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu PETER PAUL MSEGEYA.**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 24/01/2020 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Wosia ya marehemu huyo upo Mahakamani waweza kukaguliwa tarehe 09/01/2020.

Sahihi ya Hakimu

HAKIMU
MAHAKAMA YA MWANZO MJINI
MOROGORO

115579502

## KADI YA GARI IMEPOTEA

**ALLEN TANAMADUNDA LUPEMBE** Anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T 597 DCP,** Aina yake TOWNACE Yenye chasis namba : **KM510058158.** Yeyote atakaeiona anaombwa atoe taarifa kituo cha polisi.

Taarifa ya Polisi: **MOR/MOR/RB/21662/2020.**

115579402

## KUPOTELEWA NA KADI YA PIKIPIKI

**CEDRICK DEUSDEUT MBUNDA** anatangaza kupotelewa na kadi ya Pikipiki yenye namba za usajili MC 124 ABB.

Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi.

Taarifa ya Polisi: DAR/CEN/RB/2716/2020.

## CHETI KIMEPOTEA



**ANNE YUSUPH MARIAM** anatangaza kupotelewa na cheti cha **PROFICIENCY EXAMINATION FOR HUMAN RESOURCE OFFICERS** chenye Registration number PHR-DEC-16-96 kilichotolewa na TANZANIA PUBLIC SERVICE COLLEGE mwaka 2016.

Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi.

Taarifa ya polisi: DAR/TAB/RB/503720/2019.

115578802

PROBATE AND ADMINISTRATION
IN THE DISTRICT COURT (DISTRICT DELEGATE) OF ILEMELA DISTRICT
AT MWANZA
PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO 3/2019
In the matter of the Estate of the late PRISCA WILLIAM OBURE
And
In the matter of Application for Grant of letters of Administration by
ALPHONCE NYITATI MAGUBO

**GENERAL CITATION**
**(RULE 75)**

All persons claiming to have any interest in the estate of the above Named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they to think fit before the grant for letters of probate and Administration is made to the above named petitioner.

Caveat/objection to the grant should be filed on or before 31 day of January 2020 of the publication of this citation in the Gazette.

Dated at mwanza this 12th day of December, 2019.

DISTRICT RESIDENT MAGISTRATE
ILEMELA- MWANZA.

115580102

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
MAHAKAMA
USIMAMIZI WA MIRATHI FORM II
(S.M.M. 1984 NYONGEZA YA 5 KANUNI 2)
Katika Mahakama ya mwanzo MJINI -TANGA
Usimamizi wa Mirathi NAMBA 3/2020
Ombi la SALIM MBEGA LUWHUCHU
kuteuliwa
Msimamizi wa mirathi marehemu
MWANSITI SALIM MBEGA

Kwa YEYOTE ANAYEHUSIKA

Watu wote wanaodaiwa kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu huyo wanaalikwa kuja na kuhudhuria kesi wakitaka mnamo tarehe 29/1/2020 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Wosia wa marehemu huyo upo Mahakamani waweza kukaguliwa. Tarehe 08/01/2020

115579302

## KUPOTELEWA KWA KADI YA PIKIPIKI

**Musa Kasimu Selemani** anatangaza KUPOTELEWA na kadi ya PIKIPIKI yenye namba za usajili MC 897 BZU. Chesis no. LDAPAJOBIJGBO1468, Egine no. 18F01468.

Yeyote ataeona atoe taarifa kituo Cha polisi.

DOD/DOD/RB/522874/2019.

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**THE TAN CONSULT LIMITED** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba ya usajili T728 ADJ Toyota Landcruicer. Yenye Chassis No HD 1610050883. Engine No. 1HDC095899.

Yoyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi.

Taarifa ya polisi ARU/ARU/RB/24377/2020.

## WILD EXISTANCE SAFARIS LIMITED

## (UNDER VOLUNTARY LIQUIDATION)

**NOTICE IS HEREBY GIVEN to all CREDITORS and DEBTORS of WILD EXISTANCE SAFARIS LIMITED and the GENERAL PUBLIC that WILD EXISTANCE SAFARIS LIMITED** is undergoing Voluntary Liquidation under the appointed liquidator **MR CYPRIAN HERBERT MWAIMU (ADVOCATE).**

All debtors of the company and all persons holding in their possession any asset/properties of the company to pay their debts to the liquidator at the address below not later than **12:00 noon 14th** day of February 2020 and to surrender the assets and the said properties to the liquidator at the address below not later than **12:00 noon 14th day of February, 2020.**

All creditors of the company are hereby given notice that they should submit their claims with supporting documents to the liquidator at the address below not later than **12:00 noon 14th day of February, 2020 without fail.**

**CYPRIAN HERBERT MWAIMU**
**(ADVOCATE)**
**THE LIQUIDATOR**

**Sikh Union Road, Plot No.7 & 8**
**P. O. Box 1203, Arusha-Tanzania**
**Telephone/Facsimile: +255 752 393 464**
**Cellular: +255 715 393 464**
**Electronic mail: cyprian@nextlevel.co.tz**

215580202


Kwa Habari Motomoto usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku

NJOO UTANGAZE BIDHAA YAKO KWA BEI NAFUU SANA

OFISI ZA MATANGAZO
MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,
PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.
E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

HABARI MICHEZO



# RASHFORD

## ANATARAJIA UNITED KUPINDUA MEZA

**MANCHESTER, England**

MARCUS Rashford ameitaka Manchester United kuwa na morali kama 'walivyopindua meza' kwenye Ligi ya Mabingwa msimu uliopita jijini Paris wakati wakitakiwa kubadilisha matokeo dhidi ya wapinzani wao wa jiji moja, Manchester City.

United ilifungwa mabao 3-1 kwenye mchezo wa kwanza wa nusu fainali ya Kombe la EFL pale katika dimba la Old Trafford, Jumanne, wakiachwa na mlima mkubwa wa kupanda kuelekea kwenye mchezo wa pili.

Msimu uliopita kikosi hicho cha kocha, Ole Gunnar Solskjaer kilipindua matokeo dhidi ya Paris Saint-Germain baada ya kufungwa 2-0 nyumbani na wakaweza kutinga hatua ya mtoano wa timu 16.

Kwa kile kilichotokea Paris, Rashford anaona kwamba wanaweza kufanya hivyo hivyo dhidi ya City kwenye mchezo wa pili licha ya kuwa nyuma kwa mabao 3-1.

Na Rashford, ambaye kwenye mchezo huo alifunga bao la kufutia machozi akiwa amevaa kitambaa cha unahodha dhidi ya kikosi hicho cha kocha, Pep Guardiola, anawataka United kuwa na hamasa kubwa wakati watakaposafiri kwenda kule kwenye uwanja wa Etihad.

"Ni mchezo tofauti na wachezaji tofauti, lakini tunaweza kufanya kile tulichokifanya kule Paris tunatakiwa kuwa na hamasa kubwa tena," alisema akiiambia tovuti ya klabu ya United.

"Tunatakiwa kwenda pale, kufunga mabao na kushinda mchezo. Naamini tuna uwezo huo. Tulichokifanya kule Paris kinaweza kutoka pale uwanja wa Etihad, naamini hakuna litakaloshindikana."

## MBAPPE ATIA NENO KUHUSU KUONGEZA MKATABA PSG

**PARIS, Ufaransa**

KYLIAN Mbappe ametia neno kuhusu makubaliano ya kusaini mkataba mpya na Paris Saint-Germain, akisisitiza "huu sio wakati sahihi wa kuzungumzia hilo".

Mbappe amekuwa akihusishwa na mpango wa kutua kwa miamba wa Ligi Kuu Hispania, LaLiga, Real Madrid, ambapo kocha wake ambaye ni Mfaransa mwenzake, Zinedine Zidane hajaficha siri kwamba anavutiwa na mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 21.

Mkurugenzi wa michezo wa PSG, Leonardo awali alibainisha kwamba mazungumzo kuhusu mkataba mpya yanaendelea, huku mkataba wa sasa wa Mbappe ukiwa unamalizika mwishoni mwa msimu wa 2021-22.

Alipoulizwa kuhusu majaliwa yake hapo PSG bada ya ushindi wa 6-1 kwenye robo fainali ya Kombe la Coupe de la Ligue dhidi ya Saint-Etienne juzi Jumatano, Mbappe aliwaambia waandishi wa habari: "Nipo tayari kucheza soka kwanza. Kwa sababu tupo Januari sasa.

"Tumeanza kipindi cha pili cha msimu, ambako tunaweza kushindania mataji. Nafikiri sio wakati sahihi kuzungumzia hili.

"Klabu imetulia, kila mmoja anakwenda kwenye njia moja na kufikiria kuhusu kile kitakachotokea uwanjani kiwe kizuri zaidi."

Mbappe alifunga kwenye mchezo huo dhidi ya Saint-Etienne wakati PSG ikifuzu nusu fainali ya michuano hiyo.



## YOUNG ATARAJIA KUTUA MILAN

**MANCHESTER, England**

NAHODHA wa Manchester United, Ashley Young, atajiunga na Inter Milan baada ya mkataba wake na klabu hiyo utakapomalizika mwishoni mwa msimu huu.

Nyota huyo mwenye umri wa miaka 34 alitaka kuondoka katika kipindi cha dirisha dogo la usajili la Januari kinachoendelea, lakini kwa sasa United haikuwa tayari kumwachia aondoke.

Young, ambaye aichezea klabu hiyo mechi 261, Jumanne wiki hii aliachwa katika kikosi cha United kilichopambana na Manchester City katika mechi ya Kombe la Ligi ambayo ilimalizika kwa kuchapwa mabao 3-1.

Kutokana na mkataba wa Young kumalizika mwishoni mwa msimu huu, nyota huyo anaruhusiwa kufanya mazungumzo na klabu zinazoonyesha nia ya kumhitaji zilizoko nje ya England.

Kocha wa United, Ole Gunnar Solskjaer alisema baada ya mechi hiyo dhidi ya City kwamba "Huu si wakati mzuri" kuzungumza hatima ya Young, aliongeza: "Hatuwezi kujidhoofisha wenyewe; tunatakia kujiimarisha wenyewe, kama kutakuwa na mchakato wowote unatarajiwa kufanyika."

Young alijiunga na United akitokea Aston Villa mwaka 2011 na amekuwa kwenye kikosi cha timu hiyo ambacho kilishinda mataji ya Ligi Kuu England, Kombe la FA na Kombe la Ligi.






# VALVERDE
## HAFIKIRII KUMWACHIA VIDAL

**JEDDAH, Saudi Arabia**

KOCHA wa Barcelona, Ernesto Valverde amesema hafikirii kuhusu Arturo Vidal kuondoka kwa mabingwa hao wa Ligi Kuu Hispania, LaLiga, huku kukiwa na ripoti ya kutakiwa na Inter Milan na Manchester United.

Vidal amekosa namba ya kudumu kwenye kikosi hicho tangu kuwasili kwa Frenkie de Jong kutoka Ajax, hivyo kusababisha majaliwa yake kutojulikana hapo katika dimba la Camp Nou, ambapo ameanza mechi nne tu za LaLiga msimu huu.

Vidal mwenye umri wa miaka 32 amekuwa akihusishwa kujiunga na kocha wake wa zamani pale Juventus, Antonio Conte kwa miamba wa Ligi Kuu Italia, Serie A, Inter Milan, huku pia vigogo wa Ligi Kuu England, United wakiripotiwa kumwinda.

Valverde ameelezea uvumi huo jana Alhamisi kabla ya mchezo wake wa nusu fainali ya Kombe la Supercopa de Espana dhidi ya Atletico Madrid mjini Jeddah nchini Saudi Arabia.

"Hatufikii kuhusu kumwacha aende timu nyingine," alisema Valverde akiwaambia waandishi wa habari. "Leo (jana) atakuwa na sisi. Hakuna cha zaidi."

Kuhusu kutakiwa na klabu za England na Italia, Valverde alijibu: "Arturo Vidal anacheza katika klabu yetu na leo (jana) atakuwa na sisi uwanjani au benchi.

"Hatusikilizi kuhusu uvumi kutoka klabu nyingine kuwa zinamhitaji mchezaji wetu, kwa sasa yeye ni mchezaji wetu."

Vidal aliondoka kwa mabingwa wa Ligi Kuu Ujerumani, Bundesliga, Bayern Munich na kujiunga pale Barcelona mwaka 2018 na raia huyo wa Chile ameshinda mataji mawili, LaLiga na Supercopa de Espana.

# Zidane akunwa kiwango cha Madrid kwa Valencia

**JEDDAH, Saudi Arabia**

KOCHA wa Real Madrid, Zinedine Zidane aliridhishwa na kiwango cha kikosi chake wakati kikiibuka na ushindi wa 3-1 kwenye mchezo wa Kombe la Supercopa de Espana dhidi ya Valencia, juzi Jumatano.

Mabao kutoka kwa Toni Kroos, Isco na Luka Modric yalikiwezesha kikosi hicho cha Madrid kupata ushindi huo mjini Jeddah nchini Saudi Arabia, huku Dani Parejo akifunga bao kwa mkwaju wa penalti kuipa bao la kufutia machozi Valencia.

Huku Karim Benzema na Gareth Bale wakikosekana kutokana na majeruhi pamoja na Lucas Vazquez na Marco Asensio, Zidane aliichezea timu yake bila winga na kuwatumia Isco na Modric kwenye kiungo iliyokuwa na wachezaji watano, mfumo huo ulisaidia, huku Luka Jovic akicheza mbele ya Kroos, Casemiro na Federico Valverde.

Zidane amebainisha kwamba mbinu hiyo inaweza kutumika tena msimu huu kwa kuwaruhusu mabeki wa pembeni kupanda zaidi kwa ajili ya kusaidia mashambulizi.

Akizungumza na waandishi wa habari baada ya mchezo huo, Zidane alisema: "Akili yetu tuliiweka kwenye kuhakikisha tunashinda mchezo na tulistahili ushindi huu.

"Tulicheza vizuri. Wachezaji walielewa, kwa uhakika tulifanya vizuri. Tulikuwa na kila ubora kwenye mchezo huu. Na ndio maana tukawafunga kirahisi Valencia.




# PSG haikudhani Icardi atang'ara

**PARIS, Ufaransa**

MAURO Icardi amevuka matarajio ya Paris Saint-Germain baada ya juzi kufunga mabao matatu 'hat-trick' kwenye mchezo wa Kombe la Coupe de la Ligue, kwa mujibu wa mchezaji mwenzake, Marco Verratti.

Mabao hayo matatu ya Icardi yaliwawezesha mabingwa hao wa Ufaransa kuibuka na ushindi wa mabao 6-1 dhidi ya Saint-Etienne waliomaliza wakiwa na wachezaji 10 uwanjani, na kutinga nusu fainali, juzi Jumatano.

Mshambuliaji huyo wa kimataifa wa Argentina amekuwa na kiwango cha kuvutia tangu alipotua hapo akitokea Inter Milan kwa mkopo mwanzoni mwa msimu huu, na amefunga mabao 17 katika mashindano yote.

Kiungo wa PSG, Verratti amemsifia Icardi - ambaye amekuwa akihusishwa na kutakiwa Juventus, Napoli na Real Madrid kuwa amevuka matarajio ya kikosi hicho cha kocha, Thomas Tuchel.

"Mauro? Anaweza asiguse mpira, lakini anajua mpira utamfuata tu na atafunga, mara zote yupo tayari," alisema Verratti akiiambia Canal +.

"Hii ndio sifa kubwa ya Mauro. Hatukufukiria kwamba atakuwa vizuri namna hii, mwezi wa kwanza mara zote unakuwa mgumu, lakini kwake ilikuwa tofauti na tuna matumaini ataendelea kuwa kwenye kiwango hiki."

Icardi amekuwa kwenye kiwango cha kuvutia hapo kwenye jiji la Paris, akifunga mabao tisa kwenye Ligi Kuu Ufaransa, Ligue 1, wakati PSG ikiwa kileleni ikiongoza kwa tofauti ya pointi saba zaidi.

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# FERNANDINHO KUPATA MKATABA MPYA CITY

●●●Lakini Guardiola ameweka wazi kwamba anahitaji pia kuimarisha safu yake ya ulinzi...

**MANCHESTER, England**

FERNANDINHO anakaribia kusaini mkataba mpya na Manchester City, mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 34 amebainisha.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Brazil, ambaye alijiunga na mabingwa hao wa Ligi Kuu ya England akitokea Shakhtar Donetsk mwaka 2013, mkataba wake wa sasa unamalizika mwishoni mwa msimu huu.

Kocha wa Man City, Pep Guardiola amezungumzia kuhusu mpango wake wa kumbakiza Fernandinho hapo kwenye dimba la Etihad na sasa mambo yanaelekea vizuri.

"Wakati nilipoongeza mkataba wangu mwaka 2018, tuliweka makubaliano kama nitafikia malengo fulani, mkataba wangu utaongezwa," alisema mchezaji huyo akiiambia ESPN Brasil.

"Majadiliano tayari yameanza, tulizungumza mwezi uliopita. Nakaribia kufikia malengo yangu na kuongeza mkataba, lakini tutathibitisha baada ya kusaini."

Huku City ikiwa kwenye matatizo ya safu yake ya ulinzi msimu huu, Fernandinho mara kwa mara amekuwa akitumika kama beki wa kati, nafasi ambayo anaifurahia kucheza.

"Ni nzuri hasa kama inakufanya uwe bora na kuwa daraja la juu," alisema. "Kucheza kwenye nafasi tofauti kunafungua milango zaidi ya kujifunza.

"Kwenye ulinzi, naona mchezo tofauti. Imekuwa tofauti na ushirikiano ninaoupata kutoka kwa Pep ni mzuri zaidi.

"Katika umri wa miaka 34, kucheza kwenye Ligi Kuu ya England ni chanzo cha ufahari. Wachezaji wengi tu wangependa kupata uzoefu kama huu ninaoupata kwa sasa."

Fernandinho alicheza kwa dakika zote wakati City ikiifunga Manchester City mabao 3-1 kwenye mchezo wa kwanza wa nusu fainali ya kombe la EFL, Jumanne na anatarajia kuwa kwenye kikosi wakati watakapocheza na Aston Villa kwenye mchezo wa Ligi Kuu, Jumapili.

## KWA UFUPI

**ARSENAL, UNITED VITANI**

ARSENAL na Manchester United zimewasilisha rasmi ofa ya kumwania straika wa Paris St-Germain na Timu ya Taifa ya Uruguay, Edinson Cavani, ambaye ana umri wa miaka 32. ***(El Chiringuito - via Metro)***

**DIOP ANUKIA CHELSEA**

CHELSEA imemtaja beki wa West Ham, Issa Diop, ambaye ana umri wa miaka 22 kuwa mchezaji namba moja wanayemhitaji katika kikosi chao. The Blues wako tayari kutoa dau la pauni milioni 40 ili kumsajili Mfaransa huyo. ***(Express)***

**AKE AKARIBIA CHELSEA**

CHELSEA inajiandaa kutoa ada ya pauni milioni 40 ili kumsajili beki wa kati wa Bournemouth na Timu ya Taifa ya Uholanzi, Nathan Ake (24), kama itafanikiwa kuachama na beki raia wa Denmark, Andreas Christensen. ***(Sun)***

**UMTITI AGOMBEWA ENGLAND**

TOTTENHAM, Arsenal na Manchester United zinapambana kuwania saini ya beki wa kati, Samuel Umtiti (26), kutoka Barcelona ambayo inajiandaa kumuuza nyota huyo wa Timu ya Taifa ya Ufaransa. ***(El Desmarque - in Spanish)***

**ALLEGRI AISUBIRI UNITED**

KOCHA wa zamani wa Juventus, Massimiliano Allegri, atachelewa kurejea katika kazi yake ya kufundisha kutokana na kusubiri kuchukua mikoba ya Ole Gunnar Solskjaer kwenye kikosi cha Manchester United. ***(Mail)***

**LIGT KUREJEA AJAX**

AJAX inajiandaa kumrejesha kwa mkopo Matthijs de Ligt licha ya beki huyo wa Timu ya Taifa ya Uholanzi mwenye umri wa miaka 20 kuondoka klabuni hapo na kujiunga na Juventus katika kipindi cha majira ya joto mwaka jana. ***(A Bola - in Portuguese)***

**CITY KUSAJILI WANNE**

MANCHESTER City inajipanga kusajili wachezaji wapya kati ya wanne na sita mwaka huu, lakini ikitaja nafasi ya beki wa kati na beki wa kushoto ni muhimu katika kuimarisha kikosi cha Pep Guardiola. (Telegraph)

**DEMBELE ANUKIA CHELSEA**

STRAIKA wa Lyon na Timu ya Taifa ya Ufaransa, Moussa Dembele (23), alikuwa akiangaliwa na mawakala wa Chelsea na Manchester United katika mechi ambayo alifunga bao kwenye ushindi wa 3-1 dhidi ya Stade Brest katika mchezo wa Kombe la Ligi uliochezwa Jumatano. ***(Mail)***

**PALACE YAIBANIA BAYERN**

MABOSI wa Crystal Palace wamekataa kupokea ofa ya mabingwa wa Ligi Kuu Ujerumani, Bayern Munich ambao wanataka kumsajili mshambuliaji wake Wilifried Zaha. ***(Guardian)***

**PIATEK ANUKIA SPURS**

TOTTENHAM imejiunga kwenye vita ya kuwania saini ya straika wa AC Milan na Timu ya Taifa ya Poland, Krzysztof Piatek (24), ambaye klabu yake hiyo ya Italia inamuuza kwa dau la pauni milioni 30. ***(Guardian)***

**WANYAMA MBIONI KUUZWA**

MABOSI wa Spurs wanajiandaa kusajili kiungo mpya kama watafanikiwa kumuuza Mkenya Victor Wanyama (28), na kiungo wa Timu ya Taifa ya Denmark, Christian Eriksen, ambaye ana umri wa miaka 27. ***(Evening Standard)***

**MILIK ANUKIA UNITED**

STRAIKA wa Napoli na Timu ya Taifa ya Poland, Arkadiusz Milik, ambaye ana umri wa miaka 25, ametajwa kuwindwa na Manchester United. ***(Sun)***

HABARI MICHEZO

# MGUNDA AFUNGUKA SIRI YA USHINDI MFULULIZO COASTAL

**Na Somoe Ng'itu**

KOCHA Mkuu wa Coastal Union, Juma Mgunda, amesema kuwa ushirikiano na 'sapoti' wanayopata kutoka kwa mashabiki wa timu hiyo ya jijini Tanga, ni moja ya sababu ya kikosi chake kufanya vizuri kwenye mechi za nyumbani za Ligi Kuu Tanzania Bara.

Coastal Union ilipata ushindi wa bao 1-0 dhidi ya Kagera Sugar, bao pekee katika mchezo huo likipachikwa kimyani na mshambuliaji, Ayoub Lyanga dakika ya 76.

Matokeo hayo yameifanya mabingwa hao wa Ligi Kuu Tanzania Bara mwaka 1988 wafikishe pointi 29 na kupaa hadi katika nafasi ya pili kwenye msimamo wa ligi hiyo baada ya kushuka dimbani mara 16.

Mgunda, alisema kuwa juhudi za wachezaji kupambana na kutowadharau wapinzani wao, kumewasaidia kupata ushindi katika mechi nyingine na nyingine tano zilizopita.

"Kubwa zaidi ni kuwashukuru wapenzi na wanachama wa Coastal Union wa Mkoa wa Tanga kwa jinsi wanavyowasapoti vijana wangu, wamekuwa chachu kubwa ya sisi kupata matokeo," alisema Mgunda.

Naye Kocha Mkuu wa Kagera Sugar, Mecky Maxime, alisema timu yake haikutumia vema nafasi walizotengeneza katika mchezo huo ambao ulimalizika kwa wao kupata kichapo.

Maxime alisema bado hawajakata tamaa, wataendelea kurekebisha makosa yao katika mechi zinazofuata za ligi hiyo.

"Kipindi cha kwanza ndio tulipata nafasi nyingi, tukazichezea, lakini wenzetu wakapata nafasi, tena sio nafasi, tukazembea, ila keshokutwa tuna mchezo mwingine, tutapambana kusaka ushindi," Maxime alisema.

Coastal Union imeshinda mechi sita mfululizo na ilianza kutoa kichapo kwa Namungo, Ndanda, Mbeya City, Tanzania Prisons, Azam FC na Kagera Sugar hapo juzi.




Meneja wa NMB tawi la Zanzibar, Abdallah Duchi (kushoto), akimkabidhi vifaa vya michezo Salim Ali Jazira kwa ajili ya timu ya Baraza la Wawakilishi Zanzibar, kwa ajili ya kusherehekea Miaka 56 ya Mapinduzi ya Zanzibar. Vifaa hivyo ni jezi na mipira kwa timu za mpira wa miguu na kikapu vyote vikiwa na thamani ya Sh. milioni 6.5. Hafla ya makabidhiano ilifanyika kwenye ukumbi mdogo wa Baraza la Wawakilishi Chukwani Zanzibar jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Azam yanasa 'Jembe' la Mlandege

**Na Mwandishi Wetu, ZANZIBAR**

ZIKIWA zimebaki siku tano kabla ya dirisha dogo la usajili kufungwa hapo Januari 15, mwaka huu, Klabu ya Azam, imefanikiwa kuinasa saini ya kiungo mshambuliaji wa Mlandege ya Zanzibar, Khleffin Hamdoun.

Azam ilimtangaza kiungo huyo juzi usiku visiwani hapa baada ya kusaini mkataba wa miaka minne wa kuwatumikia mabingwa watetezi hao wa Kombe la Mapinduzi.

Hamdoun alionyesha kiwango cha hali ya juu wakati Azam ikishinda 1-0 dhidi ya Mlandege na kwa mujibu wa uongozi wa 'Wanalambalamba' hao, usajili huo ni mapendekezo ya Kocha Mkuu, Aristica Cioaba.

Baada ya kukabidhiwa jezi rasmi na Ofisa Mtendaji Mkuu wa Azam FC, Abdulkarim Amin 'Popat', Hamdoun alieleza kufurahishwa na kujiunga na timu hiyo.

Hamdoun alisema ana furaha ya kujiunga na Azam FC, huku akiahidi kushirikiana vema na wachezaji wenzake ili kuipa mataji timu hiyo.

Huo utakuwa usajili wa kwanza kwa timu hiyo katika dirisha hili dogo lililofunguliwa Desemba 15, mwaka jana huku likitarajiwa kufungwa Jumatano ijayo.

# Kaseja kurejea dimbani Februari

**Na Mwandishi Wetu**

GOLIKIPA wa KMC inayoshiriki Ligi Kuu Bara na Timu ya Taifa (Taifa Stars), Juma Kaseja, amesema anatarajia kurejea tena uwanjani mapema mwezi ujao.

Kaseja alifanyiwa operesheni ya goti la mguu wa kulia hivi karibuni, baada ya kubainika kuwa na uvimbe, siku chache kabla ya kuanza kwa mashindano ya Kombe la Chalenji Desemba mwaka jana.

Akizungumza na gazeti hili jijini Dar es Salaam jana, Kaseja alisema anaendelea vema na tayari ameanza mazoezi 'maalumu' chini ya madaktari wa Taifa Stars.

Kaseja alisema anamshukuru Mungu, amewahi kupata matibabu kabla ya tatizo lake kuwa kubwa na hivyo anatarajia kurejea uwanjani katika mechi za Ligi Kuu Bara hivi karibuni.

"Namshukuru Mungu niko vizuri, sina maumivu, na nimeshaanza mazoezi maalumu, kurudi uwanjani kamili hadi Februari," alisema kipa huyo wa zamani wa Simba, Yanga na Moro United.

Kaseja aliisaidia Taifa Stars kukata tiketi kucheza fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika kwa Wachezaji wa Ndani (CHAN), zitakazofanyika Aprili mwaka huu.

# KUWAONA U-17 WANAWAKE BURE

**Na Mwandishi Wetu**

SHIRIKISHO la Soka Tanzania (TFF), limesema mashabiki watakaokaa kwenye eneo la mzunguko katika mechi ya kusaka tiketi ya kushiriki fainali zijazo za Kombe la Dunia kati ya Timu ya Vijana ya umri chini ya miaka 17 ya Tanzania dhidi ya Burundi itakayochezwa Jumapili kwenye Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam ni bure.

Katibu Mkuu wa TFF, Wilfred Kidao, alisema lengo la kutotoza kiingilio katika eneo hilo ni kuongeza hamasa ya mashabiki kujitokeza kwa wingi uwanjani kuwashangilia wachezaji wao.

Kidao alisema kuwa kiingilio cha juu katika eneo la VIP A ni Sh. 5,000 wakati kwa upande wa VIP B ni Sh. 1,000.

"Tumeamua kuhamasisha kupitia viingilio hivi ili kuvutia watu wa aina mbalimbali hususani kina dada na wanawake, mara nyingi timu za wanawake zimekuwa hazituangushi," alisema Kidao.

Aliongeza kuwa kamishna wa mchezo huo kutoka Madagascar aliwasili nchini jana huku waamuzi kutoka Kenya wanatarajiwa kutua leo jijini Dar es Salaam.

# Michezo

Ijumaa Januari 10, 2020

Nipashe




## Fernandinho kupata mkataba mpya City

HABARI UK 30



Kiungo mpya wa Simba, Luis Miquissone (kulia), akipambana kuwania mpira dhidi ya beki, Shomary Kapombe katika mazoezi ya timu hiyo kwenye Uwanja wa Amaan Zanzibar juzi. **PICHA: ISAAC KIJOTI**

# SIMBA, AZAM NGOMA NZITO

●●● Makocha waahidi mawili mawili, mmoja soka la akili na kimwili, mwingine ufundi na utaalamu, huku...

**Na Isaac Kijoti, ZANZIBAR**

BAADA ya nusu fainali ya kwanza kati ya Yanga na Mtibwa Sugar kushuhudiwa jana usiku katika Uwanja wa Amaan, mtifuano mkali wa wanafainali wa mwaka jana wa Kombe la Mapinduzi, Simba na Azam FC utashuhudiwa leo.

Katika fainali ya michuano hiyo iliyopigwa mwaka jana kwenye Uwanja wa Gombani Kisiwani Pemba, Azam iliibuka na ushindi wa mabao 2-1 na kufanikiwa kutetea ubingwa huo.

Hivyo, Simba ambayo katika mchezo huo haikuwa na nyota wake wa kikosi cha kwanza, katika mechi ya leo itakayopigwa Uwanja wa Amaan saa 2:15 usiku, itahitaji kulipa kisasi huku Azam ikipania kuendeleza ubabe na kutetea ubingwa wao.

Wakizungumza na waandishi wa habari katika ukumbi wa mikutano wa Uwanja wa Amaan visiwani hapa jana, makocha wa timu hizo kila mmoja alikiri mchezo huo utakuwa mgumu.

Kocha Msaidizi wa Simba, Selemani Matola, alisema itakuwa ni mechi ngumu kwa kuwa Azam imewekeza katika mchezo huo na inacheza soka la kiushindani.

Matola alisema wamejiandaa vizuri na mashabiki watarajie soka safi la kutumia akili na kimwili zaidi tofauti na mechi ya awali dhidi ya Zimamoto.

Matola alisema tayari wachezaji walioanza kikosi cha kwanza dhidi ya Yanga kwenye mechi ya Ligi Kuu Bara ambao walibaki jijini Dar es Salaam wamewasili tangu juzi na kuungana na wenzao.

Alipoulizwa kuhusu uwezekano wa kuwapo mabadiliko katika kikosi kilichoivaa Zimamoto, Matola alisema "Ndiyo, mechi ni nyingi lazima kuwapo na mzunguko wa wachezaji ili waweze kupumzika.

"Lakini kutokana na suala la kiufundi, tunajua Azam ni timu nzuri na wanataka kutetea ubingwa wao, na sisi tunachotaka ni kutwaa kombe."

Naye Kocha wa Makipa wa Azam FC, Iddi Aboubakar, alisema wanaiheshimu Simba ni timu kubwa, lakini wao wamekuja kupambana na wanatarajia mechi hiyo itakuwa ni yenye ufundi mkubwa na utaalamu wa hali ya juu kwa kila upande.

Alipoulizwa mashabiki watarajie kuona Azam ikipata tena tabu ya ushindi kama ilivyoshinda kwa mbinde dhidi ya Mlandege, Abubakar alisema utakuwa mchezo tofauti kabisa.

"Unajua mechi ya kwanza kwenye mashindano yoyote mara nyingi timu inaanza kwa kujisuasua, lakini mashindano yanavyoendelea wachezaji nao wanabadilika.

"Halafu tambua unapocheza na timu ndogo nazo zinakamia sana, lakini mchezo dhidi ya Simba utakuwa wa kiufundi na kiutaalamu zaidi," alisema.

Simba imetinga nusu fainali baada ya kuitoa Zimamoto kwa mabao 3-1 katika mechi ya Kundi B, wakati Azam iliyokuwa Kundi A, iliitoa Mlandege kwa bao 1-0.

Fainali ya michuano hiyo inatarajiwa kupigwa Jamatatu saa 2:15 usiku katika Uwanja wa Amaan.

## Kocha mzungu atua Jangwani

**Na Mwandishi Wetu**

ALIYEKUWA Kocha Mkuu wa Black Leopard ya Afrika Kusini, Mbelgiji Luc Eymael, amewasili nchini tayari kuanza kuifundisha Yanga inayoshiriki Ligi Kuu Tanzania Bara, imefahamika.

Kocha huyo atua nchini kuchukua mikoba iliyoachwa na Mkongomani Mwinyi Zahera, ambaye nafasi yake ilishikiliwa kwa muda na Boniface Mkwasa.

Ofisa Habari wa Yanga, Hassan Bumbuli, alisema baada ya kuwasili nchini, watakamilisha mazungumzo haraka ili aweze kuanza kazi ya kukinoa kikosi hicho kinachopambana kuwania ubingwa wa Ligi Kuu Bara.

Bumbuli alisema wanaamini ujio wa mbelgiji huyo utasaidia kufikia malengo ya klabu hiyo kwa msimu huu, baada ya kuimarisha kikosi chao katika dirisha dogo la usajili.

"Ni furaha yangu kuona nimepata timu kubwa ndani ya Afrika. Ninaitambua vema falsafa yake na namna ilivyo, hivyo nina imani tutakwenda nayo sawa," alisema kwa kifupi Eymael baada ya kuwasili.

Baadhi ya timu alizowahi kufundisha kocha huyo ni AS Vita ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC), Missile (Gabon), AFC Leopard (Kenya), Rayon Sport (Rwanda, JS Kairouan (Tunisia), El Merreikh (Sudan), Polokwane City na Free State Stars za Afrika Kusini.

## Karia aendelea kung'ara Afrika

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS wa Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), Wallace Karia ameteuliwa kuwa Mjumbe wa Kamati Maalum ya kufanyia marekebisho mfumo wa Vyama vya Mpira wa Miguu vya Kikanda barani Afrika (AZA).

Kamati hiyo imeundwa baada ya kikao kati ya Shirikisho la Kimataifa la Soka (Fifa), Shirikisho la Soka Afrika (Caf) na AZA kilichofanyika hivi karibuni jijini Zurich, Uswisi na kuongozwa na Rais wa Fifa, Gianni Infantino.

Wajumbe wengine wa kamati hiyo itakayoongozwa na Rais wa Caf, Ahmad Ahmad ni Katibu Mkuu wa CAF, Mouad Hajji, Mario Gallavotti kutoka FIFA, na Rais wa Shirikisho la Soka la Niger (NFA), Hamidou Djibrilla.

Mbali ya mfumo, kamati hiyo itaangalia maeneo mbalimbali kama utawala, waamuzi, makocha, mashindano, ushirikiano na ofisi za kanda za Fifa katika kuendeleza mpira wa miguu.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002